**6 MEI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 6 Mei, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZA ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Waziri.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 225

**Hitaji la Gari la Wagonjwa na Watumishi**
**Kituo cha Afya Budushi, Kwimba**

**MHE. MARY F. MASANJA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka Gari la Wagonjwa na Watumishi Kituo cha Afya Budushi Wilayani Kwimba?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Mheshimiwa Zainab Katimba.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuajiri watumishi wa Kada ya Afya na kuwapeleka kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kote nchini. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya watumishi 9,384 waliajiriwa na kupangiwa kazi katika vituo vya kutolea huduma katika halmashauri, ambapo jumla ya watumishi 32 wa afya walipangwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba. Kituo cha Afya Budushi kina jumla ya watumishi 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 ilinunua magari *594*, *ambulances 382* na magari ya usimamizi wa huduma za afya 212, katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba imepokea magari matatu ya kubebea wagonjwa na kupelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kwimba, Kituo cha Afya Malya na Kituo cha Afya Kadashi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa dharura zinazotokea kwenye Kituo cha Afya Budushi zinahudumiwa na gari la kubebea wagonjwa lililopo Hospitali ya Sumve *(VAH),* ambayo ipo umbali wa kilomita moja. Serikali itaendelea kutenga bajeti, kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa na kuajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Masanja, tafadhali.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kwa kunipa nafasi hii. Kwanza niipongeze Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo imejenga majengo mazuri ya vituo vya afya, na leo hii wananchi wanaendelea kuyatumia. Kwa hiyo, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Kituo cha Afya cha Budushi kinahudumia zaidi ya wananchi 80,000 ambao ni wa Tarafa ya Ngulla. Wananchi hawa wanatumia Kituo cha Afya cha Budushi, lakini kituo hiki hakina gari la wagonjwa, gari ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri analiongelea ni la hospitali ya *mission* ambalo wananchi wanalipia. Hivyo, naiomba Serikali ipeleke gari pale ili hawa wananchi zaidi ya 80,000 waweze kuhudumiwa kwa huduma bora na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kituo cha Afya cha Budushi hakina mtumishi wa maabara na watumishi wengine mbalimbali. Tunatambua ya kwamba, mgonjwa yeyote anapoenda hospitali, cha kwanza kabisa ni lazima apimwe afya na pale hakuna mtumishi wa maabara. Naiomba Serikali impeleke mtumishi pale mara moja ili wananchi hawa wapate huduma iliyo bora, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nipokee maombi ya Mheshimiwa Mary Francis Masanja. Maombi haya yanatokana na nia yake ya kuona kwamba wananchi, ikiwemo wanawake kutoka katika Mkoa wa

Mwanza na Wilaya ya Kwimba wanapatiwa huduma nzuri za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita inafanya uwekezaji mkubwa sana kwa upande wa afya msingi na ndiyo maana katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, zaidi ya shilingi trilioni 1.29 zimewekezwa kwenye upande huu wa afya msingi. Tayari magari ya kutolea huduma ya kubeba wagonjwa *(ambulances)* 382 yamenunuliwa na kusambazwa kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mary Masanja kwamba, tutazingatia uhitaji huu wa gari la kuhudumia wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Budushi. Serikali itatafuta fedha ili iweze kununua gari hilo na kulileta kwa ajili ya kuwahudumia wananchi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mtumishi wa maabara, Serikali ya Awamu ya Sita katika uwekezaji wake kwenye sekta hii ya afya msingi katika kipindi cha mwaka 2021/2024 imeajiri watumishi 25,936 wa kada ya afya na bado mwaka 2024 vibali vilitolewa na Serikali kwa ajili ya kuajiri watumishi zaidi ya 8,000 katika kada hii ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutazingatia katika ajira hizi mpya kumpanga mtumishi wa kwenda kutoa huduma katika maabara kwenye Kituo hiki cha Afya cha Budushi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunaishukuru Serikali kwa kujenga vituo vingi vya afya kwenye Wilaya ya Tanganyika. Swali langu la msingi ni kwamba, kwa kuwa, Serikali imejenga vituo vya afya, na vingi havina magari ya kubebea wagonjwa, ni lini Serikali itapeleka gari kwenye vituo vya afya, Tarafa ya Karema, Mwese na Kabungu, eneo la Mishamo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea kuimarisha huduma za afya na hasa huduma ya afya msingi. Ndiyo maana katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, siyo tu Serikali imejenga hospitali za halmashauri 129, pia imejenga vituo vya afya 367.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa muktadha wa swali la Mheshimiwa Kakoso kuhusiana na kupeleka magari ya kubebea wagonjwa *(ambulance),* tayari Serikali imeshanunua magari hayo 382 na kuyasambaza kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba bado kuna uhitaji mkubwa sana wa kuendelea kununua na kusambaza magari hayo ili yaweze kutoa huduma bora zaidi ya afya msingi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea kutafuta fedha inunue magari haya ya kuwabebea wagonjwa *(ambulance)* na kuweza kuyasambaza kote nchini, ikiwemo kwenye jimbo lake katika Wilaya ya Tanganyika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa vile tuna saa moja tu ya maswali, Waheshimiwa Mawaziri tunaomba mpunguze muda ambao mnatumia kujibu maswali. Mjibu kwa kifupi kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Ndakidemi, tafadhali.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza, nianze kwa kumpa pole Mkuu wangu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mheshimiwa Nurdin Babu, pamoja na Mkuu wa Wilaya, Godfrey Mnzava, wananchi wa Mbokomu na familia zilizopata msiba kwa ngema ambayo imeua watu watatu, kwa tukio lililotokea jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niulize swali lifuatalo: Zahanati ya Funduhu katika Kata ya *Old* Moshi Mashariki ina uhaba mkubwa wa maabara pamoja na vifaa tiba. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia wananchi

wanaopata huduma katika zahanati hii ili waweze kupata huduma kutoka kwenye Serikali yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtaarifu Mheshimiwa Profesa Ndakidemi kwamba, Serikali katika kipindi cha miaka minne imeongeza mara dufu bajeti kwa ajili ya kununua vifaa na vifaa tiba katika vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali ya Awamu ya Sita inaingia madarakani ilikuta bajeti kwa ajili ya kununua vifaa na vifaa tiba ni shilingi bilioni 35, lakini wakati huu tunaozungumza, bajeti ile imepanda maradufu hadi kufikia shilingi bilioni 181.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuhakikishie kwamba, fedha zipo kwa ajili ya kununua vifaa na vifaa tiba. Nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwagiza *RMO* pamoja na *DMO* wakishirikiana na Mkurugenzi kusimamia na kuhakikisha kwamba, vifaa na vifaa tiba vinapatikana kwa sababu, fedha ipo na inapatikana kwa ajili ya kwenda kutoa huduma bora zaidi katika zahanati hii aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na jengo la maabara, Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba, inaboresha miundombinu katika sekta ya afya kwa kuendelea kujenga majengo ya kutolea huduma za afya msingi, ikiwemo zahanati. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali kupitia fedha za mapato ya ndani na kupitia fedha kutoka Serikali Kuu itaendelea kuhakikisha inaimarisha miundombinu ya kutolea huduma ya afya msingi na itakuja kufika katika jimbo lako, kwa ajili ya ujenzi wa maabara katika zahanati hii aliyoitaja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Tunaishukuru sana Serikali kwa

kutujengea Kituo cha Afya Mkulwe. Je, ni lini tutapata gari la kubebea wagonjwa kwenye Kituo cha Afya Mkulwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imenunua magari 382 ya kubebea wagonjwa na kuyasambaza kote nchini, lakini Serikali inatambua bado kuna uhitaji wa magari haya *(ambulance)*. Serikali inaendelea kutafuta fedha ili iweze kuendelea kununua magari haya na kuendelea kuyasambaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Condester Sichalwe kwamba, katika kituo cha afya alichokitaja, Serikali itatafuta fedha inunue gari hili la kubebea wagonjwa ili iweze kulileta katika kituo hicho cha afya ili huduma za afya msingi katika jimbo la Mheshimiwa Mbunge ziweze kuimarika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Wilaya ya Nkasi ni miongoni mwa wilaya zilizobahatika kupata gari la wagonjwa, lakini jiografia ya Wilaya ya Nkasi ni mbaya sana. Serikali mna mkakati gani wa kupunguza vifo vya wanawake, hasa wajawazito, kwa kuwapelekea gari karibu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari mpaka wakati huu imeshanunua magari 382 ya kubebea wagonjwa na kusambazwa kote nchini kwa ajili ya kuhakikisha kwamba huduma za afya msingi zinaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Aida kwamba tunatambua kuna umuhimu mkubwa sana wa kuendelea kupeleka magari haya ya kubebea wagonjwa katika jimbo lake kwa sababu, kama alivyosema mwenyewe, magari

haya pia kwa kiasi kikubwa yanatumika kuwasaidia akina mama wajawazito pindi wanapokuwa wamepata dharura kuweza kuwatoa kwenye kituo kimoja kuwapeleka kwenye kituo kingine, kwa ajili ya kupata huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Aida kwamba Serikali inatambua umuhimu huo, ndiyo maana inatafuta fedha ili ziweze kununua magari mengine ya nyongeza baada ya haya 382 kununuliwa kwa ajili ya kuendelea kusambazwa katika vituo vyetu, na kwenye Jimbo la Nkasi tutafika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mnivumilie, tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, sasa aulize swali lake.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba kuipongeza na kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Jemedari wetu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu, hospitali ya wilaya tayari tulishapokea *ambulance* kwa ajili ya kutoa huduma ya wagonjwa. Pia…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nikuombe radhi, zima *mic* kidogo. Utaanza kuuliza swali, halafu baadaye utatoa pongezi, karibu.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namaanisha sitauliza swali hili kwa sababu, tayari tulishapokea *ambulance* ile, ndiyo maana namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tunduru Kaskazini tunamwahidi muda ukifika hatutaipoteza kura hata moja kwa jambo jema lile na makubwa mengi aliyotufanyia. Tunamwahidi kutokupoteza kura hata moja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, ahsante sana.

*(Hapa Swali Na. 226 Liliondolewa na Muuliza Swali)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, swali hili halijaulizwa, kwa hiyo, halitakuwa na maswali ya nyongeza, poleni sana. Nadhani tunafahamu utaratibu na kanuni. Swali halijaulizwa, poleni sana wale ambao mlikuwa na maswali ya nyongeza kwenye swali hili.

Tunaendelea na Swali Na. 227, Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Mgharibi, sasa alize swali lake.

Na. 227

**Ujenzi wa Vituo vya Kuegesha Malori Nyakahura na Biharamulo Mjini**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga vituo vya kuegesha malori katika maeneo ya Nyakahura na Biharamulo Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ilitoa shilingi milioni 20 kwa ajili ya kuanza matengenezo ya awali ya usawazishaji wa eneo na ujazaji wa kifusi katika maegesho ya malori Nyakahura. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025 halmashauri imetenga shilingi milioni 15 kwa ajili ya ujenzi wa choo. Maegesho haya yataanza kutumika kabla ya mwezi Julai, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ujenzi wa maegesho ya malori Biharamulo Mjini. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, halmashauri imetenga shilingi milioni tano kwa ajili ya kupima na kuandaa nyaraka za umiliki wa eneo lililopatikana katika Kata ya Nyamahanga kwa ajili ya ujenzi wa maegesho hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini ninazo hoja mbili. Kwanza, kwenye hii ya ujenzi wa Kituo cha Malori cha Nyakahura ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Alitoa maelekezo tarehe 21, mwezi wa tisa, 2021 alipotembelea Wilaya ya Biharamulo. Wakati anaenda Ngara, alisimama Nyakahura pale, akatoa maelekezo tutafute eneo, kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa eneo tayari tumeshalipata na hiki kinachosemwa siyo ujenzi. Ujenzi wa *standard parking* ya malori unaenda *3.4 billion*. Sasa hapa tumetafuta eneo, tumesawazisha kwa sababu, barabara hii kutoka Lusahunga kwenda Benako iko kwenye ujenzi. Sasa kuondoa adha kwa wananchi imebidi itafutwe hii kwa ajili ya kupaki malori, lakini siyo *standard parking* yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu ni maelekezo ya Waziri Mkuu, na Naibu Waziri yuko hapa, na kwenye ziara ile aliambatana na watu wa TAMISEMI; naomba sasa Waziri aelekeze Halmashauri ya Biharamulo kupitia kwa Mkurugenzi na *RAS* wa Kagera waandae lile andiko haraka liletwe kwa ajili ya wananchi wale wa Nyakahura kuweza kuandikiwa mradi ule wa kimkakati na kupata hii huduma ambayo ina-*cost almost* 3.4 *billion*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, habari ya Biharamulo Mjini, tunategemea baada ya *SGR* kukamilika na kwa sehemu kubwa mizigo mingi inayoelekea Uganda na maeneo mengine itashushiwa Isaka. Sasa Biharamulo *is the last point* kama unataka kuingia kwenye Pori la Kasindaga. Kwa hiyo watu wengi wana-*opt* kulala Biharamulo Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili linalosemwa, ni nje kidogo ya mji, na hivyo huwezi kulazimisha madereva walale kule ambako unakutaka wewe. Hii ni biashara. Sasa naomba, kwa sababu tayari maeneo yapo pale Biharamulo Mjini, TAMISEMI kupitia kwa Waziri, wako tayari kuelekeza andiko jipya lingine kwa ajili ya kupaki malori Biharamulo Mjini ili watu ambao

wanakimbizana kwenda Kazindaga walale pale kwa ajili ya kutoa huduma na waweze kutoa huduma ndani ya Biharamulo Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ni maombi tu unaweza ukajibu ndiyo au hapana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ezra John Chiwelesa amekuwa akifanya jitihada kubwa sana ya kusemea miradi ya kimkakati katika jimbo lake. Hii siyo miradi ya mwanzo ambayo anaizungumzia, kwa maana ya kimkakati. Miradi hii inayoibuliwa ni miradi inayowezesha kimapato halmashauri au mamlaka zetu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii miradi inajengwa kwa taratibu mbili. Kwanza ni kupitia mapato ya ndani ya halmashauri pia kupitia Serikali Kuu. Serikali Kuu pia na yenyewe inaongeza fedha kuhakikisha kwamba baadhi ya miradi hii inaweza kupata fedha na kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa miradi hii miwili naomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwagiza Mkurugenzi afanye tathmini ya *viability* ya miradi hii miwili, na akijiridhisha waweze kuandika andiko ambalo litakuja Ofisi ya Rais, TAMISEMI na sisi tutalipeleka Tume ya Mipango. Tume ya Mipango wakishali-*approve* litakwenda Wizara ya Fedha kwa ajili ya upatikanaji wa fedha kutenga bajeti kwa ajili ya kuanza kujenga miradi hii ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kauli yangu kwa leo iwe hiyo kwa Mheshimiwa Ezra John Chiwelesa ambaye kwa kweli anapambania sana miradi ya kimkakati kwenye jimbo lake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani Mbunge wa Ushetu sasa aulize swali lake.

Na. 228

**Kumaliza Mgogoro wa Mpaka wa Shinyanga na Tabora**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza: -

Je, Iini Serikali itamaliza mgogoro wa mpaka wa Shinyanga na Tabora katika eneo la Ushetu na Kaliua ambao umechukua muda mrefu sana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa tafsiri ya ardhini ya Matangazo ya Serikali ya uanzishwaji wa Wilaya ya Kahama Mkoani Shinyanga na Kaliua Mkoani Tabora, hakuna mgogoro wa mpaka kati ya mikoa hiyo miwili. Mgogoro uliopo wa mpaka ni kati ya Hifadhi ya Msitu wa Mto Igombe unaomilikiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS)* na msitu wa Hifadhi wa Ushetu Ubagwe unaomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro huo umetokana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS)* kuweka alama za mipaka kwenye eneo la Hifadhi ya Msitu wa Ushetu Ubagwe uliopo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu Mkoani Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa mujibu wa Matangazo ya Serikali ya uanzishwaji wa Hifadhi ya Msitu wa *Igombe River,* Tangazo la Serikali Na. 32 la mwaka 1958 na Hifadhi ya msitu wa Ushetu Ubagwe, Tangazo la Serikali Na. 442 la mwaka 1958 hakuna mwingiliano wa mipaka kati ya hifadhi hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS)* itaendelea kuhakikisha Hifadhi ya Msitu wa *Igombe River* inabakia kwenye mipaka yake kama ilivyo kwenye Tangazo la Serikali Na. 32 la mwaka 1958 la uanzishwaji wa hifadhi hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Peter Chereheni.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali, kwanza mimi niseme kwamba, mgogoro upo na hata kipindi Mheshimiwa Rais ameteua wale Mawaziri wanane waliokuja Shinyanga, Mkoa ulitoa taarifa juu ya mgogoro huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilifikia hatua wananchi wangu zaidi ya 17 wakakamatwa kimakosa wakiwa na vibali na mali zao zikataifishwa zikapelekwa Kaliua na kuna kipindi ilifikia hatua kati ya Askari wa *TFS* upande wa Kaliua na wa Halmashauri yetu ya Ushetu wakakutana pale kwenye mipaka baada ya kuona mipaka ya Hifadhi ya Igombe ilihamishwa kuja kwenye eneo la Ushetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamishna wa Ardhi aliagizwa na alishafika akafanya tathmini na timu yake yote ya kusoma kutafsiri upya ramani. Kilichokuwa kimebakia ni Waziri kuja kutangaza tu mipaka ikae wapi? Naomba kujua, ni lini Mheshimiwa Waziri wa Ardhi atakuja kutafsiri na kusoma mipaka ili kuondoa mwingiliano uliopo kwa wananchi wangu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli historia aliyoitoa Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, kwamba kumekuwa na changamoto ya tafsiri ya mipaka katika eneo la Hifadhi ya Msitu wa *Igombe River* pamoja na Hifadhi ya Msitu wa Ushetu Ubagwe. Hifadhi moja ikiwa iko chini ya *TFS* na hifadhi nyingine ikiwa ipo chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu. Kama yeye mwenyewe alivyotoa historia, jambo hili limefanyiwa kazi na kufikia ukingoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamana ya tafsiri ya mipaka ya ardhi ikiwemo mpaka kati ya Hifadhi hii ya *TFS* na Hifadhi hii ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ipo chini ya Wizara ya Ardhi. Tayari Mheshimiwa Waziri wa Ardhi suala hili analifahamu, na kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Waziri

ataweza kulishughulikia aweze kupitia Wizara ya Ardhi kutoa tafsiri ya mipaka na kuweza kukamilisha kabisa kumaliza huu mgogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ndilo ninaloweza kumjibu Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, akae na amani, Serikali ipo kazini na itakuja kutatua mgogoro huu katika jimbo lake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri pia kuna nyongeza kutoka kwa Naibu Waziri wa Ardhi, karibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba swali hili lilikuwa lielekezwe kwenye Wizara yetu kwa sababu lina *mechanism* ya kiutendaji. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, baada ya maswali na majibu, tutakutana ili tuweze kulijengea hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba lilishafanyiwa kazi kwa kiasi kikubwa sana, na hivyo baada ya kipindi cha maswali na majibu tutakutana na mhusika ili tuweze kuyajenga vizuri kuyafikisha kwenye eneo halisi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Pinda, tunakushukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 229

**Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ambayo yanachangia uharibifu wa mazingira?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Muungano na Mazingira, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeandaa sera, mikakati, kanuni, miongozo na mipango ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi: Sera ya Taifa ya Mazingira (2021); Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (2021-2026); Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022–2032); na Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni za mwaka 2023 ambazo zinasomwa pamoja na Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni za mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imendeelea kuwahamasisha wananchi kuacha shughuli zinazochangia uharibifu wa mazingira, zikiwemo kukata miti ovyo, kuepuka kilimo kisicho endelevu katika vyanzo vya maji, kuepuka ufugaji unaochangia uharibifu wa mazingira na uvuvi haramu. Aidha, kuachana na matumizi ya nishati ya kuni na mkaa kwa taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 na kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kuweza kuchangia katika utunzaji wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushauri wangu kwa Serikali, kwamba Serikali iwahishe mchakato wa mipango kabambe ili kuweza kunusuru hali ya mabadiliko ya tabianchi iliyopo kwa sasa, ambayo ni hatarishi kabisa.

(a) Je ni kiasi gani Serikali imejipanga kutoa elimu kwa wananchi ili kunusuru hali ya hatari ya mabadiliko ya tabianchi inayoendelea sasa?

(b) Pamoja na mikakati mingine mingi mizuri ya Serikali je, Serikali ni kwa kiasi gani imejipanga kuhakikisha kwamba inatoa miche ya miti kwa Watanzania wote ili waweze kwenda kupanda na kuweza kukabiliana na hali ya mabadiliko ya tabianchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, Mama Msongozi kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye tasnia hii ya mazingira, hasa suala la mabadiliko ya tabianchi. Hivi karibuni nimemshuhudia katika vyombo vya habari akiwa anagawa mitungi ya gesi zaidi ya 2000. Pia nimeshuhudia akipanda miti, maana nami nilishiriki kule mkoani kwake kwenda kupanda miti. Nimpongeze sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya kutoa elimu ipo na ilishaanza na ipo endelevu, na hivi tunavyozungumza tunaendeleeanayo. Tunao mpango wa kuendelea kutoa elimu kuhusu masuala ya usimamizi wa vyanzo vya maji, hasa kwenye changamoto ya kuzingatia sheria ya mita 60. Hii imekuwa ni changamoto sana, kwa hiyo, tunaendelea kutoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la utunzaji wa taka na uhifadhi wa taka, kwa sababu bado imekuwa ni changamoto na bado wananchi wengi hawajafahamu kwamba taka ni fursa, tunayo jitihada ya kutoa elimu kuhusiana na suala la upandaji wa miti na masuala mengine ya kuishughulikia miti, kwa sababu watu wengi wamekuwa wanapanda miti, lakini kwenye kuishughulikia imekuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, utunzaji wa fukwe na visiwa, kama mnavyojua, bado kuna changamoto ya bahari kuwa zinakula visiwa na hatimaye visiwa vile vinapotea. Kwa hiyo, tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kufahamu hilo. Huo ndiyo mpango tulionao katika elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kutoa miti bure, ni kweli kwamba tumekuwa tukiuza baadhi ya miti kupitia taasisi

inayosimamia miti, ingawa kuna baadhi ya miti ambayo ni ya kimkakati, huwa ni miti ambayo inatolewa bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa wito kwa taasisi zote au watu binafsi ambao wanatengeneza vitalu kwa ajili ya miti ya kupanda, basi watafute namna ambavyo wanaweza wakawasaidia wananchi kuweza kupata miti bure kwa kuwa huwa inauzwa ili kushughulikia gharama za uendeshaji, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza: -

Je, Serikali ina kauli gani kuhusiana na kuwashirikisha wanawake, hasa wale wa pembezoni katika kuandaa mipango na mikakati ya kukabiliana na tabianchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya miongoni mwa jambo ambalo Serikali haimwachi mtu yeyote, ni suala la kupambana dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tumegundua kama Serikali kwamba miongoni mwa watu ambao ni waathirika wakubwa wa athari ya mabadiliko ya tabianchi ni wanawake na watoto, ndiyo maana Mama Samia Suluhu Hassan akaja na mkakati na sera ya masuala ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kumnusuru mama na binti na mambo mengine ya kimazingira, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Tunaelekea Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrew, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Protas.

Na. 230

**Kumaliza Kusambaza Umeme Kwenye Vitongoji**

**MHE. VENANT D. PROTAS K.n.y. MHE. JACQUELINE K. ANDREA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza kusambaza umeme kwenye vitongoji vyote nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* imekamilisha kupeleka umeme katika vitongoji 33,657 kati ya vitongoji 64,359 vilivyopo nchini. Aidha, vitongoji 30,702 bado havijafikiwa na huduma ya umeme, ambapo kati ya hivyo, vitongoji 7,736 tayari vipo katika hatua ya utekelezaji kupitia miradi mbalimbali; na vitongoji vilivyosalia 22,966 vitapatiwa umeme kwa kipindi cha miaka mitano kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Protas.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza naipongeza Wizara na Serikali kwa hatua kubwa ya vitongoji zaidi ya 30,000 kuwa vimefikiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu dogo la nyongeza ni kwamba, kwenye bajeti hii ambayo tunaendelea nayo, walituahidi Wabunge kila jimbo mtatupatia vitongoji 15 ikiwemo Jimbo la Igalula ambako tulipeleka orodha kila Mbunge vitongoji 15. Jimbo la Igalula tulipeleka kwenye vitongoji vya Nyapimbi, Makungu na kwenye maeneo mengine. Mpaka leo tunakwenda kumalizia ngwe ya bajeti hii, hakuna mkandarasi aliyanza ujenzi

wa vitongoji hivyo 15. Je, Serikali ina kauli gani kwa wakandarasi ambao wameshawapa mkataba na bado hawajaingia *site?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge. Katika miradi hii ya vitongoji 15 katika mikoa yote, tayari tumeshapata wakandarasi; na kwa kweli katika mikoa mingi wakandarasi wako *site,* walikuwa wanatafuta vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye baadhi ya mikoa tayari vitongoji hivi vimeshaanza kazi na baadhi, vifaa ndiyo vinakwenda. Kwa upande wa Igalula tutafuatilia kama kuna changamoto yoyote, na baada ya hapo tutaendelea kumsimamia mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto tuliyonayo ni kwamba, wakandarasi hawa wanafanya kazi katika majimbo yote kwenye mkoa. Kwa hiyo, *issue* inakuja pale kwenye kuanza kwenye jimbo moja baada ya nyingine, kwa sababu mkandarasi ana *scope* maalum ya utekelezaji wa mradi. Kulingana na muda, naomba Waheshimiwa Wabunge tuwape muda, wakandarasi wengi wako *site,* wana uwezo, na watawafikia kwenye maeneo yenu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Abubakar Damian Asenga Mbunge wa Kilombero sasa aulize swali lake.

Na. 231

**Kupunguza Mlima Mang'ula Kona – Kilombero**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapunguza Mlima Mang'ula Kona Kilombero ikiwa ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Mlima Mang'ula Kona ambalo liko Kilombero, kandokando mwa barabara ya Mikumi – Kidatu – Ifakara. Eneo hilo limeshafanyiwa ukaguzi na kazi ya usanifu ipo kwenye hatua za mwisho kwa ajili ya kupunguza ama kukata kipande cha mlima na uimarishaji wa kingo ili kuzuia maporomoko ya udongo wakati na baada ya kukata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kupunguza mlima itaanza mara tu baada ya kukamilika usanifu na kumpata mkandarasi wa kutekeleza kazi hiyo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa kweli kwa jambo hili, na leo wananchi wangu watakuwa na furaha kubwa kwa sababu lilikuwa ni jambo muda mrefu. Naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini ujenzi wa barabara kubwa ya *TANROADS* inayotoka Kikwawila – Mbasa – Katindiuka – Lipangalala – Daraja la Magufuli – Malinyi itaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tulikuwa tuna mkandarasi tumempata wa Barabara ya Ifakara – Mlimba kwa muda mrefu sana yule mkandarasi hajaanza kazi na ile barabara ina shida kubwa sana pamoja na daraja la Lumemo ambapo tulitarajia mkandarasi akianza atatusaidia kuweka ule mto vizuri ili wananchi wasipate mafuriko kama ambavyo wamepata jana. Je, ni lini huyu mkandarasi ambaye yuko Barabara ya Mlimba ambaye amekaa *site* muda mrefu ataanza ujenzi ule?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Asenga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Ifakara – Malinyi ni barabara ambayo inaenda mpaka Songea. Barabara hii hata katika bajeti yetu na tayari tupo kwenye mchakato sasa hivi mkandarasi tulishampata ambaye atajenga kilometa 112 ni kati ya zile barabara ambazo zilikuwa kwenye Mpango wa *EPC+F*. Kwa hiyo, hii barabara itajengwa, tutaanza na kilometa 112 kwa Mpango wa Sanifu, Jenga, kuanzia Ifakara – Lupilo hadi Mtimbira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara yake ya pili ya kutoka Ifakara kwenda Mlimba, tunajenga kilometa 100 ambazo tuna *lot* mbili. Wakandarasi wote wameshapatikana, na ambacho bado hakijakamilika, tumesham-*advance*, lakini tunaendelea kum-*advance* ili aanze kazi, lakini tayari ameshaanza kufanya *mobilization* wakati mkandarasi wa pili tunatafuta *advance* ili naye aweze kuanza kazi. Kwa hiyo, tuna hakika katika kipindi hiki ambacho mvua inakatika, wakandarasi wote watarudi *site*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape Nnauye.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya kukarabati Barabara ya Kusini kwa maana ya Barabara ya Dar es Salaam kwenda Lindi – Mtwara na kazi nzuri iliyofanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wizara ya Ujenzi ya ule ukarabati, naomba kuuliza swali dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni kwamba umefika wakati wa kuijenga upya barabara nzima badala ya kuendelea na ukarabati ambao kila mwaka tunaingiza fedha za walipakodi kukarabati; na barabara yote kwa kweli imeoza? Nadhani wakati umefika wa kuijenga upya barabara nzima ya kutoka Dar es Salaam – Lindi kwenda Mtwara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimhakikishie Mheshimiwa Nape, Wabunge wa Kusini, pamoja na Watanzania wote kwamba Barabara ya Dar es Salaam – Kibiti –

Lindi hadi Mingoyo, kweli ni barabara ambayo imechoka, lakini pia ni barabara ambayo imekuwa ikikumbwa sana na mafuriko. Kwa hiyo, tuna mipango mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kwanza ndiyo huo aliousema Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea kujenga madaraja kwa kiwango cha usanifu ambao upo madaraja ya kudumu yenye ukubwa ambao umesanifiwa kulingana na mafuriko yanayotokea. Kwa hiyo, wakandarasi wako *site* kwenye madaraja yote ambayo yamekuwa yanakumbwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa pili ni kwamba, maeneo yote ambayo yamechoka na yameainishwa, tutaanza kuyajenga. Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha bajeti, amesema kwamba kwenye vipande vile vikorofi vyote ambavyo vimeharibika sana tutaanza kuvijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hilo haitoshi kwa kuwa ni barabara yote tunaona imechoka. Mpango mkubwa ni kwamba hivi tunavyoongea sasa hivi, Wizara inatoa kipaumbele cha kwanza katika hiyo barabara na tuko kwenye mazungumzo na wenzetu wa *World Bank* ili kuijenga barabara yote. Huo ni mpango wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa pili, tuna mpango wa kuja na *infrastructure bond* ambayo tayari tumesham-*engage consultant* ili kupitia *Road Fund* kama tutapata ile *infrastructure bond,* basi kipaumbele pia ni kuijenga hiyo barabara yote. Kwa hiyo, tuna hakika katika hiyo mipango miwili ya kudumu ambayo itatupatia fedha za kuijenga barabara yote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda, sasa aulize swali lake.

Na. 232

**Ujenzi wa Barabara ya Mpomvu – Nyarugusu – Ulyang'ulu – Busanda**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza: -

Je, ujenzi wa Barabara ya Mpomvu kupitia Nyarugusu kwenda Bulyankulu kwa kiwango cha lami upo katika hatua gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mpomvu – Nyarugusu inajulikana kwa jina la Geita – Bukoli – Bulyankulu *Junction* (Ilogi) yenye urefu wa kilometa 61.2. Kwa sasa Serikali iko katika hatua za mwisho za manunuzi ya Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magessa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri Mheshimiwa Waziri yanayotia matumaini kwamba wako kwenye hatua za mwisho, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza: ni lini barabara ya kutoka Ushirombo kuja Katoro itajengwa kwa lami kwa sababu iko kwenye bajeti hususan kipande kile cha kutoka Nyikonga kuja Katoro? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, je, Waziri yuko tayari kuambatana nami kwenda Jimboni ili akazione barabara hizi na ajue, kwa nini tunaendelea kuzisema kila mwaka, kwa sababu zina uhitaji wa wananchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swali la pili, niko tayari kutembelea hizi barabara, na bahati nzuri hizi barabara ninazifahamu kwa sababu nimeshazitembelea. Kwa hiyo, kwa ajili

ya kwenda na Mheshimiwa Mbunge kukutana na wananchi, niko tayari tutakapokuwa tumepata ratiba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Ushirombo kwenda Katoro, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeshaanza kazi. Tumeanza na kilometa 5.3 kutoka Ushirombo hadi sehemu inayoitwa Bwenda, na mkandarasi ameshapatikana yuko kwenye hatua za awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kutoka Kashelo kwenda kwenye Daraja la Nyikonga pamoja na daraja lake, tunajenga kwa Mpango wa *World Bank* kupitia Mpango wa Rais na hivi sasa tuko hatua za manunuzi na eneo ambalo tutajenga hapo kama kilometa 10.4. Kwa hiyo, maeneo yaliyobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kukamilisha barabara yote yenye urefu wa kilometa kama 58. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya hoja za Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 233

**Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Ruvuma**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza: -

Je, kwa nini ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma umesimama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma unatekelezwa kwa awamu ambapo hadi sasa Serikali imetoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 3.3 na tayari jengo la huduma za mionzi limekamilika sambamba na kusimikwa mashine

ya *CT-Scan* na *Digital X-Ray* na tayari huduma zinatolewa. Aidha, ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje *(OPD)* unaendelea na jengo la kusafisha figo *(Dialysis)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma, na mradi huu unatarajiwa kukamilika katika awamu tatu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa katikati hapo mradi huu ulisimama na ukawa unatutia shaka na sisi tulikuwa tunataka huduma kwenye hospitali hiyo ya rufaa kwa sababu watu wanakwenda mpaka Mbeya au Dar es Salaam. Ni lini sasa Serikali itaharakisha ujenzi wa hospitali hiyo kwa awamu hizo zilizobakia ili tuweze kupata huduma pale pale Mkoa wa Ruvuma? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji huo, lakini kama ambavyo anajua, wana hospitali ambayo ina uwezo na ukubwa kama hospitali ya mkoa, lakini hospitali anayoizungumzia ni hospitali inayojengwa kwenye eneo jipya ili baadaye kuachia hii ambayo ipo sasa kuwa ni hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejenga katika awamu hizi tatu. Kabla ya mwisho wa mwaka wa bajeti ya 2025/2026, tutakuwa tumefika awamu ya pili, na itakuwa imebaki kazi ndogo sana ili kuweza kukamilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha, haya.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kutuletea *CT-Scan* katika Hospitali ya Wilaya ya Hai ambayo inahudumia pia wananchi kutoka Wilaya ya Siha? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuijali hospitali yake ya wilaya, lakini nimkumbushe tu kwamba hospitali yetu ya Mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi) tayari imesimikwa *CT-Scan*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua, unaposimika *CT-Scan* ni miundombinu, lakini hasa hasa siyo miundombinu, ni utaalamu. Yaani kwa maana ya madaktari wabobezi na kwa maana ya hospitali ya *level* ya wilaya, bado mkakati huo haujaanza kwa maana ya kutengeneza miundombinu, na pia kuweka wataalamu wenye uwezo wa kusimamia mashine hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sasa kwa wilaya yetu ya Siha na Wilaya yake kwa kutumia Hospitali ya Mawenzi na hata Hospitali ya Kibongoto ambayo ni kilometa chache kutoka kwenye Jimbo lake, mambo yataendelea kuwa mazuri kwa watu wa Hai.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Hospitali yetu ya Mkoa wa Manyara haina kabisa wodi kwa ajili ya wagonjwa wanaume na kwa ajili ya wagonjwa wanawake. Je, ni lini Serikali itakwenda kujenga wodi hizo ili huduma ziendelee kutolewa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mkoa wa Manyara ni hospitali ambayo kwa sasa, kwa kweli inafanya huduma kama Hospitali ya Mkoa. Hospitali ya Mkoa wa Manyara ilianza kama hospitali ikitumia jengo la mama na mtoto kama ndiyo sehemu ya *OPD*. Kwa hiyo, najua anachosema ni kwenye kuongeza wodi ya akina baba, lakini na wodi ya akina mama. Katika awamu hii, bajeti hii ya mwaka huu imetengwa shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kutazama kwenye huo mkoa wake kuona ni nini ambacho kina kasoro ili kiweze kujengwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 234

**Kurejesha Zao la Pamba Mikoa ya Kusini mwa Tanzania**

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurejesha kilimo cha pamba katika Mikoa ya Kusini mwa Tanzania?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mikoa ya Kusini mwa Tanzania ikiwemo Mkoa wa Mtwara, Lindi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Ruvuma hairuhusiwi kulima pamba kutokana na karantini iliyowekwa kufuatia uwepo wa funza mwekundu. Karantini hiyo iliwekwa tangu mwaka 1947 na kuhuishwa mwaka 2000 baada ya wakulima wa Halmashauri ya Chunya Mkoani Mbeya kuripoti uwepo wa funza huyo ambaye alisababisha uharibifu wa pamba kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, utafiti uliofanyika mwaka 2022 katika mikoa yenye karantini ulithibisha kuwa funza mwekundu bado yupo katika maeneo hayo. Hivyo, mikoa hiyo bado haijaruhusiwa kurejesha kilimo cha pamba kwa lengo la kudhibiti kusambaa kwa funza huyo katika maeneo mengine ya uzalishaji wa pamba nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima katika maeneo yaliyowekewa karantini wanashauriwa kuendelea kulima mazao mengine ikiwemo korosho, ufuta, alizeti, chai, mihogo, mahindi na mbaazi kulingana na ekolojia ya maeneo waliyopo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Angelina Malembeka, tafadhali.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya ziada. Kwanza namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake yaliyohusisha karantini ya mwaka 1947 ambapo ni miaka 51 iliyopita na kuhuishwa tena mwaka 2000, miaka 25 iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tuna vyuo vya kilimo ikiwemo Chuo Kikuu cha *SUA*, Morogoro; tuna Uyole, Mbeya; tuna Ukiruguru, Mwanza; Tengeru, Arusha; Naliendele, Mtwara; na vinginevyo. Kule tuna wataalamu wa kutosha na watafiti makini. Je, ndani ya miaka hiyo 51 hadi sasa wameshindwa kufanya utafiti na kupata suluhisho la kuondoa funza mwekundu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Ndani ya miaka hiyo 51 baada ya utafiti wa awali, kilimo cha mwaka 1947 ni tofauti na kilimo cha miaka hii ya 2020. Tuna tofauti kuanzia kwenye pembejeo za kilimo, vifaa, dawa, mbegu na hata usimamizi. Je, Serikali imejipangaje kuondoa tatizo hili ili zao la pamba lilimwe tena katika mikoa ya Kusini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nampongeza sana Mheshimiwa Malembeka kwa kazi nzuri ya kufuatilia kurejeshwa kwa zao la pamba katika mikoa ya Kusini. Nimthibitishie jambo moja kwamba, tafiti ni sayansi na sayansi inachukua hatua, ni mchakato *(process)*. Kwa hiyo, hatuwezi tukatoa matamko ya kisiasa kulazimisha vyuo vikuu ama taasisi zilizo chini yetu kwa mfano, hizo *TARI* alizozieleza kwamba jamani mwakani muwe mmemaliza tafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi jukumu letu ni kuhakikisha kwamba wanaendelea kutafuta teknolojia bora na ya kisasa, lakini vilevile, wanaendelea kufanya tafiti kwa kadiri ya utaratibu ambao wamejiwekea. Kwa hiyo, sisi kama Wizara ya

Kilimo tunatambua kwamba Chuo Kikuu cha *SUA* pamoja na Taasisi zetu za tafiti nchini bado wanaendelea na tafiti, na zitakapokamilika maana yake watatoa majibu na kukabiliana na huyu funza mwekundu ili tuweze kurejesha kilimo cha pamba katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwondoe tu shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi bado inaendelea, na utafiti kwa sababu ni sayansi, tuwaache wanasayansi waendelee kufanya hiyo kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa je, ni lini huo utafiti utakamilika ili wananchi wa vijiji vya Kata za Mjele na Kata za Ikukwa Wilaya ya Mbeya waweze kurudi na kulima pamba ili nao waweze kupata mapato kiuchumi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kama ambavyo nilijibu katika swali la nyongeza la mwuliza swali kwamba utafiti ni mchakato, tafiti ni sayansi na tafiti siyo masuala ya kutoa matamko. Kwa hiyo, siwezi kusema lini utafiti utakamilika. Tuwaache wanasayansi waendelee kufanya utafiti na shughuli hii itakapokamilika watatupa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, wapo katika hatua nzuri kwa sababu muda wote wako *site* kuhakikisha kwamba wanakabiliana na huyu funza mwekundu. Kwa hiyo, ninaamini kulingana na mabadiliko ya teknolojia, mwafaka utapatikana mapema iwezekavyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba zao la pareto linalimwa kwa ufanisi mkubwa hasa katika Mkoa wa Iringa Wilaya ya Kilolo, Wilaya ya Mufundi na Wilaya ya Iringa yenyewe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Moja ya zao ambalo sisi kama Serikali tunalipa kipaumbele sasa hivi ni pamoja na zao la pareto, na nchi yetu sasa hivi ni ya pili kwa uzalishaji wa pareto Afrika, nafikiri na duniani. Kwa hiyo, jukumu letu ni kuongeza kasi kwa kutoa elimu kwa wakulima ili waweze kuingia katika kilimo cha pareto hususan katika maeneo ambayo umeainisha kama Kilolo, Mufindi pamoja na Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaendelea kufanya hivyo kwa kutumia Maafisa Ugani na vyombo vya habari kuhabarisha umma juu ya umuhimu wa wakulima kuingia katika kilimo cha pareto. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru Serikali, imeshafanya utafiti Jimbo la Mbulu Vijijini kwamba linafaa kulima zao la vitunguu swaumu. Je, ni lini sasa wanapeleka fedha kujenga mabwawa yote ambayo tumekubaliana na ipo kwenye bajeti ya mwaka huu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba Mheshimiwa Flatei Massay anafahamu kwamba utaratibu wa bajeti katika nchi yetu ni *cash budget,* na kwa sababu tunatumia mfumo huo, ni kwamba sisi tunavyopewa fedha, tunazigawanya kwenda katika maeneo yote nchini ikiwemo katika Jimbo lake la Mbulu Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutaendelea kuleta fedha kuhakikisha mabwawa yote ambayo tumeyaainisha katika Jimbo la Mbulu Vijijini yanakamilika kwa wakati kulingana na jinsi ambavyo tumeyaweka katika mipango yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana. Tunaendelea swali linalofuata kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani

ya Nchi, Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 235

**Hitaji la Gari la Zimamoto – Kondoa**

**MHE. ALLY J. MAKOA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka gari la zimamoto Wilaya ya Kondoa ili kukabiliana na majanga ya moto yanayotokea mara kwa mara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuboresha utendaji kazi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika kulipatia vitendea kazi kupitia mradi wa ununuzi wa magari na vifaa vya kuzima moto na uokoaji wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 100 kutoka Kampuni ya *ADEX* iliyopo Dubai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo utawezesha kupatikana kwa vitendea kazi mbalimbali ikiwemo magari 150 ya kuzima moto na uokoaji yatakayotoa huduma katika Wilaya zote nchini ikiwemo Wilaya ya Kondoa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Makoa.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa majanga ya moto yameendelea kuharibu mali za wananchi, ni lini Serikali inatuahidi kutuletea haya magari ili kuwapa matumaini hawa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ili kuyatunza magari haya, nini mpango wa Serikali kuhakikisha maeneo yote yaliyotajwa yatafikiwa na gari hizi zitapata *parking* bora kwa ajili ya kuyahifadhi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Ally Juma Makoa kwamba, mradi huo tayari umeshatekelezwa na magari yameshanunuliwa, na awamu ya kwanza tayari yameshaingia hapa nchini. Awamu ya pili itaingia mwezi Agosti, 2025. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba gari litafika katika Halmashauri ya Kondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusu *parking*, nitoe rai kwa Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri ya Kondoa kwa kushirikiana na Kamanda wa Zimamoto wa Mkoa wa Dodoma kuhakikisha wanatenga eneo kwa ajili ya *parking* ya magari hayo yatakapowasili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kyerwa ina rekodi ya matukio ya moto ikiwa ni pamoja na shule ya watoto wadogo ambayo imewahi kuungua. Wakati huo huo tunategemea Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe kupata gari la zimamoto na ile ni wilaya inayokua kwa kasi. Nataka kujua mkakati wa haraka wa kuhakikisha ile wilaya ina gari la zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mji wa Nkwenda, lini itapatiwa gari la zimamoto kwa sababu ni mji unakua, ukiwa na *petrol station,* kuhakikisha kwamba tunaepusha majanga ambayo yamekuwa yakijitokeza kama siku zilizopita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, Serikali imeshaagiza magari 150 tayari kwa kusambazwa katika wilaya zote hapa nchini ikiwepo na Wilaya ya Kyerwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ninakushukuru sana.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya sasa aulize swali lake.

Na. 236

**Mradi wa Maji Miji 28 – Rorya**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza:-

Je, lini Mradi wa Maji Miji 28 Rorya - Tarime utakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Miji 28 wa Rorya - Tarime uliopo Mkoani Mara. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa dakio *(intake)* katika Ziwa Victoria lenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 29 kwa siku, ujenzi wa miundombinu yenye uwezo wa kutibu maji lita milioni 28 kwa siku, ulazaji wa bomba umbali wa Kilometa 90, ujenzi wa matenki yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 10 sanjari na ujenzi wa kituo kimoja cha kusukuma Maji *(booster station)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 12.5%, na kwa mujibu wa mkataba unatakiwa kukamilika mwezi Julai, 2025 na kunufaisha wananchi 460,885 waishio katika Wilaya za Rorya na Tarime, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru Serikali kwa ujenzi na utekelezaji wa huu Mradi wa Miji 28 kwa maana ya Rorya – Tarime na tuna imani utakapokamilika wananchi wengi wanakwenda kunufaika na mradi huu. Pamoja na kazi nzuri hiyo, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi zaidi ya Kata tatu kwa maana ya Nyamagaro, Nyamtinga na Kiangasaga ni

moja ya kata zinazozunguka chanzo cha maji eneo lilipojengwa chanzo hiki. Wananchi hawa waliridhia wakati chanzo kinajengwa kupisha maeneo yao bila kulipwa fidia yoyote na Serikali, ili iweze kulaza bomba na kujenga chanzo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijue, Serikali sasa haioni umuhimu wakati mradi huu ukiendelea, wananchi wa kata hizi waweze kunufaika na maji kabla ya mradi huu haujakamilika kwa 100% ili angalau eneo la chanzo wananchi hawa waanze kunufaika na mradi wa maji safi na salama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; chanzo cha maji cha Mradi wa Kinesi kinahudumia zaidi ya wananchi 20,000. Chanzo hiki kimeanza kutitia kwa sababu ya ongezeko la maji kwenye eneo hili na siyo salama kabisa kwa watoa huduma kwa maana ya maafisa wanapotoa huduma pale inapotokea changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nijue, Serikali haioni kuna umuhimu wa kutoa fedha na kubadilisha ujenzi mwingine wa chanzo hiki ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza, kwa sababu sasa hivi siyo salama na kimekaa muda mrefu na kiukweli kimechakaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni kuna umuhimu sasa wa kujenga chanzo hiki pembeni ili kunusuru madhara yanayoweza kutokea kutokana na changamoto ya chanzo hiki cha maji mradi wa Kinesi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, na pia namshukuru sana Mheshimiwa Jafari Chege, Mbunge wa Rorya, kwa namna ambavyo anaendelea kuwapigania wananchi na kwa namna ambavyo anaendelea kushirikiana na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Nyamagaro, Kiangasaga pamoja na Nyamtinga, kwanza kabisa ninawapongeza sana wananchi wa kata hizi kwa kujitolea na kuhakikisha kwamba

mradi huo unapita bila fidia yoyote, na ahadi ya Serikali bado ipo pale pale kwamba, mradi huu utawanufaisha wananchi wale ambao wapo kwenye chanzo. Pale ambapo chanzo kinapoanza, basi wananchi wa eneo hilo waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, umekuwa ni utaratibu wetu Wizara ya Maji kuhakikisha kwamba miradi ambayo haihitaji kukamilika kwa 100% kama kuna *existing infrastructures* ambazo zina uwezo wa kupokea maji ambayo tayari yameshazalishwa, basi haihitaji kusubiri mradi ukamilike kwa 100% ili wananchi wapate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Jafari, wananchi wake kabla mradi haujakamilika kwa 100% wataanza kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa swali la pili, chanzo chetu cha Kinesi kweli kimekuwa na changamoto. Hivyo, nitumie fursa hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji kumwelekeza *RM* Mkoa wa Mara kwenda kwenye chanzo hicho na kukikagua, kujiridhisha changamoto iliyopo kama itahitaji kukihamisha, basi Serikali itafanya hivyo na tutatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, wananchi hawapotezi hicho chanzo ambacho kimekuwa ni msaada kwao, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiwekeza katika vyanzo vipya vya maji ili kukidhi mahitaji ya maji kwa wahitaji hasa katika Jiji la Mwanza ikiwemo na Ilemela Manispaa. Wameanzisha chanzo cha maji Butimba, vilevile wamekarabati *Capri Point* na tayari wanakarabati Igombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyopo, ongezeko la watu linasababisha maji yasifike kwa watu kama ambavyo ilivyo kutokana na uchakavu wa miundombinu. Je, ni lini sasa Serikali

itabadilisha miundombinu chakavu ambapo kunakuwa na upotevu wa maji mengi, na wamejenga matenki kwa ajili ya kupokea maji na kusambaza lakini hayawafikii walengwa kama ambavyo ni kusudio la Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi Mheshimiwa Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, Mbunge wa Ilemela ni zuri, kwa sababu, kwanza kabisa miundombinu ikiwa chakavu hata pale maji yasipofika kwa wananchi, tunapohitaji kuweka *booster station* katikati ili ya-*pump* iwekwe, maana yake ile *pressure* ikishakuwa kubwa na miundombinu ikiwa chakavu maana yake itakuwa ina-*burst* na matokeo yake maji yanazidi kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, Serikali tumeshaliona hilo na sisi tunachukua hatua kuhakikisha kwamba tunaendelea kurekebisha miundombinu iliyochakaa ili kuhakikisha kwamba tunazuia upotevu wa maji na wananchi wanaendelea kupata zao la maji kama ilivyokusudiwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, na pia naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara kwa kutupatia shilingi bilioni 12 kwa ajili ya Mradi wa Maji Sigino, Babati. Imebaki shilingi milioni 400 kwa ajili ya Kitongoji cha Endasago. Mheshimiwa Naibu Waziri alifika ukatuahidi kwamba tutapatiwa hizo fedha. Ni lini hizo fedha zitafika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Gekul kwa sababu nakumbuka tulienda katika miradi hiyo na aliwasemea wananchi wake na anaendelea kuwasemea wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata jana aliongea na Mheshimiwa Waziri, lakini sisi tayari tumeshawasilisha madai haya Wizara ya

Fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba fedha hizi zinapelekwa kwa ajili ya kuhakikisha mradi huo unaendelea vizuri, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Bananga**.**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Mkoa wa Tabora hususan Jimbo la Tabora Mjini kuwa na mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria, lakini baadhi ya kata ambazo zina mazingira ya vijiji bado hazipati maji yanayostahili. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na *TUWASA*, ili kuona namna bora wananchi hawa wanaoishi mjini na kwenye kata za vijijini nao waweze kupata maji kama ambavyo kata nyingine zinapata? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Hawa kwa kuwasemea Wanatabora. Ni jukumu la kila Mbunge kuhakikisha kwamba anawasemea wawakilishwa. Ni kweli kabisa Mradi wa Ziwa Victoria ambao uliigharimu Serikali shilingi bilioni 680 umekuwa ni *game changer* katika Mkoa wa Tabora na hasa upatikanaji wa maji katika Mji wa Tabora kwa sasa ni 99%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunatambua kwamba 99% ni katika wale waliopo katika mtandao ambao tayari upo. Tunatambua kwamba, kuna maeneo mengine mtandao bado haujafika na Serikali sasa tumeweka mkakati wa kuendelea kupanua wigo ili kila mwananchi afikiwe na mtandao, maji yaweze kumfikia na kuhakikisha kwamba kila mwananchi wa Tabora awe kijijini au mjini anafikiwa na huduma ya maji safi na salama, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninashukuru kwa ukamilishaji wa mradi wa maji kwenye Kata ya Manyamanyama, na Mheshimiwa Waziri alikuja kuzindua, lakini kuna mradi ambao umeanzishwa Kata ya Mcharo kwa ajili ya

usambazaji wa mabomba ya maji na hasa ukizingatia kuna Chuo cha Kisangwa ambapo wanafunzi wanasoma, hakuna maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ni lini mtakamilisha mradi huu, ili wananchi wa Nyamatoke, Changuge, Mcharo, Kisangwa na maeneo mengine kwenye kata hiyo waweze kupata maji safi na salama? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, na pia namshukuru sana Mheshimiwa Ester Bulaya kwa kuendelea kuwapigania Wanabunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mradi huu tayari tumeshaanza kusambaza mabomba, pia tupo ndani ya muda wa mkataba. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, pale ambapo tutafikia kulingana na mkataba ninaamini kabisa mradi utakuwa umekamilika, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini mkandarasi anayetekeleza mradi wa maji uliopo Kihesa, Mgagao, Masege na Masalali katika Jimbo la Kilolo, atalipwa, kwa sababu wananchi wameusubiri kwa muda mrefu sana, ili waweze kupata maji safi na salama? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Iringa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa Mgagao, Masalali uliopo Wilaya ya Kilolo Mkoa wa Iringa ni mradi ambao unagharimu shilingi bilioni 1.3 na tayari umefikia 85% ya utekelezaji wake. Sasa Serikali imebakiza kipengele cha *pump* peke yake na inatafuta fedha ili kumlipa Mkandarasi aweke *pump* na wananchi

waweze kupata huduma ya maji safi na salama, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Rorya, Tarime unatakiwa kuhudumia majimbo matatu. Nilishiriki kwenye kutia sahihi, mradi ukasimama tukashiriki kupiga kelele fedha imeenda. Juzi Mheshimiwa Balozi Dkt. Nchimbi amefanya ziara pale Mogabiri kwenye tenki la maji, nikasikitika kuona kwamba hakuna matoleo ya maji kwenda Makao Makuu ya Halmashauri yangu ya Nyamwaga ambayo inaweza ikahudumia Kata ya Binagi, Nyarero, Nyamwaga, Kibasuka, Kanyange, Nyakonga na Muriba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri aniambie tulichoongea alikaa akabadilisha, akatoa maelekezo kule Musoma Mara, au yale makubaliano yanaendelea kule ili mimi nisiende kukaangwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Waitara Mbunge wa Tarime kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi unapokuwa unajengwa unakuwa umesanifiwa na *design* yake ndiyo inaonesha *scope* ya kazi na maeneo ambayo yatapata maji, lakini kama kuna changamoto hiyo, kama Serikali ninaomba niipokee na nielekeze wataalamu wetu waende waangalie ili watupatie majibu ya uhakika kama tumeenda kinyume na usanifu ulivyofanyika, basi tutachukua hatua kama Serikali ili kuhakikisha watu wa Mheshimiwa Waitara wanapata huduma ya maji safi na salama baada ya mradi huo kukamilika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tutaongeza maswali matatu ya nyongeza, atakuwa Mheshimiwa Hussein Amar, Mheshimiwa Butondo, Mheshimiwa Josephat Kandege na Mheshimiwa Kunambi. Mheshimiwa Hussein, karibu.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa tuliomba fedha kwenye bajeti hii ya 2025, shilingi bilioni 4.3 kwa ajili ya kukamilisha usambazaji wa maji kwenye Kata ya Kaboha, Shabaka, Mwingiro, Nyabulanda, Nyugwa, Bukwimba, Busolwa na Nyang'hwale, je, Serikali itatoa fedha hiyo ili tuweze kukamilisha mradi huo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hussein, Mbunge wa Nyang'hwale kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge na amekuwa akifanya ziara kwenye kata yake, na nilibahatika kufanya ziara katika Jimbo lake, tulienda katika baadhi ya kata. Nimhakikishie kwamba ahadi ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Watanzania wanasambaziwa huduma ya maji safi na salama wakiwemo wananchi wa Nyang'hwale. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itatoa fedha, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mradi wa Igaga – Mwamashele – Lagana umekamilika sasa kwa zaidi ya mwaka mmoja na ulianza kufanya kazi, lakini ghafla miezi mitatu pamepatikana *breakdown* ya kawaida tu, wananchi hawapati huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kutoa maelekezo, ili utatuzi wa marekebisho na matengenezo ya mabomba maeneo yaliyoharibika yafanyike haraka na huduma hiyo ianze kutolewa kwa wananchi hao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninamshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Butondo Mbunge wa Kishapu. Ni kweli kabisa Mheshimiwa

Butondo kwanza kabla ya kuuliza swali hili, tayari ameshatuwasilishia Wizarani jambo hili na tayari tumeshaanza kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo yangu ni kwamba, kuwepo na uharakishwaji wa ukamilishaji wa hiyo *breakdown* iliyokuwa imetokea ili wananchi wa Mheshimiwa Butondo waendelee kupata huduma nzuri ya maji safi na salama, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Godwin Kunambi, jiandae. Mheshimiwa Paresso, karibu.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 upotevu wa maji umefikia 36.8% sawa na hasara ya shilingi bilioni 114. Nini mkakati wa Serikali kudhibiti huu upotevu wa maji ili tusiingie hasara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upotevu wa maji unaokubalika ni kati ya 15% - 20%. Mheshimiwa Paresso ameonesha namna ambavyo Serikali inaweza ikapoteza fedha. Ni kweli kabisa, kwanza mkakati wa Serikali ni kuanzia pale kwenye usanifu wenyewe. Tunapofanya ule usanifu, tunahakikisha kwamba hakuna kitakachopotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, miundombinu ambayo imekuwa na uchakavu. Tunahakikisha kwamba na yenyewe inaendelea kuboreshwa. Cha tatu, ni utoaji wa huduma yenyewe. Pale ambapo utoaji wa huduma unaweza ukawa na watu ambao hawaelewi namna ya utoaji wa huduma na penyewe tunaendelea kudhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu ni kwamba mnyororo mzima wa utoaji wa huduma ya majisafi na salama usiwe na chembechembe za upotevu wa maji ambao unatokana na uzembe ambao tuna uwezo wa kuuzuia, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Godwin Kunambi.

**MHE. GODWIN KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake njema ya kumtua mwanamke ndoo kichwani wa Tarafa ya Mlimba kwa kupeleka fedha bilioni 7.4. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, swali langu, mradi ule kwa mujibu wa mkataba ulipaswa ukamilike ndani ya miezi 12, sasa yapata miaka miwili. Wale wananchi wa Tarafa ya Mlimba wangependa kujua ni lini mradi huu utakamilika? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, na pia namshukuru Mheshimiwa Mbunge wa Mlimba, kaka yangu Mheshimiwa Kunambi. Ni kweli kabisa mradi huo ulitakiwa kukamilika ndani ya mkataba ambayo ni miezi 12, lakini kulikuwa na changamoto zilijitokeza hapa, na bahati nzuri tumezi-*accommodate* tayari, na tunaamini kabisa kwamba, mkandarasi sasa atarudi *site* kwa ajili ya kwenda kuukamilisha mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tukifahamu kabisa kwamba changamoto ilikuwa ni malipo ambayo mkandarasi tuliyekuwa tumefikia katika sehemu ya kujadiliana namna bora ya kumlipa, sasa tayari tumeshawasilisha kwa ajili ya malipo. Nitarajie kwamba huo mradi utakamilika kabla tunapoenda kwenye Uchaguzi Oktoba, 2025 ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana nami kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Napenda kufahamu, ni nini mkakati wa Wizara? Kwa sababu hapa karibuni kama utakumbuka, Serikali ilitoa visima zaidi ya vitano kwenye kila Jimbo, lakini bado Majimbo mengi visima hivyo havijafungiwa *pump* baada ya kuvichimba na wananchi wanakosa huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, nataka kufahamu, ni lini *pump* kwenye Kijiji cha Masiku na maeneo mengine kwenye Jimbo la Ndanda zitafungwa ili wananchi waweze kupata huduma ya maji baada ya kuchimbiwa visima kwa muda mrefu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nimshukuru sana Mheshimiwa Cecil Mwambe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba, Serikali kupitia Programu ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ya visima 900 ambapo ni visima vitano kwa kila Mbunge wa Jimbo tayari vimeshachimbwa vya kutosha. Kuna baadhi ambavyo vilikosa maji, lakini vile ambavyo vimeshapata maji, mtandao wake *(point source)* kituo rahisi cha kuchotea maji vimeshakamilika. Tulikuwa tumetoa kandarasi kwa baadhi ya wazabuni ili waweze ku-*supply* hizo *pump*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kwamba wameshaanza ku-*supply* kwenye maeneo mengine na tayari wameshaanza kufunga. Tunaamini kabisa kwamba na Jimbo la Mheshimiwa Cecil na vijiji vyake vitafikiwa kabla ya mwaka huu wa fedha kuwa umeisha, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na swali la Uchukuzi. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa kujibu hoja zinazohusu Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba, sasa aulize swali lake.

Na. 237

**Ujenzi Bandari ya Karema**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza: -

Je, kwa nini Serikali iliamua kujenga bandari Karema wakati upande wa *DRC* bado hawajajenga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikishirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo zilisaini Hati ya Makubaliano kwa ajili ya kuboresha na kuimarisha miundombinu ikiwemo bandari ili kuchochea shughuli za kiuchumi baina ya nchi hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutimiza azma hiyo, Serikali kupitia *TPA* ilianza maboresho ya Bandari za Kigoma pamoja na ujenzi wa Bandari mpya ya Karema katika Ziwa Tanganyika. Kwa sasa *TPA* inaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya kuendeleza Bandari za Moba na kwa upande wa Kalemie ujenzi umeanza kwa kushirikiana na mwekezaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza naomba nitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa ujenzi mkubwa sana wa bandari wa zaidi ya shilingi bilioni 49, na kwa zaidi ya miaka miwili, sasa umekamilika pamoja na kwamba haujaanza kufanya kazi. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi, pamoja na mikakati hii mizuri ambayo Serikali inayo, na bandari hizi zitakapokamilika kwa upande wa *DRC* lakini itakuwa ni bandari tu zimekamilika, ipo haja ya kupatikana barabara kutoka Bandari ya Moba mpaka kufika Lubumbashi ambako Watanzania wengi ndiko soko wanakolitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri ni shahidi, alipofanya kikao na *Country Manager* wa *TPA* pale Lubumbashi na Ubalozi wetu mdogo, walimthibitishia umuhimu wa hii barabara. Je, ni upi mkakati wa kuanza ujenzi wa barabara kutoka Moba mpaka Lubumbashi ili kuiunganisha nchi yetu ya Tanzania moja kwa moja na *DRC* bila kupitia nchi ya Zambia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa tunatambua jitihada hizi ambazo zinafanywa na Serikali zinaweza zikachukua muda mrefu kwa sababu ni uwekezaji mkubwa, na bado mpaka sasa hivi wafanyabiashara kulifikia Soko la Lubumbashi ambao ni miongoni mwa miji mikubwa ambayo inawapatia Watanzania wengi pesa, bado wanapitia changamoto kubwa na kadhia kubwa wanapopitia nchi ya Zambia kutokana na vita ya uchumi iliyopo kwa sababu kila mtu analiangalia Soko la *DRC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni ipi hatua madhubiti ya Wizara hii ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Wizara nyingine kukaa chini kuendelea kutatua changamoto za wafanyabiashara wanaoliendea Soko la Lubumbashi ambazo wanapitia kwenye nchi ya Zambia? Ni upi mkakati wa haraka na dharura ili Watanzania wasiendelee kuumia? Ahsante *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wetu wa Uchukuzi, natumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Sichalwe kwa jinsi anavyofuatilia. Mheshimiwa Sichalwe ni moja ya wadau muhimu wanaofuatilia sana namna ambavyo Serikali inaweza ku-*access* Soko la Kongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba nchi yetu imebarikiwa kuzungukwa na nchi nyingi zisizo na bandari, na upande wa Zambia tuna zaidi ya mzigo wa tani milioni saba, na upande wa Kongo zaidi ya mzigo wa tani milioni 10 na nchi nyinginezo. Hata hivyo, bado hatujafikia inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumpa pongezi hizo, naomba nijibu maswali yake mawili ya nyongeza ambayo ameyauliza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ameuliza habari ya suala la barabara kutoka Moba kwenda Lubumbashi. Huu ni ushauri anaoutoa mara kwa mara, nasi Serikalini tumeshaupokea na tumeshaanza kuandaa taarifa ya wataalamu ili kutazama fursa zilizopo na mchakato mzima wa namna ya kufikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaendelea na hilo, ukizingatia swali lake la msingi aliuliza ni kwa nini Serikali ilianza kujenga Karema wakati upande wa pili hatujaanza pengine kupatumia, Serikali kwa kushirikiana na wenzetu wa Kongo tayari tumeshaanza kufanya *utilization* ya bandari hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza, ukienda pale Kongo upande wa Katanga eneo la Manono, tuna madini mengi ya *lithium* na *copper* ambapo ujenzi wa barabara kilometa 450 kutoka kule Manono – Katanga – Kalemie umeshaanza sambamba na usanifu wa awali ili hapo baadaye tuweze kujenga *SGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa miaka mingi sana Bandari ya Kalemie ilikuwa haitumiki na imekuwa ni kilio cha Wabunge wengi sana wanaotumia Ziwa Tanganyika. Tayari ujenzi huo umeanza kama nilivyozungumza na wenzetu wa Kongo kwa kutumia mwekezaji wanajenga Bandari ya *New Kalemie*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo peke yake haliishii hapo. Ili kuona Serikali imetambua umuhimu wa fursa zilizopo katika Ziwa Tanganyika, inakwenda sambamba na ujenzi wa meli nne ili wawekezaji hao waweze kusafirisha mzigo wa *lithium* na *copper* na madini mengine kutoka kule Katanga kuja hapa kwetu, kwenda mpaka Bahari ya Hindi ambapo tunaanza na meli nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tayari wameshaanza kujenga meli ya kwanza tarehe 1/4/2025 na meli nyingine nne zitakuwa zimekamilika ndani ya miaka hii miwili. Tunategemea mzigo zaidi ya *metric tons* 1,500,000 katika mwaka wa kwanza

utaanza kupitishwa. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa kwa kufuatilia jambo hili na nimeona nitoe kwa ufafanuzi mkubwa zaidi ili aweze kupata picha hiyo kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nakubaliana na changamoto zilizopo kwenye upande wa madereva wetu wanapotoka hapa kwenda upande wa Kongo kupitia upande wa Zambia. Changamoto hizo zinaendelea kushughulikiwa kwa kushirikiana na nchi hizi mbili kidiplomasia kwa lengo la kuboresha biashara hiyo ili sisi sote kwa sababu wao ni wanufaika na sisi ni wanufaika na maeneo mengine tuweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wetu mzuri na wa kudumu zaidi ni kutazama namna ya kuweza kufikia nchi *specific* kupitia Ziwa Tanganyika kama ambavyo nimeeleza kwenye maelezo ya awali, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru, unaweza ukarejea.

Waheshimiwa Wabunge, tunawashukuru kwa maswali na Serikali ambayo imeendelea kujibu, na sasa tunahitimisha kipindi chetu cha maswali. Naomba sasa niwatambulishe wageni ambao wapo Bungeni.

Kwenye wageni waliokaa kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi kutoka Lushoto Mkoa wa Tanga ambaye ni Ndugu Ally Kassim Daffa, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Lushoto. Karibu sana, karibu sana Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge. Wapo wageni 32 wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambao ni Wajumbe wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Kijiji cha Sangaiwe, Halmashauri ya Wilaya ya Babati Mkoani Manyara, karibuni sana viongozi wetu. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Msongwe Kasekenya, Mbunge na Naibu Waziri wa Ujenzi, ambao

ni Kamati ya Siasa kutoka Wilaya ya Ileje wakiongozwa na Ndugu Robson Mwaipula, Mwenyekiti wa Wazazi Mkoa wa Songwe, karibuni sana viongozi wetu. *(Makofi)*

Tunao wageni 25 wa Mheshimiwa Maryprisca Winfred Mahundi, Mbunge na Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ambao ni wafanyakazi wa Kampuni ya *TICON* kutoka Mkoa wa Mbeya, karibuni sana wageni wetu *(Makofi)*

Tunao wageni 50 wa Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, ambao ni wanachama wa Taasisi ya Itambue Thamani Yako, Tawi la Dodoma, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, ambaye ni Ndugu Bryceson Tumaini, mtoto wake kutoka Busanda Mkoa wa Geita. Karibu sana, karibu sana kijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, ambao ni wapigakura wake kutoka Meru Mkoa wa Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 55 wa Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, ambao ni walimu na wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Feza kutoka Dodoma, karibuni sana wanafunzi kutoka Shule ya Feza. *(Makofi)*

Pia, naomba nimtambue kwa upekee mtoto Irfan Juma Usonge ambaye ni mtoto wa Mheshimiwa Juma Usonge na Mheshimiwa Munira Mustapha, karibu sana Bungeni Irfan. Haya wazazi hongereni kwa kulea. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ambao ni baba yake mdogo na ndugu zake kutoka Bunda Mkoa wa Mara. Karibuni sana. Baba yake mdogo na ndugu zake, wako wapi? Aah, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi ambao ni ndugu zake kutoka Lushoto Mkoa wa Tanga, karibuni sana wageni wetu kutoka Tanga. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke ambao ni wapigakura wake kutoka Kasulu Mkoa wa Kigoma, karibuni sana ndugu zetu kutoka Kigoma. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Aloyce John Kamamba ambao ni rafiki zake kutoa Bukoba Mkoani Kagera, karibuni sana ndugu zetu. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ambaye ni Mhandisi Samson Hasunga, mfanyakazi wa *TARURA* kutoka Mbozi Mkoa wa Songwe. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge ambao ni ndugu zake kutoka Vigwaza, Chalinze mkoani Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, ambao ni rafiki zake kutoka Tanzania, Ujerumani, na Nigeria, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Dodoma Ndugu Aisha Madoga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, ambao ni viongozi wa Taifa Letu Kesho Yetu (TK) kutoka Tandahimba Mkoa wa Mtwara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, ambao ni watumishi wa Halmashauri ya Ushetu Mkoani Shinyanga. Wapo? *Yes,* karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 21 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe na Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati ambao ni wanamaombi kutoka Jijini Dodoma na Kwaya ya Amani kutoka Veyula, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni vijana 26 na walimu nane kutoka Kituo cha Huduma ya Watoto na Vijana, kinachotoa huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu chini ya usimamizi wa KKKT Mtibwa Mkoani Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, tunao wanachama 100 wa Shirika la *International Peace Information,* Umoja wa Amani Kwanza kutoka Tanzania na Uganda, wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Umoja huo Dkt. Judith Mollel. Ahsanteni sana wageni wetu, karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji. Kwa upande wa Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi tutatumia dakika tano kwa kila mchangiaji, na kwa Wabunge wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo tutatumia dakika 10. Namwita sasa Mheshimiwa Prof. Muhongo, karibu.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ndugu zangu wa CHADEMA kule, CHADEMA naomba mnipatie na mimi tano ziwe 10. Wamekubali. Sasa ... *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Samahani Profesa, samahani Profesa.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** *Mic* yako iko sawa?

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unanipata?

**MWENYEKTI:** Nakupata, endelea.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuhusu dakika 10 za CHADEMA umenipata? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, sasa ni hivi ndugu zangu, mimi nadhani hii miradi ya barabara (miundombinu) ukifuatilia duniani kote, nchi zote ni miradi ya kudumu. Kwa hiyo, kwa upande wa Tanzania lazima tuipitishe bajeti kwa sababu lazima barabara zijengeke. Hata huko Marekani na wapi, barabara lazima zijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba nina barabara moja na ninatoa shukrani nyingi kwamba Mheshimiwa Rais alivyokuwa jimboni nilimwomba vitu viwili tu; barabara na mradi wa umwagiliaji na vyote vimekubalika Serikalini. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais na miradi yangu imekubalika inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaongelea barabara yangu kwa kifupi, hiyo ya kilometa 92. Barabara yangu inaunganisha vijiji vyote 68. Kiuchumi inakubalika, ni roho ya Mkoa wa Mara na Tanzania nzima. Barabara hii makadirio yake mwaka 2020 gharama yake ilikuwa Dola za Marekani milioni 50. Leo hii mwaka 2025 gharama zake ni dola milioni 53. Kwa hiyo, unaona ndani ya miaka mitano ambavyo hatukutekeleza huu ujenzi wake kwa haraka, gharama zimeongezeka kwa zaidi ya dola milioni tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu kwa Wizara ya Ujenzi, kwanza tujaribu kutekeleza miradi hii ya barabara kwa haraka, kwa sababu tutapunguza ongezeko la gharama za ujenzi wa barabara za lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara yangu ina miradi miwili ndani yake. Ina kilometa 40 ambazo nadhani wiki hii wanamaliza majadiliano na mkandarasi. Kwa hiyo, nawaomba *TANROADS* na Wizara waweze kumpatia mkataba aanze kujenga kabla ya tarehe 01 mwezi wa Saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii nayo ina mradi wa pili, daraja kubwa la kisasa ambalo gharama yake ni karibu shilingi

bilioni 60. Naishukuru Benki ya Dunia *(World Bank)* wamekubali kufadhili hii barabara. Kwa hiyo, naomba *TANROADS* na Wizara waharakishe kupata *no objection*. Niliwaomba kwamba yakiwa magumu saa nyingine wau-*outsource* watu ambao tumefanya kazi nao tuweze kupata hiyo fedha haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo dakika nilizokuwa naomba kuongezewa nataka kutoa mapendekezo ya kupata fedha za kutekeleza miradi ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti na ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi ukienda kwa kila Mtanzania ukiuliza anachohitaji ni vitu vitatu; maji, umeme, na barabara. Tukiri kwamba bajeti yetu ni finyu, haiwezi ikatekeleza kwa haraka sana. Sasa, haya ndiyo mapendekezo yangu ya kupata fedha za kutekeleza ujenzi wa barabara zote ikiwemo na ya kwangu ya Musoma Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuongeze bajeti, na kuongeza bajeti ninamaanisha miradi mikubwa mikubwa kwa miaka miwili inayokuja tuipunguzie bajeti kwa 40%. Hiyo bajeti iliyopunguzwa 40%, siyo kwamba tunasimamisha miradi mikubwa, ila tunaipunguzia na hizo fedha ziende kwenye ujenzi wa barabara, maji, na umeme. Hiyo ni *strategic planning* na *financial deployment*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha pili cha fedha za kujenga barabara lazima tuanze kukopa kwenye benki zetu za ndani na ambazo Serikali ina hisa. Tukubaliane tuwe na *concessional loans*, yaani wasitoe riba zaidi ya asilimia nne. Hiyo itafanya Wizara ya Ujenzi ipate fedha za kutekeleza miradi yake, *concessional loans* kutoka kwenye benki zetu za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha tatu, ile *PPE* tunayosema *triple P (Public Private Partnership)* ianze kujenga barabara na hizi barabara za *triple P* tunapaswa kuanza kupata tozo *(road tolls)*. Hizi ni fedha nyingi sana na sehemu nyingine kote duniani ukienda barabara kubwa unasimama mahali unalipa au unakuwa umelipa kabla ya kuanza safari yako. Hayo ni

makusanyo makubwa sana yatafanya barabara zetu ziweze kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha nne, hauwezi ukakwepa kukopa nje. Hili la mikopo jamani lisiwatie homa sana, tutaliongea kwenye bajeti. Tuna takwimu ya mikopo ya nchi kubwa duniani hapa. Kwa hiyo, nasi tusiogope kukopa ili mradi hiyo mikopo itumike kama inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mikopo mizuri hapa ninayoongelea ni mikopo ile ya riba kidogo, ambayo ni ya 0.05 mpaka *three percent*, *concessional loans*. Hiyo ndiyo mikopo ya *World Bank*, mikopo ya *IMF*, mikopo kama hiyo tuichukue, tujenge barabara, tusambaze maji, tusambaze umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha nne ni *EPC+F* yaani *E* ni *Engineering, P – Procurement, C – Construction* na *Financing, EPC +F*. Huu ni mtindo unatumika sehemu nyingi sana duniani. Mnamtafuta mtu ambaye ana fedha, ana uwezo wa ujenzi wa barabara, mnampatia barabara anajenga mnalipana pole pole, lakini hapa tahadhari ni kwamba usiende kwenye *EPC+F* wakati wewe hujui gharama za barabara yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi Musoma Vijijini wakija, najua barabara yangu ni dola milioni 53. Kwa hiyo, naweza kumpokea kwa sababu najua tayari najua gharama za barabara. Kwa hiyo, hii ni njia nyingine ya kuweza sisi kupata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia ya mwisho ni kwenda kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange*. Miradi mikubwa yote duniani inaendeshwa kwa *stock exchange*. Hata migodi yote mikubwa unaiona duniani ni *stock exchange*. Sasa kwa sababu viwanja vyetu vya ndege vingine ni makampuni, kama kiwanja cha ndege Dar es Salaam na Kilimanjaro, hivyo viwanja vya ndege viende kwenye *stock exchange* ya Dar es Salaam na tuweze kupata hapo fedha za kuweza kujenga viwanja na barabara. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni mapendekezo ya ujenzi wa barabara za Tanzania. Bado tunakuwa waoga, tunajenga barabara kwa mtindo ambao baadaye unafanya unakuwa wa gharama kubwa. Barabara za *highways* zote tuseme Dodoma Morogoro, Musoma - Mwanza hizo barabara zinapaswa kuwa na njia nne, mbili kwenda, mbili kurudi na zinavyozidi kwenda zinapaswa kuwa na njia tatu na sehemu za kupumzikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka hii barabara ....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa muda wako ulishaisha tafadhali.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya nashukuru sana, naomba waendelee kujenga barabara ya Musoma Vijijini na tuendelee kutafuta fedha za kujenga barabara. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa tulimpa dakika saba na amezitumia vizuri, tunakushukuru sana Mheshimiwa Profesa.

Waheshimiwa Wabunge, samahani kidogo kuna marekebisho ya matangazo ya wageni. Nimepata maelekezo hapa kwamba wale wageni ambao walitangazwa kuwa wanatoka Kamati ya Siasa ya Ileje, naomba nifanye marekebisho kuwa ni Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Songwe. Naomba wasimame tena kama wapo bado. Basi tunaomba radhi kwa hilo, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale na Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, ajiandae. Ni dakika tano na itapiga kengele moja tu ambayo itaashiria kwamba muda wako umeisha na utazimiwa *mic*.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hoja iliyopo Mezani leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mungu kwa kutupa pumzi yake ya uhai, na pia napeleka pongezi kuu kwa Kiongozi wetu Mkuu wa nchi Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi zake nzuri ambazo anazifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Tumeona maelezo yenu ni mazuri, tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu yaweze kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze na barabara ya kutoka Liwale kwenda Morogoro. Hii ni barabara ya kuunganisha mikoa miwili, ni ya muhimu sana. Tunaiomba Serikali kuna kipindi barabara ya kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara iliharibika, wananchi wanaotoka Liwale – Nachingwea walikuwa wanazunguruka sana mpaka kufika Dodoma. Wanatoka Liwale wanapita Nachingwea, wanaenda Masasi, wanaenda Ruvuma – Njombe – Makambako – Iringa mpaka warudi Dar es Salaam au waje Morogoro ni safari ndefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba sana Serikali watutengenezee barabara ya kutoka Liwale kwenda Morogoro, itawasaidia sana wananchi wa kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza Serikali kwa mapitio na ujenzi wa barabara ya Kibiti - Lindi. Hii barabara inakatisha tamaa, kwani ni mbovu sana. Kama alivyoongea jana Mbunge wa Dar es Salaam, Mama Kisangi alisema kuna maeneo ni korofi, yanakatisha tamaa. Vilevile kuna Mbunge wa Songea aliongea, Mheshimiwa Mama Msongozi akasema kuna vidungurushi, yaani kuna yale mashimo ya hatari, barabara hizi zinakatisha tamaa. Serikali imechukua jitihada ya kuitengeneza, imeanza na madaraja, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe angalizo kidogo, pale Somanga, maji kila siku yanavuka daraja yanapanda juu. Ombi kwa wakandarasi ambao wanaitengeneza barabara ile, waangalie eneo lile, kama hawana uwezo wa kuweka *flyover,* basi hilo daraja wahakikishe wanaliinua, kwa sababu wakiweka

daraja bila kuinua eneo lile, yale maji yatavuka juu ya daraja, na itakuwa ni kazi bure, bado tutaendelea kupata shida wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa kupitia barabara ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pamoja na utengenezaji wa madaraja, tuendelee kuwasisitiza na kuwaomba kwamba ile barabara kiukweli ilitengenezwa chini ya kiwango, ni mbovu, mbovu, mbovu sana. Bado tuendelee kuwasisitiza Serikali waendelee kutengeneza kipande kwa kipande mpaka wakamilishe barabara ile, kwa sababu barabara ile siyo ya kutengeneza sehemu moja, ni ya kuibomoa yote, haifai kabisa. Tunaomba Serikali na tunasisitiza kwenye jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuiongelea pia barabara ya kutoka Masasi kwenda Nachingwea - Liwale. Barabara hii ni ya muhimu sana, kama inavyoonekana kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, imekuwa ikijirudia kila siku. Naiomba Serikali na tunajua inao mpango huo wa kuianza hiyo barabara lakini bado nisisitize kwamba barabara hii ni ya kimkakati, kuna mambo mengi sana ya msingi ambayo yanatakiwa yatumike kwenye barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa unaenda Liwale kutoka Nachingwea, mvua ikinyesha ya dakika tano tu ile barabara huwezi kwenda, inateleza, inajaa maji, inakatisha tamaa. Tunaiomba Serikali na kuwasisitiza, tunajua mna hilo lengo, tunaomba mtutengenezee barabara ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ile tangu tumepata uhuru mpaka leo haijawahi kuonja lami. Wananchi waliopo kule ambao hawajawahi kufika mjini Dar es Salaam wala wapi, hawaijui lami. Nawaomba, ile barabara bado ni mpya japokuwa ni barabara kongwe ya miaka mingi na ni barabara inayotoka kwenye mkoa mwingine kwenda mkoa mwingine. Tunaiomba Serikali na kuwasisitiza, tutengenezewe barabara ile kwa kiwango cha lami ili wananchi waweze kuona faida za kodi zao ambazo wanazilipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia barabara hiyo ya Masasi kwenda Liwale kuna waathirika ambao nyumba zao zimebomolewa, wamechukuliwa maeneo yao, na ni miaka mingi

zaidi ya 15. Kwa kweli hii inakatisha sana tamaa wananchi. Naiomba Serikali tufanye juu chini ili tuweze kuwalipa wale waathirika wa barabara hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, atafuatia Mheshimiwa Asia Halamga, Mheshimiwa Phillipo Mulugo, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nampongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kile anachokifanya kwenye Wizara hii ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona juzi ameongeza pia bajeti kuwapa watu ambao wana changamoto, maana Mkoa wetu unaongoza kwa mafuriko. Pia nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutuletea kaka yangu huyu wa Kizaramo Mheshimiwa Ulega. Mheshimiwa Ulega ni Waziri ambaye anaingia *site* na sasa hivi wakandarasi wanapungua vitambi, maana ukiwa unanenepa hutakiwi kudaiwa. Kwa hiyo, kwa kifupi Mheshimiwa Ulega, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Morogoro Kusini Mashariki tunaendelea kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kile alichokifanya katika barabara yetu ya Ubena - Zomozi. Mkandarasi yupo *site*, pesa imetoka, tunashukuru Mungu *Alhamdulillah*. Hili ambalo tunaweza kulisema kwa kuisemea Wizara, leo hii tunaona wenzetu wakifurahia barabara, lakini sisi wana Morogoro Kusini Mashariki, huu upande wetu wa Bigwa – Kisaki; mimi ninakaa kiti karibu na Mheshimiwa Spika, nilibahatika kuona namba yangu amei-*save* vipi? Ameni-*save* Bigwa - Kisaki, kwa sababu miaka mitano nalilia barabara tu. Kaka yangu Mheshimiwa Ulega wewe ni mtu wa vitendo, tayari kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kitendo cha wewe kuelekeza pesa zije pale, barabara ianze ndugu yangu. Kaka Ubunge naupenda huu; kazi naitaka hii; wananchi wa Morogoro Kusini Mashariki wanataka barabara ya Bigwa – Kisaki. Haiwezekani miaka mitano naongea neno moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi ina Rais msikivu, ametupa kilometa 78 na ameruhusu pesa ije. Mheshimiwa Ulega shida ipo wapi? Unanasa wapi? Mimi nakuona mwamba, jembe kabisa, lakini hapa unakwama wapi Mheshimiwa Ulega? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba, leo naondoka na shilingi ya Mheshimiwa Waziri, nakwenda nayo Kusini Mashariki, watanirudisha kama akisema analeta barabara. Maana kuna vitu unaongea mwishowe; mimi kuna siku nakaa na Spika hapa nilivyojiona ameni-*save* Bigwa - Kisaki nikajiuliza, hivi ni kero au anavutiwa na ninavyochangia kila siku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kitu kimoja kwa kaka yangu Mheshimiwa Ulega, anionee huruma. Sijaja humu ndani hata siku moja kuchangia chochote. Wanamorogoro Kusini Mashariki wanataka barabara ya Bigwa - Kisaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza kwenye hii Wizara kaka yangu Mheshimiwa Ulega; upande wa Mkurugenzi wa *TANROADS, brother* mtu poa sana. Kaka siyo kama nakujaza, Mkurugenzi wa *TANROADS* mwambie Waziri wako Bigwa - Kisaki wanataka barabara. Mkandarasi anataka *75 percent* tu ili aingie *site*. Twendeni *site* jamani, shida ipo wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najua Mheshimiwa Waziri ana Mkurugenzi mzuri na mambo yataenda, kama alivyokuwa na Mkurugenzi mzuri baba yangu Kondoro wa *TBA,* ukimtazama mvi na anavyoongea ni vitu viwili tofauti. Ana Mkurugenzi Mnyawezi. Sisemi kwa sababu ni baba mwenye nyumba wangu wa *TBA,* lakini nasema kwa sababu *he has a good heart*. Alishawahi kuniita siku ya kwanza akaniambia, uongozi ni kuweka rekodi, kapambane uweke rekodi. Rekodi yangu mimi ni kuhakikisha Bigwa - Kisaki inakuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nikishindwa kuchukua neno la baba yangu Kondoro la kuweka rekodi ni kwa sababu ya Mheshimiwa Ulega na Mkurugenzi wake wa *TANROADS*. Nawaomba, leo hii mimi nipo kwenye orodha ya wale ambao watakaoshika shilingi yake mpaka nijue hatima ya barabara yetu ya Bigwa – Kisaki, kwa sababu haiwezekani *over five years* mimi niko hapa Bigwa – Kisaki. Mtu mwingine wa nje anashangaa yule hajui kuongea au! Nitaomba nini hatuna barabara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mheshimiwa Rais ametuletea barabara za ndani zote, kwetu sisi vitu vilivyoletwa kwetu kwenye Jimbo la Kusini Mashariki natembea kifua mbele, mimi ndio Mbunge na nitaapa pale mwezi wa 11, na ninatembea nikiamini Chama cha Mapinduzi kitashinda kwa kishindo na Mheshimiwa Rais atashinda kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe, hili ni ombi langu mimi na wana Morogoro Kusini Mashariki.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Taletale.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Taletale, nakushukuru sana.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Asia Halamga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mulugo, Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi, ajiandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara ya Ujenzi bajeti ya mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambazo anaendelea kuzifanya ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba nijikite ndani ya Mkoa ninaotoka, Mkoa wa Manyara katika Wizara hii ya Ujenzi. Kwanza tuendelee kupongeza kazi kubwa ambazo zinafanywa na Wizara hii ya kuendelea kuhakikisha kwamba barabara zetu zinaendelea kupitika, licha ya changamoto kubwa ya mvua inayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Manyara una jumla ya takribani barabara za *TANROADS* kilometa 1,657, lakini kilometa ambazo zina lami ni kilometa 257; kilometa ambazo hazina lami, ambazo ni changarawe ni kilometa 1,400. Utaona ni kwa kiwango gani bado tuna uhitaji mkubwa wa kuunganishwa na mtandao wa barabara, licha ya barabara kuu ambazo zinazounganisha nchi yetu ya Tanzania kati ya Mkoa wa Manyara na Mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi letu wananchi wa Manyara ni kwamba tuna barabara ndani ya Mkoa ya kuufungua Mkoa ili kuondoa kupita Wilaya, kutoka Simanjiro kuja kupitia Arusha kwa ajili ya kuja Manyara. Tunaomba sana tuzingatiwe, kwani upembuzi yakinifu umeshafanyika. Tunaomba tuwekwe kwenye bajeti ili sasa tusipite mkoa mwingine kwa ajili ya kuja kupata huduma ndani ya Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ambazo tunaomba zifunguliwe sasa ni barabara ya kutoka Babati kuja Kiteto kwenda Simanjiro kwa maana ya Orkesumet. Hii itakuwa imesaidia sana kuufungua Mkoa wa Manyara na kuendelea kuhakikisha kwamba kilometa hizi 1,400 tunaanza kuzipata kwa ajili ya kutengenezewa barabara ya lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa ya ujenzi wa madaraja ambayo imefanyika; daraja la Katesh, daraja la Dabili, daraja la Msasani, daraja la Minjingu na daraja la Losinyai kule Simanjiro. Kazi hizi zinaendelea, lakini tunachokiomba ni fedha ili kazi hizi zilizosimama kwa sasa ziweze

kuendelea. Fedha itolewe ili madaraja haya yaweze kupitika na wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kilometa 257 ambazo nimezisema za lami ndani ya Mkoa wetu wa Manyara, bahati mbaya sana miongoni mwa lami hiyo ni lami inayotoka Singida kuja Arusha, ambacho kimsingi kama umepita njia hiyo ni njia muhimu sana kwa wakazi wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa, kwa sababu wanatumia barabara hiyo kutoka Arusha kwa maana ya kuja kupita Manyara kuelekea Singida na kwingineko kwa Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitokea Dar es Salaam kuja Arusha, sehemu korofi iliyoharibika ni kipande cha Mkoa wa Manyara ambacho kinaanzia Dareda kinakuja Masakta – Masqaroda – Endagau - Endasak – Nangwa - Measkron, kinakuja mpaka Katesh, tunakwenda Mogitu - Gehandu ndani ya Wilaya ya Hanang ndicho kipande kikubwa ambacho kimeweza kuharibika na kukatika sana, na wakati wote imekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wanaotumia barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba ukarabati ufanyike walau wa dharura ili kuweza kunusuru ajali ambazo kwa sasa zinapatikana kwa sababu ya mashimo makubwa ambayo yamejitengeneza katika kipande hiki cha barabara nilichokitaja kutoka Dareda kwenda Gehandu mpaka Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuishukuru sana Serikali, kwani mwaka 2024 kwenye Bajeti ya 2024/2025 ulisainiwa mkataba wa kilometa saba za lami Kipande cha Dareda *Center* mpaka Dareda *Mission*. Kazi hiyo mpaka sasa hivi haijaweza kuanza na barabara ilishasainiwa mwaka 2024 katika Bajeti ya 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba sasa kazi hiyo iweze kuanza ili kile ambacho kilisainiwa na kilikusudiwa kiweze kwenda kufanya kazi na kuleta tija kwa wakazi wa Manyara kwa sababu, tunachokiamini ni barabara kubwa ambayo inatumika kufungua uchumi wa maeneo mengine kwa sababu, malori na bidhaa nyingi zinapitia pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, tunaomba Barabara ya Mogitu – Haydom iweze kujengwa kwa kipande cha lami, lakini pia, Barabara ya Nagwa kuja Kondoa iweze sasa kutengewa fedha kwa ajili ya lami, kwa sababu upembuzi yakinifu umeshafanyika na kazi hii kubwa ndani ya Mkoa wa Manyara, hususan Wilaya ya Hanang, kama ambavyo nimeitaja, iweze kwenda kufanyiwa kazi kwa sababu, wananchi wana imani kubwa sana na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. *Privilege* kama hizi zitakuwa chache sana Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Phillipo Mulugo, anafuatia Mheshimiwa Aloyce Kwezi na Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, ajiandae. Mheshimiwa Aloyce Kwezi.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nichukue nafasi hii awali ya yote kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kaliua. Nianze kwa kuipongeza Wizara hii ya Ujenzi chini ya Waziri, Mheshimiwa Ulega, kwa kazi nzuri zinazoendelea katika nchi yetu. Pili, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa miradi mikubwa sana aliyoileta katika nchi yetu na anayoendelea kuitekeleza, hususan katika Jimbo langu la Kaliua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Kaliua napongeza kwa sababu zifuatazo: Moja, Kaliua tumekamilisha ile barabara ya kwenda Kigoma kilometa 38 ambazo zina thamani ya shilingi bilioni 38. Pili, Kaliua tulikuwa tuna ujenzi wa barabara ya kutoka Uganza ambapo Mheshimiwa Waziri alikuja kama Waziri wa Mifugo kipindi kile; akija sasa hivi inawezekana akapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uganza kwenda Usinge tumekamilisha kilometa 7.5 zenye thamani ya shilingi bilioni 11.6.

Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana wewe kwa usimamizi mzuri, kwa sababu, tayari taa za barabarani zimeshawaka hivi tunavyoongea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mtendaji Mkuu wa Mkoa, Mlimaji anafanya kazi nzuri sana. Hii ni awamu yangu ya pili kwa sababu, mwaka 2024 nilisema hivi hivi kwenye bajeti hii na wakati nasema zile kilometa 7.5 zilikuwa hazijajengwa. Sasa nasema kwa sababu zimekwisha, taa zimewekwa na nina kila sababu ya kusema vijana kama hawa mwaangalie kwa macho mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Kaliua Mjini kuna *by pass* pale, kilometa nne zimekwisha, taa za barabarani zimewekwa na kilometa 1.5 iliyokuwa imebaki tayari, Mkandarasi *Samota General Construction,* kilometa 1.5 mkataba umeshasainiwa. Ninaamini ndani ya wiki hizi mbili ndugu zangu wa Ushokola kwenda Relini kazi itakwenda kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maombi kwa Mheshimiwa Waziri. Kwanza wananchi wa Usinge, Uganza, Kaliua, wanahitaji kumwona akienda kuzindua ile barabara ya kilometa 7.5, kwa hiyo, namkaribisha. Alikuja kama Waziri wa Mifugo, sasa aje tuchinje ng'ombe tule na wananchi wa Usinge kwa ajili ya ukamilishaji wa ile barabara. Ila ombi lao wananchi wa Usinge, wanasema taa za barabarani zimewekwa mbali, kuna upungufu kidogo. Naomba tuongezewe angalau taa 20 pale ili Mji wetu wa Uganza, Usinge, ukae vizuri zaidi, nami namwamini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ambalo nilikuwa nataka kuliomba, kama ombi maalum, ni barabara yetu ya kutoka Mpanda, Kaliua mpaka Kahama. Barabara ile ni ya kiuchumi. Leo nimekuja na ushauri huu, najua wanaendelea na upembuzi yakinifu, kwamba, kwa sababu ule mji tumejikuta vinabaki vile viraka vya *TANROADS,* hasa kutoka pale Ushokola kama unaenda Zugimlole, *TARURA* tunapiga lami zetu huku tunakutana na kile kipande ambacho kinakuwa bado kwa upande wa Ushokola. Nawaomba zile kilometa mbili tuwekewe ili kuwe na muunganiko mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, barabara hiyo hiyo ya kuelekea Kahama siyo lazima tuanze kwa kasi. Kwa sasa, ninashauri, twendeni taratibu kama inawezekana. Kwa mfano, tuanze na kilometa 10 kwenye Bajeti ya 2025/2026 kuanzia pale Kasungu kwenda Kazaroho kwenda Igwisi tukiwa tunaelekea Ulyankulu. Tutakapomaliza upembuzi yakinifu, mambo yakakaa vizuri, ninaamini mambo mazuri yatakuja, ninaamini Serikali yangu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kaliua ahadi yao ni kumpigia kura za kutosha, nyingi sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na wana imani na mimi Mbunge wao, Mbunge wa vitendo. Wanaamini kazi nzuri na kuwasemea na Madiwani wangu wa Chama cha Mapinduzi kule mambo ni bambam. Huyu ndio Mheshimiwa Dkt. Samisa Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kubwa ambalo mimi nashauri ni kuhusiana na malipo ya wakandarasi, yanatukwaza kwa sababu, wale tuna mahusiano nao, ni ndugu zetu, ni jamaa zetu. Wanapokuwa hawajalipwa na wamekopa benki, *interest* inakuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, katika eneo ambalo ataonekana ame-*perform* pia, ni kuwasaidia wazawa wetu. Naomba kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kwezi. Mheshimiwa Phillipo Mulugo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa wasaa huu kuchangia Bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Cha kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ametekeleza kutuletea fedha zetu katika miradi ya maendeleo katika Jimbo la Songwe, siyo barabara, lakini katika miradi yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, naomba leo nichangie kwa upole mkubwa sana na ninaomba Mheshimiwa Ulega anisikilize, ni juu ya barabara yangu ya lami. Toka nimeingia Ubunge mwaka 2010 nimekuwa nikiililia barabara hii ya kutoka Mbalizi – Mkwajuni mpaka Makongorosi. Tumekuwa tukiongea kila mwaka na kila mwaka kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ipo, zaidi ya miaka saba sasa, lakini hakuna kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka 2023 tuliiingiza kwenye bajeti wakasema ingefanyika, lakini hewa. Mwaka 2024 tumeiingiza kwenye bajeti, lakini mpaka sasa tunaenda kumalizia muhula bado sijapata chochote. Mheshimiwa Ulega, angalia Wabunge wenzangu wanavyochangia, wanavyoshukuru, kwa ajili ya barabara zao za lami, lakini katika nchi nzima unaweza ukasema nimebaki peke yangu. Ni barabara ya kutoka Mbalizi kwenda Wilaya ya Songwe. Wilaya ya Songwe ni mpya, lakini sina lami. Mheshimiwa Ulega wewe ni rafiki yangu, tumeingia Ubunge pamoja, hebu naomba uliangalie kwa umakini sana jambo hili, sina barabara ya lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara mwaka 2024 kwenye Jimbo langu akaahidi kwamba, angeweza kunipa lami lakini…

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka wapi?

**TAARIFA**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampa Taarifa mzungumzaji, asiseme kwamba ni yeye tu. Mimi pia Nyang'hwale; kutoka Kahama – Nyang'hwale – Busisi, barabara hii zaidi ya miaka 15.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa unapokea Taarifa?

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwomba Mheshimiwa Waziri. Naomba sana jambo hili liangaliwe kwa mapana marefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni madaraja kwenye jimbo langu. Ninalo Daraja la Muheza kwenda Isanzu. Ni barabara ya *TANROADS,* limeharibika kabisa. Hiki kipindi cha mvua barabara hii haipitiki na vijana wanalala pale mtoni siku tatu wanasubiri kwa ajili ya kwenda kupeleka mifugo yao kwenye masoko huko Isanzu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo Daraja la Magamba kwenda Mpona na lenyewe ni hatari tupu. Mwaka 2025, kwenye *Road Board* tumejaribu kuingiza kwenye bajeti, itakapofika huko kwenye bajeti itakayokuwa inaendelea leo naomba nisikie kwamba, na yenyewe ipo. *Otherwise,* Mheshimiwa Ulega, nisingependa nishike shilingi yako. Wewe ni kijana, lazima uwe unasikia haya mambo, na unafanya ziara kwenye majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimemsikia Mheshimiwa Waziri alikuwa Mbeya, nikajua labda angenitembelea na pale Songwe, lakini sikumwona. Naomba afike Mkoa wa Songwe na aje Wilaya ya Songwe. Wale wenzetu wa Ileje wana lami, wenzetu wa Mbozi wana lami, kule Momba unapoenda Sumbawanga kuna lami, lakini kwangu kuchepuka hapa Mbalizi kwenda kijijini kule Songwe hakuna lami. Mheshimiwa Ulega, nakuomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho, toka nimekuwa Mbunge tumekuwa tukipitisha barabara zetu ziingie kwenye *TANROADS,* lakini mpaka leo. Yaani kila siku wanasema kuna hiyo sera ya kuomba maombi barabara zile za *TARURA* zinazokuwa ni ndefu ziingie kwenye *TANROADS,* lakini sijawahi kuona hata barabara moja imekubalika ili siku moja na sisi tufanye sherehe ya kusema kwamba, barabara hii ya kutoka Kapalala kwenda Gua angalau imekubalika, kwamba, imeingia kwenye *TANROADS* au hii karabara ya kutoka Kininga kwenda Ngwala, kwenye mgodi mkubwa, kwenye madini adimu duniani, *rare earth,* hakuna barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wale wa *rare earth* na Kampuni ya Mamba, wanahangaika kweli kupeleka mitambo yao kule. Ni madini ambayo Tanzania hapa hayapo, ni madini ambayo Afrika hayapo, yapo *China* peke yake, lakini yapo kule Ngwala porini. Kwa nini, msitulee barabara ili madini haya tuweze kuyachimba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa *Eng.* Kasekenya anajua na alishafika mpaka kule Ngwala, atakwambia. Tuleteeni barabara basi jamani tujenge uchumi wa nchi yetu. Ni madini makubwa na yana hadhi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki leo dakika ziishe. Ombi kubwa ni hayo mambo mawili; madaraja yangu na barabara ya lami. Wenzangu wanafurahia, amesema Mheshimiwa wa Nyang'hwale hapa, labda kama Wilaya yake ni mpya, lakini mimi kule kwangu ni kwa siku nyingi. Naomba unileteе lami zile kilometa 91 kutoka Mbalizi – Mkwajuni – Saza mpaka Makongorosi. Ahsante sana Mheshimiwa Ulega, nimechangia kwa sauti ya upole, sauti ya Kimungu, najua utakuwa umenisikia. Tumsifu Yesu Kristu. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mulugo.

Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, wakati Mheshimiwa Hussein Amar akichangia hoja ya Mheshimiwa Mbunge alitaja pia, barabara yake. Nadhani alitaja kwa sababu hajapata fursa ya kuchangia. Naomba uichukue hoja yake kama mchango wake kwa siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu.

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii. Nami nianze kwa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika kuijenga nchi yetu, lakini hususan kuboresha miundombinu ya barabara. Sisi watu wa Tanga Mjini ni moja ya mashahidi wa kazi kubwa nzuri ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Ulega, Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya na timu yake kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya. Wakati naomba kuchangia, Wabunge wameona jina langu, Mheshimiwa Musukuma mtani wangu ananimbia Ummy, Tanga una hoja? Tanga kila sehemu kuna lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazo barabara nne ambazo leo nataka kuziongea hapa. Kwanza ni barabara ya Tanga – Pangani. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Ulega, nilipompigia mara tu baada ya kuteuliwa tulimpa kilio cha kusuasua kwa ujenzi wa Barabara ya Tanga – Pangani, akaja, na tunamshukuru Mheshimiwa Rais akatupatia shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Barabara ya Tanga – Pangani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Mheshimiwa Ulega, ni sasa wamsimamie kikamilifu mkandarasi ili aweze kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Tanga – Pangani kwa wakati, hususan kufidia muda wa takribani mwaka mmoja ambao ulipotea. Kwa nini, tunapigania kukamilika haraka Barabara ya Tanga – Pangani? Siyo tu itasaidia usafiri wa watu na mazao, lakini itaufungua Mkoa wa Tanga kwa upande wa utalii. Tunataka kama vile watu wanakwenda *beach* za Nyali, *Beach* za Diyani, tunataka watu waje *Beach* za Pangani, kwa mdogo wa Mheshimiwa Jumaa Aweso ili tuweze pia, kuvutia watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara hii ya Tanga – Pangani, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, wakati tunasubiri hiyo lami, kuna kipande cha kutoka Mwahako barabarani mpaka Shule ya Istiqaama, hakipitiki wakati wa mvua. Kwa hiyo, tunaomba angalau wakamwage kifusi wakati ujenzi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni barabara ya kuanzia *Junction* ya Liemba – Kiomoni kwenda Pande - Mjesani hadi Mlingano - Muheza. Ninashukuru Mheshimiwa Shangazi jana aliomba, tunaomba barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami iwe ni *bypass* ili pia, kuweza kuchukua mizigo mikubwa inayotoka Bandari ya Tanga na Bandari ya Mombasa kwenda ndani na nje ya Tanga. Tatu, ni Barabara ya Mabokweni – Maramba – Bombo

Mtoni hadi Kwamndolwa. Tunaomba barabara hii pia, ijengwe kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, naomba pia, nizungumzie Barabara ya Chalinze – Segera, Chalinze – Tanga. Barabara hii sasa hivi ni nyembamba. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia, amefanya kazi kubwa na nzuri ya kuboresha Bandari ya Tanga. Kwa hiyo, barabara ile haikidhi mizigo mikubwa inayotoka Bandari ya Tanga na Bandari ya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba ipandishwe hadhi barabara hii iwe ni *trunk road,* ili sasa iwe na *connectivity* kutoka mizigo ya Bandari ya Tanga, Bandari ya Mombasa na Bandari ya Lamu ili kwenda kuunganisha na sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia, kuzungumzia kipande kidogo tu cha Barabara ya Mabokweni kwenda Mikweni, kilometa moja tu. Hatuombi lami, lakini basi, tunaomba Mheshimiwa Ulega na mimi nakuamini sana, najua uchapakazi wako, najua uchakarikaji wako, najua jinsi unavyojituma, angalau mkawekee hata kifusi, ili barabara hii ipitike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanga ni Jiji, amesema ndugu yangu Mheshimiwa Shangazi. Uwanja wa Ndege wa Tanga siyo mkubwa, kwa hiyo, ndege kubwa hazitui katika Uwanja wetu wa Tanga. Sasa hivi ukitaka ku-*book* ndege ndogo, zinakuja ndege tano kwa siku na zote zinajaa. Watu wa Tanga pia wanataka kupata ndege hizi anazonunua Mheshimiwa Rais, za *ATCL,* waweze kurahisisha maisha yao, lakini kuna wawekezaji wa Bomba la Mafuta wanakwenda na kurudi kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Tanga tunaomba kukamilika au kuongezwa kwa urefu, kitaalamu mnasema *runway* ya Uwanja wa Ndege wa Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, niomba, kwa sisi watu wa Mjini, wakati Mheshimiwa Musukuma ananiambia sihitaji lami, ni kwamba tunahitaji lami, na pia tunahitaji taa za barabarani. Naomba sana, kama vile tulivyofanikiwa kuletewa taa za

barabarani kutoka Pongwe. Mheshimiwa Ulega nakushukuru sana mtani wangu Mzaramo, basi naomba zifike mpaka *Airport* ili sasa mtu akiingia aone kweli, sasa anaingia katika Jiji la Tanga, waja leo kuondoka majaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana Mheshimiwa Ulega, chapaka kazi. Wewe na timu yako, Naibu Waziri, mnafanya kazi nzuri, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu. Tunaendelea na Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil David Mwambe na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, ajiandae.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna ya pekee, ambavyo ameendelea kutusaidia kutupa fedha nyingi kwa ajili ya madaraja hasa Daraja la Sukuma pamoja na Daraja la Simiyu, jumla ya shilingi bilioni 57 zimekuja kwenye madaraja, haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, ameshika nafasi kwa muda mfupi. Hongera sana, tumeanza kuona na tunaamini kwamba, atafanya kazi kubwa pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na wengine, Wakurugenzi wa Taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa ninaomba kushauri Mheshimiwa Waziri, haipingiki sasa kutoka Mwanza mpaka Nyanguge kupanua barabara, kwa sababu, huko ndiko sasa hivi uwekezaji wa viwanda unaendelea; Kisesa, Nyanguge, yote ile ina viwanda vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi foleni kutoka Mwanza mpaka Kisesa ni dakika 40 ndipo unaanza kukimbia. Kwa hiyo, watu wanapoteza muda mrefu kwenda kufanya kazi za kiuchumi. Naomba sana, barabara kutoka Mwanza mpaka Nyanguge upembuzi yakinifu umeshakamilika. Sasa ipanuliwe, kwa ajili ya kuondoa msongamano wa magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Barabara ya Nyanguge kwenda *Lamadi Border,* ni barabara ambayo imeharibika kabisa, viraka vinawekwa juu ya kiraka, gharama kubwa inatumika kwa Serikali kuziba viraka na ajali nyingi zinatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba, Mheshimiwa Waziri Ulega yupo hapa na Katibu Mkuu, kwa kweli, hebu waweke fedha kwa ajili ya ujenzi mpya wa barabara hiyo ambayo ni zaidi ya kilometa 100 itakuwa imekamilika. Kwa sababu, wameweka shilingi bilioni 48 za Daraja la Simiyu, sasa kama barabara hiyo kila siku inazibwa viraka na daraja jipya wamejenga, haitaleta maana. Hebu ijengwe vizuri hiyo barabara ili iweze kuendelea. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mniruhusu nisiruhusu taarifa kwa sababu nina dakika tano. *(Makofi)*

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Barabara ya kutoka Magu kwenda Bukwimba kwenda Hungumalwa, ambayo mwaka 2024 mlitutengea fedha na mkandarasi yupo kazini, nimpongeze. Aliwapongeza jana wakandarasi wazawa, lakini wapo hoi tabaani, naomba walipeni fedha ili waweze kuendeleza miradi hii kwa sababu, wameanza kusimama. Barabara ya Bukwimba – Hungumalwa imesimama, kilometa 10, mkandarasi yupo kazini. Toeni fedha ili aweze kuendelea na barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Barabara ya *Airport* – Nyanguge, ili kupungzua *jam* ambayo ina watu wanaotoka Musoma, na wanaotoka Simiyu kwenda *Airport,* barabara hii imeanza na kilometa 10 kule *Airport.* Tungeomba sasa, mwaka huu wa fedha ziwekewe za kutosha ili kuhakikisha kwamba barabara hii inakamilika kutoka *Airport* mpaka Nyanguge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo barabara ya kutoka Magu – Mahaha ambayo usanifu unaendelea. Tunaomba baada ya

kukamilika usanifu, ziwekwe fedha kwa ajili ya ujenzi wa lami. Barabara hii inafungua uchumi wa Wilaya ya Magu kutokea Simiyu. Kuna kipande ambacho tayari usanifu umekamilika, kwenda Bariadi ambako kwa kweli nako uchumi unafunguka kwa ajili ya Mkoa wa Mwanza. Naomba fedha ziwekwe kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo barabara ambazo zina sifa ya kwenda *TANROADS,* na tumemwandikia na kumpelekea Mheshimiwa Waziri. Tunaomba sasa atume watu wake waje waangalie. Barabara ya Kisesa – Kayenzi ambayo inatoka *trunk road* kwenda barabara ya *TANROADS;* ina sifa zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara inayotoka Matela – Nyakasenge inatoka *trunk road* inakutana kule na barabara ya *TANROADS*; hizo zina sifa zote. Barabara ya kutoka Nyanguge – Kisesa B – Kwimba Boda – Barabara Kuu – Barabara ya *TANROADS*, nayo iingizwe kwenye *TANROADS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara inayotoka Ilungu kwenda Kwimba, ni barabara ambazo zinatoka barabara kuu zinaunganishwa na barabara ya *TANROADS*. Kuna barabara inatoka Kisamba – Simiyu ni barabara inayotoka barabara kuu kwenda Barabara ya *TANROADS*. Barabara hizi zina sifa zote. Hata barabara ya kutokea Magu Buhumbi – Kwimba – Lumeji ni barabara ambazo zina sifa ya kuingia *TANROADS*. Tumeshampelekea Mheshimiwa Waziri, atume watu wake waje wakague kwa sababu zina sifa ya kuingia *TANROADS*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakuona unaniangalia, naunga mkono hoja. Dakika tano ni chache lakini Mheshimiwa Waziri ameeshayaelewa haya mambo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, mtaniwia radhi, sitaruhusu Taarifa kwa sababu tuna dakika tano tano tu.

Tunaendelea na Mheshimiwa Cecil David Mwambe, mniruhusu nifanye marekebisho kidogo kwa Mheshimiwa Timotheo Mnzava, kabla yake ataanza Mheshimiwa Getere halafu atakuja Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pia kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja muhimu sana iliyopo mbele yetu asubuhi hii. Kwa namna ya kipekee kabisa, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazozifanya maeneo yote ya Kusini ikiwemo pamoja na Jimbo la Ndanda. Awamu hii tumeweza kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa zaidi ya 85%. Hii ni kazi kubwa sana ambayo imefanyika katika kipindi kifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niungane na kumpongeza ndugu yetu Mzee Ebenezer Mwapapo, *contractor* ambaye ni mzalendo mkubwa sana. Kwa taarifa tu, ni mlipa kodi mkubwa kati ya walipa kodi waliopo Mkoa wa Mtwara na anafanya kazi nzuri. Tumeona barabara nyingi Mkoa wa Mtwara, Mkoa wa Lindi na maeneo mengine amekuwa akizitengeneza yeye, na tunatambua kazi yake kubwa, lakini ni kiongozi mkubwa ndani ya chama na ndiyo msaada mkubwa sana kwenye eneo letu la kazi na tumeshirikiana vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mambo machache ya kusema hapa. Jambo la kwanza kabisa ni masikitiko yetu baada ya kuondolewa ule mradi wa *EPC+F,* kwa maana ya ujenzi wa barabara kati ya Masasi – Nachingwea – Liwale, hali imekuwa ni mbaya sana. Sasa hivi kutoka Masasi mpaka kufika Nachingwea kilometa 42 tunatumia zaidi ya saa tatu au nne. Tunaiomba sana Serikali iangalie namna bora ya kufanya ili hii barabara sasa ijengwe. Wananchi walikuwa na matumaini makubwa lakini wameanza kukata tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa karibuni barabara ya Dar es Salaam – Ngurukuru – Lindi ilikatika, jambo ambalo lilirudisha nyuma sana Mkoa wa Lindi kimaendeleo. Vilevile kulikuwa na hali mbaya sana kwa wakazi wa Mkoa wa Lindi pamoja na Mtwara. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuhakikisha kwamba daraja lile linajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu tulikuwa tunasema kwamba barabara ile yote inayokuja mikoa ya kusini ni mbovu, inahitaji kujengwa tena upya, tena ijengwe iwe bora zaidi kwa sababu eneo linalojegwa barabara ni karibu sana na bahari. Kwa hiyo, barabara hii imekuwa inaharibika kila mara, tuweke pale tuta kubwa ikiwezekana lakini tutumie utaratibu wa kujenga kwa *asphalt* kama ilivyo barabara ya Iringa – Mbeya na maeneo mengine. Nadhani mnauona ule ubora unaotakiwa, ndiyo ubora hasa sisi tunaohitaji hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo barabara nyingine ambayo tunajaribu kuishauri Serikali, lakini sioni kama wanaamua kuifanyia kazi kwa uhakika mkubwa sana. Ipo hii barabara inayoanzia Masasi – Nachingwea – Liwale – Mahenge, zaidi ya kilometa 120. Barabara hii pia inaweza kukufikisha Ifakara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kama barabara inayokuja Dar es Salaam inakuwa imekatika, na ni sera ya Chama Cha Mapinduzi ni kuhakikisha mikoa inaunganishwa, lakini Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Morogoro haijaunganishwa. Hii barabara tunayoisema ndiyo barabara bora kwa sababu kwanza ipo nje kabisa ya bahari na siyo rahisi kuharibika kwa sababu hata aina ya udongo ulioko kwenye maeneo yale ni mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo jambo lingine ambalo sisi tumeendelea kushauri kila mara. Serikali mfanye uwekezaji mkubwa sana kwenye Bandari ya Mtwara. Sasa ili Bandari ya Mtwara iweze kuwa na tija ya kutosha pamoja na kusafirisha korosho na mazao mengine ya kilimo, kulikuwa kuna haja sasa ya kukamilisha ujenzi wa reli ya kusini ambayo ina kilometa 1,000 zile zinazotakiwa pale kwa nia ya kupeleka mzigo Bandari ya Mtwara. Tunaweza tukapata chuma kutokea Ligangala na Mchuchuma na pia pamoja na makaa ya mawe kutokea Ngapa na maeneo mengine, ili kuleta tija zaidi pale bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliishauri Serikali, kwa kweli reli ya kusini inatakiwa iwe ndiyo reli mama ya Tanzania. Kwa sababu, kuna malighafi inayopatikana yenye uwezo wa kutengeneza reli nyingine. Sasa tunatengeneza *SGR*, tunafanya *importation* ya

chuma na vitu vingine, tunatengeneza na hizo reli nyingine, zote tunafanya *importation* ya chuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatumia vibaya *forex*, tunaagiza chuma kutoka nje wakati tunacho chuma cha Liganga na Mchuchuma. Naomba niseme kwamba chuma pamoja na makaa ya mawe ni masuala ya muda tu, itafika wakati fulani tena makaa ya mawe hayatakuwa yanatakiwa huko duniani. Kwa nini tusitumie nafasi hii tuliyonayo kuhakikisha kwamba tunatumia hiyo chuma vizuri, tuna-*extract* na kuitumia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri katika mikakati yake mirefu ahakikishe sasa kwamba Liganga na Mchuchuma, kwa maana ya reli ya kusini inaanza kujengwa mapema kwa sababu kuna watu wanasubiri kwa muda mrefu. Wengine walikuwa wanadai riba zao, lakini hicho kitu hakifanyiki. Ile sasa iwe kama ndiyo reli mama kwa sababu italeta chuma, tuta-*extract* chuma ambacho kitakwenda kujenga reli nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu madeni ya wakandarasi. Kote kule unapozunguka wakandarasi wanalalamika, hasa zaidi wakandarasi wazawa, wengine wanadai zaidi ya shilingi bilioni tatu na wanatozwa riba na benki…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipatia, lakini kwa msisitizo niseme tuiangalie kwa kina kabisa barabara ya Liwale – Masasi – Nachingwea kwa sababu zinarudisha sana nyuma uchumi wa Wilaya ya Nachingwea.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniface Mwita Getere atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mheshimiwa Josephat Kandege ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nampongeza Waziri wa Ujenzi ndugu yangu Mheshimiwa Ulega, Naibu wake Mheshimiwa

Kasekenya; Katibu Mkuu, Omary na Msonda na watumishi wote wa Wizara ya Ujenzi, wanafanya kazi nzuri sana. Mheshimiwa Ulega hajawahi kushindwa chochote. Tumemwona kwenye Wizara ya Mifugo, anafanya kazi vizuri sana. Sasa hivi anatembea kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais hasa kwa Jimbo langu la Bunda na kwa Mkoa wa Mara kwa ujumla. Tunampongeza kwa shilingi milioni 56 ya Barabara ya Makutano – Nyamswa – Sanzati ambayo mpaka sasa hivi tunavyozungumza imeshakamilika. Tunampongeza kwa shilingi milioni 67.2 ya barabara ya kutoka Nyamswa – Bunda – Bulamba ambayo imekamilika. Tunampongeza kwa barabara ya kutoka Bulamba – Kisolya, milioni 53, imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi tunampongeza sana kwa kweli, hamna namna ya kusema zaidi ya kumpongeza kwa juhudi kubwa ambayo ameifanya kwenye barabara hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ya Barabara ya Sanzati – Nata. Kwa kweli hili ni tatizo kubwa, na Mheshimiwa Kasekenya ameshafika pale, na takribani Mawaziri wote, labda Mheshimiwa Ulega ndiye ambaye hajafika pale, lakini wote waliokuwepo wameshafika pale, lakini barabara ile imeshindwa kukamilika. Wale watu waliwapa thamani ya mradi ni shilingi bilioni 51 na sasa wamewapa shilingi bilioni 6.7. Maana yake ni kwamba bado wanadai shilingi bilioni 44 na *point*. Wale watu wanateseka, wametoka kwenye ile barabara, wameweka lami juu ya barabara kwenye mchanga, wala haifanyi kazi. Inasikitisha sana kutengeneza barabara nzuri kama ile halafu tumeshindwa kuimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile barabara ndiyo barabara inayotoka Makutano – Sanzate – Nata – Mugumu, imeshindwa kukamilika. Tuelewe hapo wote, Mbuga ya Serengeti ni 80% ya Mkoa wa Mara, ndiyo wanaokaa pale ndani, lakini Mji wa Mugumu kuja Musoma hauna barabara ya lami. Kwa kweli kuna vitu vingine vinasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hii barabara ya Nata – Sanzati, kwa kweli kama wanataka kutukwamisha kwenye Ubunge ni hii barabara. Tunaomba watuokoe kwa sababu hali ni mbaya. Huwezi kutengeneza barabara miaka yote hiyo na haikamiliki na tumetumia hela nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali sana, naomba Mheshimiwa Ulega atoe fedha. Nimesikia juzi kuwa wanawapa shilingi bilioni mbili, wapatie ili waendelee kufanya hiyo kazi. Kuna changamoto nyingine ya barabara ya kutoka Bukama – Salama Kati – Kulusanga – Mihingo, halafu inatoka Mgeta – Mhingo – Mikomalio. Tuliomba shilingi bilioni 1.4 hawajatoa mpaka sasa hivi, na ile barabara imekwenda *TANROADS*. Tunaomba hizo fedha ambazo *TANROADS* waliomba, wawape ili wafanye kazi ile, barabara iishe. Tafadhali sana Mheshimiwa Ulega, nakuamini kwenye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya kutoka Balili – Mgeta ambayo inafanyiwa tathmini kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami. Tunaomba hiyo tathmini ifanyike haraka ili barabara iingie kwenye lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mambo mengi hapa yanazungumzwa. Nilikuwa natazama wenzetu wa Shelisheli, wenzetu wa Mauritius, wenzetu wa Congo, wanafanyaje kwenye wakandarasi wazawa? Wana sheria inayosema hivi, "ili mkandarasi wa nje afanye kazi kwenye nchi, lazima awe na mkandarasi wa ndani." Sisi hapa mnasema *subcontract* wawepo, lakini wanakwepwa. Hivi kweli inawezekanaje tukope shilingi bilioni 30, shilingi bilioni 300 au shilingi bilioni 400 kutoka nje, tuzilete ndani ya nchi yetu, halafu mtu huyu huyu kutoka nje aje afanye kazi arudi na hizo hela? Hivi inawezekanaje hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani tukope fedha kuja ndani, halafu tumpe mtu kwenda kukaa nazo, haiwezekani. Kwa hiyo, tuweke sheria kwamba kila mkandarasi wa nje sheria yake ni kwamba awe na mkandarasi wa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kufanya mradi wowote; hawa wakandarasi mnaosema wa shilingi bilioni 10, au shilingi

bilioni 50, waungane wawe sasa kwenye viwango hivyo. Kila mkandarasi kutoka nje awe na mzawa kutoka ndani ili waweze kufanya kazi ili hela zikiletwa hapa, nyingine zibaki hapa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Getere. Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, atafuatia Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Emmanuel Peter Chereheni ajiandae.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye anaendelea kutustahilisha sisi wote humu ndani miongoni mwa Watanzania walio wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anafanya kazi kubwa na nzuri kwenye sekta zote ikiwemo kwenye sekta hii ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nampongeza kaka yangu Mheshimiwa Ustaadhi Abdallah Ulega kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kwenye nafasi hii ya kuwa Waziri wa Wizara hii. Mheshimiwa Ulega ni mtu mzuri, mtu rahimu, mchapakazi, hatuna shida naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tu Mwenyezi Mungu amsaidie dude hili linaloitwa ujenzi lisimbadilishe, aendelee kufanya kazi yake vizuri. Pia tuipongeze timu yote ya Wizara ya Ujenzi, kwa maana ya Naibu Waziri, Katibu Mkuu na pia Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* kwa kazi nzuri na kazi kubwa ambayo anafanya kwenye maeneo yote ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mchango kwenye maeneo machache. Eneo la kwanza niongeze na kukoleza sauti kwenye maeneo ambayo Mheshimiwa Shangazi aliyasema jana na Mheshimiwa Ummy ameyasema leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Handeni – Kiberashi – Mtoro ni barabara ambayo sisi watu wa Tanga tunaamini ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa mkoa wetu na kwa uchumi wa nchi yetu. Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa kwenye bandari. Bila kuwa na uhakika wa barabara hii, kazi kubwa ya kwenye bandari haitakuwa na matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kazi inayoendelea kufanywa kwenye baadhi ya vipande kwenye barabara hii kwa sasa. Pia natambua maelekezo aliyoyatoa Mheshimiwa Rais na ameyarejea jana vizuri sana kwenye hotuba yake. Tunaomba yafanyiwe kazi aliyosema Mheshimiwa Rais, yafanikiwe ili ndoto za watu wa Tanga na manufaa ya kazi kubwa ya uwekezaji inayofanyika kwenye bandari yaweze kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni kuhusu Barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge. Barabara hii ni muhimu sana kwa ajili ya kuufungua Mkoa wa Tanga, kufungua uchumi wa Tanga, hasa hifadhi yetu ya Saadan kwenye kukuza utalii. Tunatambua kazi inaendelea kufanyika, tunaomba mwendelee kumsimamia mkandarasi, kazi hii ifanyike vizuri kwa manufaa ya mkoa wetu na ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa barabara ya Soni – Bumburi – Dindira – Korogwe, hii barabara tumeipigia kelele sana. Tunafurahi leo ninachangia tofauti kidogo na mchango wangu wa mwaka 2024, kwa sababu nimeona kazi iliyoanza kufanyika kwa sababu Serikali tayari ilishatangaza zabuni ya kumpata mkandarasi wa kufanya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba nisisitize hapa, Mheshimiwa Waziri aongeze spidi ya kazi, anakwenda pole pole. Wiki iliyopita niliuliza swali hapa Bungeni kuhusu barabara hii, Naibu Waziri alinijibu kwamba ipo kwenye hatua za manunuzi. Sasa hii kesi sisi watu wa Tanga, watu wa Korogwe na Bumbuli tulishaiacha, tumemkabidhi mwenyewe, mwenye Wanakorogwe wake, mwenye Bumbuli wake ambaye sio mwingine ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 24 ya mwezi wa Pili Mheshimiwa Rais akiwa Lushoto, Mheshimiwa Waziri alikuwepo, akawaambia watu wa Korogwe na watu wa Bumbuli juu ya barabara hii. Naomba ninukuu maneno ya Mheshimiwa Rais, "Nataka niwaambie, tarehe 6 ya mwezi ujao wa Juni, 2025 tunafungua tenda kutafuta mkandarasi na barabara itaanza kujengwa; na tunaanza kujenga kilometa 22 kuanzia Soni – Bumbuli na kilometa 9.3 kwa Meta – Shemshi, tutakwenda pole pole. Tutaanza hapo na polepole tutakwenda." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni maneno ya Mheshimiwa Rais. Sisi humu ndani tumeacha hii kesi kwa Mheshimiwa Rais, ametoa ahadi na aliwaahidi watu wa Korogwe na watu wa Bumbuli. Mheshimiwa Waziri bado kasi kwenye kazi hii sioni kama ni ya kuridhisha, tunaomba waongeze kazi ili jambo hili liweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine, tunayo barabara ya kutoka *Old Korogwe* – Magoma – Mashewa – Bombomtoni – Mabokweni. Barabara hii ni muhimu sana, na kaka yangu Mheshimiwa Kitandula amesema hapa kwa zaidi ya miaka 13 kabla hajaingia Serikalini. Mimi nimeisema kwa takribani miaka saba, au sita sasa hivi, lakini pia ilikuwa na ahadi za viongozi wetu wa dini; Shehe Mkuu wa Tanzania ameisemea sana barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ulega, tukiwa na Mheshimiwa Rais, Tanga, tulifanya vikao mimi, yeye na Shehe Mkuu kuhusu barabara hii. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, nimeona kwenye hotuba yake ukurasa wa 84 ameeleza kwamba kwenye mwaka wa fedha unaokuja tunakwenda kuanza ujenzi wa barabara hii kilometa 10 za kutoka *Old Korogwe* mpaka Kwa Mndolwa na Kilometa 10 za kutoka Mabokweni – Maramba. Jambo hili ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mmoja tulifikiri tukasema, tumesema sisi Wabunge hawakutusikia, Marais wameahidi hawakufanya, na viongozi wa dini wakasema. Tukajiuliza, wenzetu hawa wanataka aseme nani ili wamsikie? Leo tumeona kwenye kitabu cha Mheshimiwa Ulega, tunaomba ahadi hii ikatekelezwe kwa sababu barabara hii ni barabara muhimu sana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naiomba Serikali iongeze kasi ya barabara ya kutoka Ndungu – Mkomazi. Kwenye hotuba yake…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** …amesema imefika asilimia 2.4 tuongeze kasi, barabara hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mnzava, kwa mchango wako. Mheshimiwa Josephat Kandege atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya ya kuweza kusimama na kuchangia katika bajeti hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa nzuri ambayo anaifanya kuhakikisha kwamba nchi yote inapitika. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wasaidizi wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nitakuwa na mchango katika maeneo mawili au matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza, ni ukweli usiopingika, na Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri analijua, juu ya umuhimu wa ujenzi wa barabara ya lami kuanzia Kasesha Boda – Matai. Barabara hii ni ya jumla ya kilometa 60 yenye thamani ya bilioni 37.353. Fedha ambayo imeshalipwa ni shilingi bilioni 6.943, fedha ambayo inadaiwa kwa maana ya *certificate* ambayo inasubiriwa kulipwa ni shilingi bilioni 13.027. Hivi

ninavyoongea, mkandarasi hayupo *site* kwa sababu anadai fedha hii ili aweze kurudi *site*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii umuhimu wake hakuna mtu ambaye anatilia mashaka. Ili kuondokana na msongamano wa malori ambayo yapo mengi sana Tunduma. Ufumbuzi wa haraka ni kuhakikisha kwamba barabara hii inakamilika. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri katika *certificate* ambazo ni za kuhakikisha kwamba zinafuatiliwa na zinalipwa ni pamoja na hiki kiasi cha shilingi bilioni 13.027. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa barabara hii naomba tu nitoe takwimu jinsi ambavyo imekuwa ikileta mapato kwa *TRA,* kwa maana ya *customs*. Mwaka 2021/2022 barabara hii tuliweza kukusanya kiasi cha shilingi bilioni tu, lakini baada ya ujenzi kuanza, mwaka 2022/2023 *TRA* wamekusanya jumla ya shilingi bilioni nne; mwaka 2023/2024 wamekusanya shilingi bilioni 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni nini? Barabara hii ikikamilika kwa ujenzi wa kiwango cha lami, maana yake ni kwamba, yale malori yote ambayo yanatakiwa kwenda Rwanda, Burundi, Mwanza, Uganda, yale ambayo yanatoka Zambia, *South Africa,* hawatapita Tunduma. Makusanyo yatakuwa makubwa sana na watakuwa wamepunguza umbali mrefu badala ya kuzunguka Tunduma, na msongamano ambao upo Tunduma itabaki ni historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande cha pili ambacho ni kilometa 30 tayari mkandarasi ameshasaini, lakini hawezi kuingia kwa sababu hajalipwa *certificate* ya kwanza. Thamani ya *project* ni shilingi bilioni 36.365, *advance payment* ili aingie kazini ni shilingi bilioni 3.525.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa barabara hii ikiwa inaunganisha nchi hizo ambazo nimezitaja na ili kupunguza umbali huo ambao watu wanalazimika kupita, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, barabara hii ipewe kipaumbele ili kama Taifa tuanze kuchuma fedha ambayo *obvious* iko, inapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba nieleze juu ya namna bora ya kuhakikisha kwamba msongamano wa malori unapungua Tunduma. Mheshimiwa Rais alivyokuwa kwenye ziara mwezi wa Saba mwaka 2024, aliridhia umuhimu wa kuunganisha kipande cha kutoka Laela. Mheshimiwa Sangu anajua, wameshaanza upande wa kwake, ni jumla ya kilometa 90 ili barabara hii ianze kujengwa kwa kiwango cha lami, tuunganishe ili tupunguze msongamano ambao uko Tunduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ikiunganishwa, tafsiri yake ni kwamba tunaenda kuunganisha pamoja na *Kasanga Port*. Tafsiri yake, kile alichokuwa anakisema Mheshimiwa Conchesta, ukiwa unataka kwenda Lugumbashi hulazimiki kwenda Kalemie. Kalemie ni kilometa 1,000 na ushee, lakini huku tunaongelea kilometa 480. Hivi tufanyeje ili tuweze kufika *DRC* bila kupita Zambia? Ni kuhakikisha kipande hiki kinajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tuhakikishe bandari ya asili kwa tafsiri aliyokuwa amefanya Mbelgiji, ni *port* iliyoko eneo linaitwa Mulilo na wala siyo Kalemie. Kalemie ni mbali sana. Mnaitafuta *Congo* ipi ambayo haina mazao ambayo tunahitaji kama Taifa? Njia ya *shortcut* ni kupita *Kasanga Port*. Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi analijua, na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kwa kushirikiana wahakikishe zile kilometa chache ndani ya *DRC* tunazijenga kwa sababu wanufaika wa kwanza ni sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi barabara ambazo nimezitaja zina manufaa makubwa sana kiuchumi. Mheshimiwa Waziri. Katika hiki kipande cha pili, wananchi wa Vijiji vya Tatanda, Kaluko, Kasesha pamoja na Katete, wameahidiwa fidia ili ujenzi uanze. Naomba hili lifanyike na wananchi wako tayari kupisha ili kazi nzuri ya kuunganisha kwenda Zambia, lakini wakati huo kwenda upande wa pili wa *DRC,* inafanyika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, nadhani itoshe ili yatiliwe uzito mkubwa katika bajeti hii. Mheshimiwa Waziri, uhakikishe yanaenda kufanyiwa kazi. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kandege. Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma. Mheshimiwa Mrisho Gambo, ajiandae.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukurani nyingi kwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa fedha alizowapelekea wananchi wa Ushetu. Vilevile, natoa shukurani kwa Mheshimiwa Waziri, na Naibu Waziri kwa jinsi ambavyo wanatupa upendeleo wananchi wa Ushetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukurani nyingi kwa Meneja wa *TANROADS* Mkoa wetu wa Shinyanga, *Eng.* Samweli Mwambumbu. Kijana anafanya kazi kwa kujitoa kwa kusimamia fedha na miradi mikubwa ambayo imeletwa kwa wananchi wa Ushetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa madaraja manne ya shilingi bilioni 18 kwa wananchi wa Ushetu. Kwa kweli umetutendea haki. Kazi inafanyika vizuri, wakandarasi wako kazini, Meneja wetu wa mkoa na timu yake na vijana wake wanawasimamia vizuri kabisa. Kwa hiyo, tuna uhakika yatakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daraja la Mwabomba ambalo lilikuwa ni kero kwa wananchi lina mkandarasi, Daraja la Ubagwe lilikuwa kero kwa wananchi, lina mkandarasi, Daraja la Kasenga – *Igombe River* nalo lina mkandarasi, na Daraja la Uyogo – Ng’hwande na lenyewe tayari lina mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, nina barabara yangu ya kutoka Tulole - Chona - Chambo. Ni barabara ya zaidi ya kilometa 15, kutoka Kahama kwenda Tulole, ukiianza tu Ushetu imeondolewa *TANROADS* ikarudishwa *TARURA;* ukimaliza Chona ukaingia Tabora pale, inaingia *TANROADS*. Hiki kipande kimenichonganisha sana na wananchi. Nimelia sana, lakini pia *RCC* imesema sana, hebu kirudishwe *TANROADS* kiendelee kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pale namshukuru sana Meneja wangu, anaendelea kujitolea kukitengeneza, lakini ni kipande ambacho kinatuumiza sana na kutuchonganisha na wananchi. Naomba kirudishwe *TANROADS.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nina barabara yangu nimeiomba sana na *RCC* imepitisha zaidi ya mara mbili. Barabara inayotoka Nyankende pale Mwadui – Nyambeshi – Bunanda – Imalabupina – Kalo (Bulungwa) – Sabasabini - Mpunze mpaka Nyandekwa, ni kilometa kama 76. Hii barabara nimeiombea sana kwenda *TANROADS.* Ni barabara ambayo inajenga na kusimamia uchumi wa Halmashauri ya Ushetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa barabara yangu ya kutoka Mwabomba inayokuja Nyankende mpaka Ulowa, mpaka *Igombe River,* wamenipandishia *TANROADS* inaendelea kutengenezwa. Sasa naomba na hii barabara waichukue pia, kwa sababu ndiyo mhimili mkubwa wa Halmashauri ya Ushetu na yenyewe waipeleke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nina barabara yangu ya kilometa 54 ambayo ipo kwenye Ilani na pia, kila mwaka ipo. Naibu Waziri, Mheshimiwa Kasekenya anaijua na ameshakuja kuteimbelea. Nimeiombea lami na kwenye Ilani ipo. Leo ni mwaka wa tano, mwaka jana waliingiza, wakatenga kama shilingi bilioni tatu, lakini hakuna kilichofanyika. Basi nipewe na mimi, unajua Ushetu ni eneo ambalo lina uzalishaji mkubwa, lakini hatuna hata ile lami ya kupigia picha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2024 Mheshimiwa Naibu Waziri amenipa mita 500 tu pale Uyogo, lakini sasa hebu nisaidiwe, kuitengeneza angalau hata kidogo kidogo waitengee fedha. Naridhika na fedha wanazonipatia na ninawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, lakini basi hebu nitendeeni haki kwa hizi kilometa 54 za barabara inayotoka hapa Kahama – Nyandekwa, inapita Ukune inaenda Kisuke – Nyamilangano mpaka Uyogo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi angalau waanze kuijenga taratibu kwa kiwango cha lami kwa sababu waliahidi wenyewe.

Mheshimiwa Rais ameahidi mwenyewe, amepita pale akaona umuhimu wake na kwenye Taarifa ya Itifaki ya Mwenge wameiona, wananchi walilalamika sana. Naomba tutendewe haki angalau ianze kujengwa kidogo kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, niliomba taa za barabarani pale Nyamilangano. Mheshimiwa Naibu Waziri aliniahidi mwaka 2024, na kwenye swali langu la msingi alisema ataweka. Naomba nipewe basi hizo taa pale Uyogo na pia zile taa za barabarani pale Nyamilangano, angalau wananchi wangu pia waone sasa kazi ni kubwa. Pamoja na fedha wanazonipatia, na zile taa waniwekee pale barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa barabara yangu ya kilometa 30 ya kutoka Uyogo kwenda Ulowa imepandishwa na yenyewe kwenda *TANROADS* na imeanza kutengenezwa, lakini shida iliyopo, barabara ile bado ni finyu na ni ndogo. Naomba sasa ipanuliwe kwa sababu wananchi wangu wanapata ajali sana katika eneo hilo. Ipanuliwe iingie kwenye kiwango cha barabara ya *TANROADS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nawaomba, pale Kahama kuna barabara ya kwenda...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Mrisho Gambo na Mheshimiwa Kaboyoka ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Ulega, kwenye nafasi yake, kwa kweli amefanya kazi

kubwa kwa kipindi kifupi, lakini mimi na yeye tuna jambo letu. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, atukumbuke kwenye kipande changu cha lami cha kilometa 20 kutoka Nkome. Najua kuna changamoto ya fedha, lakini Mungu akijaalia akipata *advance* naomba atukumbuke, kwa sababu wakandarasi wako *site* tunasubiri hiyo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nashauri, najua tunaenda kufungua Daraja la Busisi. Hili daraja wafaidika wakubwa ni watu wa ng'ambo, maana yake Sengerema, Geita, Bukoba, na Kigoma. Sisi kwetu hili ni jambo la kihistoria, siyo jambo la mzaha, na siyo jambo la kawaida kama unavyofikiria. Ni jambo kubwa sana na tunahitaji kuhudhuria sherehe hizi ambazo Mheshimiwa Rais atakuwa mgeni rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ufunguzi wa ujenzi wa daraja ulifanyika Misungwi upande wa Mwanza na sisi tumejipanga kupeleka watu kwenda kumshangilia Mheshimiwa Rais na kumpongeza kwa kazi kubwa aliyoifanya. Mpaka sasa mimi jimboni kwangu kuna mabasi zaidi ya 30, wanasubiri tu tarehe ya Mheshimiwa Waziri, watatangulia hapo siku tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba, ili tuwe *fair*, sherehe hizi zifanyike upande wa Busisi Sengerema ili iwe rahisi watu wa Kigoma, Kagera, Geita na Mwanza nao wavuke tukutane, siyo kila mara mnatuvusha kwenda Mwanza. Kwa hiyo, naomba sana wanapoandaa sherehe hizi, zifanyike upande wa Busisi Sengerema. Eneo linatosha, basi tufanyie hapo ili na sisi tuweze kupata nafasi ya kumwona Mheshimiwa Rais wetu na kumpongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kale Kakiingereza kake kale alikokafanya kwa Wachina Dar es Salaam. Safi sana Mheshimiwa, kamefanya kazi. Naona Wachina sasa waliogopa kile Kiingereza, wamekimbia kwa kweli, lakini nina ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wote tunapita kwenye hiyo barabara. Hebu fikiria mtu anayetoka *Airport* ya Dar es Salaam anakaa Mbweni, kama itaisha hiyo barabara mpaka

Mbweni na Tegeta, nataka uniambie ukipita kuanzia *Airport*, unazionaje zile kona? Maana ninaona kama tunarudishwa kucheza *twist;* unakata kulia, unakata kushoto, unakata kulia mpaka unafika Mbweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukishuka usiku, huwezi hata kulala. Ukipitiwa usingizi kidogo tu imekata kona, imekata kulia. Mheshimiwa Waziri ukipita tena ninaomba uangalie hata ule uwekaji wa zile kingo za Barabara, zimeshagongwa karibia zote kuanzia mwanzo huku walikomaliza mpaka unafika mjini. Kila *angle* imegongwa. Sasa nadhani tuna ma-*engineer* wazuri na Besta yuko hapa, oneni namna ya kuzipunguza zile kona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajaribu kulinganisha na nchi nyingine. Sioni mahali ambapo kuna hiyo barabara ya *design* hiyo, kuzunguka kuanzia mwanzo mpaka mwisho, unakata kona tu. Sasa naona nishauri kwamba, kule upande wa kulia na kushoto, zile kingo wajaribu kuzipunguza kwa kweli, zinatusababishia ajali. Ninyi wenyewe ni mashahidi, aidha mmeweka makubwa sana au imekuwaje, sijui. Mtaona jinsi gani mtakavyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, ni kweli kama Waheshimiwa Wabunge tunavyosema, mimi binafsi kwenye jimbo langu pamoja na kwamba sina lami, ndiyo nakuomba nisaidiwe, lakini tunaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa fedha nilizopokea, kwa barabara zangu zilivyo nzuri muda wote wa mvua za masika. Tunaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyopo, unafahamu tunaye mkandarasi kuanzia Sungusila – Nzera – Nkome, barabara hiyo tayari ina Mkandarasi wa Kichina kilometa 30 kutoka Geita kuja Sungusila zenyewe zimefanyiwa *maintenance*. Kule aliko Mchina, hakuna *maintenance,* barabara ni mbaya kwa kweli. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aone namna ya kutusaidia kuweza kumsimamia Mchina ili aweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, sisi tunaungana na Buchosa na Sengerema. Barabara ya Buchosa – Sengerema – Nkome ni barabara ya kimkakati sana. Yaani haya maeneo ndiyo yanailisha Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, naomba tutakapoenda kufungua daraja letu, tusiende sana kwenye bure. Hili nalisema kwa uzalendo tu. Tumefanya kazi kubwa sana kwenye lile daraja. Ni daraja kubwa la kihistoria. Mimi ninapitisha gari zangu pale kama 30 au 35 kwa siku. Tunalipa shilingi 10,000, shilingi 15,000 mpaka shilingi 80,000 hadi shilingi 100,000 kwa malori. Sasa naomba tusidekeze sana kwenye bure. Tuweke tozo hata shilingi 5,000. Watu wasilipe, lakini magari yale yanayofanya biashara tulipe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunahitaji madaraja mengine. Kuna daraja la kutoka Mwanza kwenda Kamanga. Tunahitaji nako tuwekewe daraja kubwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Musukuma, tumekupata. Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Kaboyoka na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle ajiandae.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo ambalo linaguswa kwa kiwango kidogo sana na Wizara ya Ujenzi na *TANROADS* ni pamoja na Jimbo la Arusha. Ukizungumzia Barabara ya Mianzini – Ngaramtoni kilometa 18, Jimbo la Arusha tuna meta 200 tu, nyingine zote ziko Wilaya ya Arumeru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wake kwa miaka yote mitano toka mwaka 2020 mpaka sasa tumekuwa tunajenga hoja kwa Barabara yetu ya kutoka Arusha *Airport* kwenda Kilombero,

inatakiwa ijengwe kwa njia nne. Kwa miaka yote mitano, Serikali imekuwa inafanya usanifu, na mpaka leo tumeona taarifa ya Mheshimiwa Waziri inatuambia usanifu umekamilika ndani ya miaka hiyo mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa kwenye bajeti hii Mheshimiwa Waziri atuambie sasa baada ya kukamilisha usanifu, ni lini watatangaza *tender* apatikane mkandarasi na hasa ukizingatia kwamba tunaenda kwenye masuala ya *AFCON,* na Mheshimiwa Dkt. Samia ameweka vizuri masuala ya utalii pale kwenye upande wa *Royal Tour?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, hiyo barabara ikitengenezwa itasaidia pia kuondoa mafuriko. Kuna Kata kama *ya Unga Limited*, Sombetini, na Osunyai, mafuriko ni makubwa sana. Barabara ikijengwa, tunaamini kwamba mitaro itatengenezwa na changamoto kwa wananchi itaweza kuondoka. Pia, tunaomba wakalipe fidia angalau kwa kipindi hiki wakati tunasubiri na michakato mingine ya kujenga hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusiana na Barabara ya Arusha – Kibaya – Kongwa, na yenyewe pia tumeipigia debe kwa miaka yote mitano. Mara ya kwanza mkataba ulisainiwa kupitia *EPC+F*, zikatokea changamoto. Umekuja tena mradi mwingine, mnasema sanifu na kujenga lakini mmeshasaini mkataba kwa kilometa 70 na hapa Bungeni wamejibu mara nyingi sana, lakini hadi leo tunavyozunguza, mkandarasi bado hajafika *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itatusaidia kupata barabara ya njia nne kutoka Kona ya Mbauda, kushuka mpaka kule chini Kwa Morombo ambako tunakwenda kujenga stendi ya kisasa. Itasaidia pia kuondoa na mafuriko kwenye eneo la Kata ya Sombetini pamoja na Kata ya Osunyai. Kwa hiyo, sasa tuambiwe huyo mkandarasi atakwenda lini *site* ili itusaidie kwenye masuala ya *AFCON* na kazi yote ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia anaifanya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kuhusiana na mafuriko. Tunajenga barabara nzuri. Mfano, Barabara ya Sakina – Tengeru, imejengwa vizuri, lakini maji yameelekezwa kwa wananchi. Ukiangalia Kata ya Ngarenaro, Kata ya Sakina, ukiangalia Kaloleni yenyewe, ukienda kule Baraa, na ukienda Kimandolu, kote mvua ikinyesha ni vurugu tupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunategemea sasa wakafanye *study* ya kutosha ile yale maji yanayopita pale wayatafutie njia ya kupita yaende kwenye mitaro au kwenye mito kama Mto Nduruma ili tuweze kuwaondolea wananchi adha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunashukuru kuona kwamba kuna baadhi ya jitihada zimeanza mfano kwenye Kata ya Terrat, kuna barabara ya Namba Sabini kule kwenye Mtaa wa Olkungu. Tumeona tayari mkandarasi amepatikana lakini alikwenda akachimba chimba, baadaye ameweka greda pembeni kazi haiendelei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba akasukumwe ile kazi ikafanyike ili wananchi wa Olkungu pale Namba Sabini wasipate changamoto hiyo. Pia, Mitaa kama ya Bondeni Kati, eneo la Mpambazuko pia lisipate changamoto hiyo ya mafuriko pamoja na Mtaa wa Laitayok kwenye Kata hiyo ya Terrat. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na malipo ya wakandarasi. Tunajua *TANROADS* na Wizara ya Ujenzi wangependa kujenga barabara zote nchi nzima, lakini ili wajenge barabara wanahitaji kuwa na fedha. Tumekuwa na taarifa kwamba wakandarasi wetu wana changamoto kubwa ya kupata malipo ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba Wizara ya Ujenzi ikae na Wizara ya Fedha ili itoe kipaumbele cha kutosha, maana najua wakipata fedha kusukumana na wakandarasi ili kazi ziende ni jambo ambalo wana uwezo nalo. Kama hamna fedha mkandarasi ameshafanya kazi, ametoa *certificate* kama fedha hakuna, kazi haiwezi kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kikubwa zaidi wakandarasi wetu wanapata hasara, wamekopa fedha kutoka benki, na nilikuwa nimejenga hoja kwenye Bunge hili, wakandarasi wa nje wakipewa kazi wanawekewa na riba. Serikali ikishindwa kulipa fedha kila baada ya muda riba inaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wakandarasi wa ndani na tumesema Serikali yetu inaangalia wazawa, kwa nini wao wakipewa kazi, Serikali ikichelewa kuwalipa, nao tusiwawekee riba ili mwisho wa siku zile riba wanazopata kwenye maeneo ya benki na maeneo mengine zisiendelee kuwaumiza? Wako baadhi ya wakandarasi ambao wameweza kuuza nyumba zao, mali zao na wamefilisiwa kwa sababu ya kucheleweshwa kulipwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu Mheshimiwa Dkt. Samia anawapenda Watanzania, anawapenda wananchi na anawajali wakandarasi wazawa. Sasa wanaomsaidia kwenye Wizara ya Fedha na Wizara ya Ujenzi, tumsaidie Mheshimiwa Rais kuweka mipango mizuri zaidi na tusitangaze *tender* kama hatuna fedha. Tusim-*award* kazi mkandarasi kama hatuna fedha. Kwa kufanya hivyo tunawarudisha nyuma badala ya kwenda kuwasogeza mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la kumalizia, kuna changamoto kwenye upande wa fidia. Barabara yetu ya Arusha *Bypass* ile kwenye Kata kama za Moshono na kata nyingine, wako wananchi ambao maeneo yao yamezuiliwa na Serikali kwa muda mrefu, wanaambiwa watalipwa fidia. Mwananchi anashindwa kuendeleza, kujenga na anashindwa kuuza na Serikali haimwambii ni lini itamlipa fidia. Naomba mtuambie ni lini mtalipa fidia na ikishindikana, basi wale wananchi wawe huru na maeneo yao na Serikali ikiyahitaji watakuja kule.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa sababu ya changamoto ya muda,

nakushukuru sana na nitaunga mkono hoja baada ya kupata majibu ya kuniridhisha kulingana na masuala ambayo nimeyaelezea.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mrisho Gambo. Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle. Mheshimiwa Boniphace Butondo, ajiandae.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nichangie Bajeti ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamesimama hapa wakimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Wizara hii kwa kazi nzuri ambazo zimefanyika kwenye majimbo yao. Kwa upande wangu ninapata kigugumizi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata kigugumizi kwa sababu maalum. Kuna mchezo unaofanyika katika Jimbo la Same Mashariki kuhusiana na barabara hii ambayo imepangwa kwenye bajeti 2025/2026. Mchezo huu umeanza muda mrefu sana, kiasi inaonesha kwamba Jimbo la Same Mashariki, barabara zake zinafanyiwa hujuma ya makusudi, kwa maana zimeshapangwa kwenye bajeti, hii ni mara ya tatu, lakini utekelezaji wake hauonekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niwape *scenario* inayoweza kufanya tuone kwa kweli kuna mchezo mchafu unafanyika katika barabara hii. Kwa hiyo, mchango wangu uko kwenye sura ya tatu; Mpango wa Bajeti ya mwaka 2025/2026 na unazungumzia kuendelea na ujenzi wa barabara ya Same – Kisiwani – Mkomazi kilomita 97. Ndungu – Mkomazi wameweka vipande viwili kilomita 36, Same – Kisiwani kilomita 56.8, jumla wanazungumzia kilomita 92.83 na bajeti yake ni shilingi bilioni sita kama nimesoma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika barabara tajwa hapo juu tarehe 18 Agosti, 2021, Serikali ilisaini mkataba wa kutengeneza kipande cha Mroyo – Ndungu. Katika kujibu swali langu la msingi

Na. 22, hapo tarehe 31 Februari, 2024, majibu ya Naibu Waziri wa Ujenzi kwa wakati huo alisema kwamba, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi milioni 860 zilizotumika kwa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara ya Same – Kisiwani – Ndungo – Mkomazi, ambapo aliweka kilometa 96.46 na alisema kazi ilikamilika mwezi Septemba, 2022, ilichukua miaka mitatu kufanya kazi hiyo. Miaka mitatu na shilingi milioni 860. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Naibu Waziri ambaye ninamheshimu na ninampenda sana, aliendelea kusema kuwa, katika mwaka wa fedha 2021, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 6.3 ambazo zilitumika kwa kazi ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa kipande cha kilometa 5.2, nacho hicho kilikuwa Gonja – Ndungu. Aliendelea kusema kwamba, ujenzi ulikuwa umefikia 25% na barabara hii ilikuwa inategemewa ikamilike Juni, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza hivi, kama kilometa 5.2 zimechukua huu mwaka wa nne hazijakamilika, kweli tunafikiria kilometa 92.85 zilizowekwa kwenye bajeti hii zitakamilika? Ni barabara hiyo hiyo, kipande kidogo tu, na hicho kipande kidogo cha kilometa tano kilitengewa shilingi bilioni 6.3, hii kilometa 92.83 kimetengewa shilingi bilioni sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa akili ya kawaida, unasema huu ni usanii. Kama kilomita tano, kwanza imechukua huu mwaka wa nne hazijaweza kutengenezwa, na Mkandarasi bado analipwa. Maana nitawasomea jinsi ambavyo Mkandarasi amelipwa na kazi ilisimama tangu mwaka 2024 Waziri akibu swali hili, na kazi imesimama mpaka leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo tunaletewa usanii wa kusema kilometa 92 zitatengenezwa kwa hela ambayo ni ndogo kuliko ile iliyopangiwa kilometa tano. Kwenye zile kilometa tano, hata kitone cha lami hakuna. Kasehemu kalikotengenezwa ni kujaza mawe, na sehemu hiyo walisema kwamba mkataba ambao ulikuwa uishe baada ya mwaka mmoja umechukua mwaka wa nne, wanasema kwamba walikuwa hawajui kwamba kuna maji chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza, sehemu hiyo walisema imechaguliwa kwa vile ni mbovu. Kwa hiyo, ilitakiwa itengenezwe kwa maana ina matatizo. Sasa ikatengewa shilingi bilioni 6.2. Moja, upembuzi yakinifu haukuwa umefanywa kwenye kipande hicho? Kama ulifanywa, haukuonyesha kama chini kuna maji? Pili, kwa nini mkataba huu ulitolewa kabla ya hata upembuzi yakinifu wa barabara yote haujaisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile kuambiwa shilingi bilioni 5.2 zitatumika kwenye kilometa 5.2, hiyo fedha sasa imekwenda wapi? Ukiangalia huu mradi, ulianza tarehe 1 Septemba, 2021 na ulitegemewa kukamilika Septemba, 2022, lakini mkataba uliongezwa hadi Juni, 2024. Sasa mpaka leo hivi tunavyozungumza hakuna kazi, ilisimama pale pale na gharama ya ujenzi ndiyo hivyo kama nilivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa kazi hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri akijibu swali ilikuwa 55%. Malipo ya awali (tusikilize hapo vizuri) kwa Mkandarasi yalikuwa shilingi milioni 783, malipo ya hati ya pili ni shilingi milioni 896, malipo ya tatu ni shilingi 1,139,150,000, na deni la Mkandarasi ambalo anadai hati ya nne ni shilingi 1,489,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajiuliza, hivi kakipande hako ambako hata pale palipowekwa mawe hapafiki hata nusu kilometa, kama imezidi ni nusu kilometa, huku kwingine kote hakujatengenezwa, na bilioni hizi zimetumika; na hizo bilioni kwenye bilioni sita zilizobaki ziko wapi? Kwa maana Mkandarasi hajalipwa tangu mwaka 2024 mwezi wa Februari, Mheshimiwa Naibu Waziri akilizungumzia pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita nilikuwa kule kuhakiki kwamba Mkandarasi ameanza kazi, hakuwa ameanza. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema hapa kuna uchafu unaofanyika. Kilomita 92 uweke shilingi bilioni sita, kilometa tano uweke shilingi bilioni 6.3, kazi mpaka leo mwaka wa nne 55%, hiyo fedha nyingine imeenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo jana alivyokuwa akichangia Mheshimiwa Halima Mdee alisema, au kuna mfuko mwingine hela

inatoka huku, inaingia huku? Kwa hiyo, ina maana barabara hii inatumika kama shamba la bibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili hiyo, nasema hakuna haja ya kuiweka kwenye bajeti kwa maana mnatuchezea. Malizeni kile kipande, na ionekane hiyo shilingi bilioni 6.3 imetumika kwa sehemu hiyo. Kwa maana mpaka leo hakuna hata kilomita moja ya lami. Hii ni kuonyesha kwamba kwa kweli kuna mchezo mchafu, na haya ndiyo yanasababisha kuomba *Special Audit* kwa *CAG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumalizia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaboyoka, ahsante sana. Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, anafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, ajiandae.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi uliyonipa. Nami niungane na Wabunge wenzangu wengine wote, kwanza kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii ya Ujenzi, Mheshimiwa Abdallah Ulega amekuwa ni Waziri ambaye anafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Godfrey Kasekenya Msongwe ambaye amekuwa Naibu Waziri kwa miaka mitano hapa. Hii ni ishara kwamba anafanya kazi nzuri, tunampongeza sana. Pia nampongeza sana Katibu Mkuu Balozi *Eng.* Aisha pamoja na Naibu Katibu Mkuu, ndugu yetu Dkt. Charles Msonde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetumwa na wananchi wa Jimbo la Lupembe kuchangia mambo mawili katika bajeti hii ya Ujenzi. Jambo la kwanza, wananchi wa Jimbo la Lupembe wamekuwa na kilio cha muda mrefu sana kwa ajili ya hii barabara ya Kibena – Madeke. Barabara hii imeahidiwa tangu mwaka 2000 Awamu ya Tatu, Awamu ya Nne, na Awamu ya Tano kulikuwa na ahadi ya maneno tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nina faraja kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu, kwamba nimesoma kwenye hii hotuba ya Wizara ya Ujenzi ukurasa wa 31 Waziri amesema mambo yafuatayo na ninaomba kuyanukuu. Mheshimiwa Waziri anasema, "katika barabara ya Njombe – Kibena – Lupembe – Madeke kilometa 126, sehemu ya Kibena – Kidegembye kilometa 42, taratibu za manunuzi ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ujenzi, zipo katika hatua ya mwisho." Mheshimiwa Rais ahsante na hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wahenga walisema, moyo usiokuwa na shukrani, hukausha mema yote. Nasi wananchi wa Lupembe tuna imani kubwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwamba hii barabara iliyokwama kwa muda mrefu yeye katika Awamu yake ya Sita atakwenda kuijenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna imani na Mheshimiwa Rais, kwa sababu alituahidi kujenga Makao Makuu ya Halmashauri, amejenga, ameshamaliza. Aliahidi kujenga vituo vya afya, amejenga, ameshamaliza. Aliahidi kupeleka umeme, amepeleka Jimbo zima la Lupembe. Tuna imani na Mheshimiwa Rais, barabara hii atakwenda kuikamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, wananchi wa Lupembe wamenituma pia, pamoja na kutangaza hiki kipande cha kilomita 42, wanashauri pia kutangaza sehemu nyingine ya pili ya kuanzia kule Lupembe ili waje wakutane pale katikati kwa ajili ya ujenzi wa hii barabara iweze kwisha mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, wananchi wangu wa Kijiji cha Nyombo, Kidegembye penyewe, Matembwe, Wanginyi, Lupembe Barazani, Mfiriga mpaka Madeke wanahitaji fidia kwa ajili ya maeneo yao. Juzi nilikuwa kwenye Mwenge kule Njombe, nimekuta kazi ya uthamini wa mali unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la wananchi wa Lupembe, wanaomba maeneo haya yalipwe fidia mapema ili nyumba zao na mali zao ziweze kuwa na thamani sasa. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hotuba yake

baadaye jioni awapatie matumaini wananchi wa Lupembe, hii fidia yao italipwa lini? Kwa sababu uthamini unaendelea kule sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nakumbuka Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja Lupembe pamoja na Waziri aliyepita, Mheshimiwa Ulega ndiyo bado hajafika Lupembe. Barabara hii ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaombe, barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Mkoa wa Njombe na Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Hii barabara inaunganisha mpaka Ifakara kule Mlimba kwa ndugu yangu Mheshimiwa Kunambi mpaka Morogoro kuja hadi Kilosa. Ni barabara muhimu kwa uchumi wa Taifa, ni barabara ya kimkoa. Naomba ipewe uzito kama walivyoahidi kwenye bajeti hii, ujenzi uanze mara moja, wana Lupembe wapate hii barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ahsante na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Butondo, atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Kunambi, Michael Constantino Mwakamo ajiandae.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango katika Wizara hii ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nami niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo nchi yetu imeendelea kupiga hatua kubwa sana kimaendeleo katika sekta mbalimbali, na jitihada kubwa kwa kweli anayoifanya kuhakikisha kwamba Wizara hii inaongezewa bajeti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba miundombinu katika Taifa letu ambao ni uti wa mgongo wa maendeleo wa nchi, inapewa kipaumbele mwaka hadi mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa kazi kubwa kweli wanayoifanya, pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Wizara hii. Kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana, japokuwa changamoto bado zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunawapongeza sana, na kwa namna ambavyo kwa kweli wamekuwa na ushirikiano mkubwa na Wabunge na kwa vyovyote vile tumekuwa tukiwasiliana pale palipo na changamoto na wakati wote wamekuwa wakisaidia kuchukua hatua za haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kwa kweli kumpongeza Meneja wangu wa *TANROADS* Mkoa Ndugu Joel Mwambungu, kwa kazi nzuri anavyosimamia barabara za Mkoa wa Shinyanga, lakini na ushirikiano mkubwa anaouonyesha kwetu sisi Wabunge na hususan mimi Mbunge wa Jimbo la Kishapu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Katibu Mkuu kwa namna ambavyo amefikia maamuzi ya kumthibitisha sasa kuwa Meneja wa Mkoa, kwa sababu amekaimu kwa kipindi kadhaa, lakini kazi yake nzuri, ushirikiano na umoja anaouonesha baina yetu sisi Wabunge, kwa kweli maendeleo ni makubwa na barabara zetu sasa zimekuwa katika kiwango kizuri katika Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nianzie mchango wangu kwa barabara ya Kolandoto – Kishapu. Barabara hii ipo kwenye Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi, na sote tunafahamu Ilani ni mkataba baina ya wananchi na chama. Kimsingi Chama Cha Mapinduzi ndicho kilichoshinda na kikaweka ilani mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa barabara hii ipo kwenye ilani tangu mwaka 2015 – 2020 na 2020 – 2025, lakini barabara hii haijaanza kutengenezwa. Huu mwaka wa fedha 2024/2025 tunaoumalizia ilitengewa jumla ya shilingi bilioni moja kama fedha za kuanzia utekelezaji wa mradi huu. Sasa tumekwenda hatua, barabara hii haijatekelezwa, na hii tunakwenda hatua za mwisho,

lakini kwenye hii bajeti mmeongeza shilingi milioni 900. Hizi fedha sielewi, ni ndogo sana. Sijajua labda ni kwa ajili ya *mobilization* na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nipate majibu sahihi, kwamba barabara hii itakwenda kutekelezwa katika kipindi hiki cha mwaka huu unaoanza 2025/2026? Ama hizi shilingi milioni 900 zilizoongezwa ni kwa ajili ya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, barabara hii ni moja kati ya zile *trunk road*, ni barabara inayotoka Kolandoto – Kishapu – Lalago – Meatu na hii barabara inaunganisha Arusha – Manyara – Singida. Ni barabara muhimu sana, na barabara hii ikijengwa ikakamilika, itaharakisha sana jitihada za kiuchumi katika mikoa hii yote minne. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ione umuhimu wa kuanza kujenga hii barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi imejitabanaisha wazi kabisa kwamba, mkakati mkubwa ni kuhakikisha kwamba wilaya na mikoa zinaunganishwa. Sasa barabara hii ndiyo inayounganisha mkoa na wilaya, Wilaya ya Kishapu ina miaka mingi tunahangaika na vumbi. Kwa nini Serikali isifike mahali ikatekeleza takwa la Chama cha Mapinduzi kwa maana ya Ilani, kuhakikisha kwamba barabara hii inapelekewa lami na tutawasaidia wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri atuambie tu, sijajua wanafanya utaratibu gani, lakini *trafficking* ya barabara hii ni kubwa sana. Kuna magari mengi, kuna malori mengi ambayo yanasafirisha pamba, yanasafirisha kunde; na Mkoa wa Shinyanga tunalima pamba na Kishapu ndiyo inaongoza kwa kulima pamba. Kwa hiyo, kwa kipindi hiki ni vurugumechi, malori yote yanayotoka Singida, yanayotoka Simiyu yanapitia barabara hii, lakini hatuwezi tukaelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka mmoja tumekuwa tukitumia zaidi ya shilingi milioni 600, kufanya matengenezo ya mara kwa mara kwa barabara hii. Kwa hiyo, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuweka lami ili tuondokane na gharama

za matengenezo ya mara kwa mara, isiwe tunatengeneza mara nne kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwahurumie wananchi, kwa sababu inafika mahali wazazi wanajifungua barabarani, kwa sababu barabara hii inaharibika mara kwa mara na inakuwa na mashimo makubwa. Sasa kwa nini tusitengeneze barabara hii? Tunahujumu Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, tunakwenda kwenye uchaguzi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Butondo, ahsante, nakushukuru.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini naomba sana Mheshimiwa Waziri kwenye majumuisho, atoe majibu ya matumaini, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Godwin Kunambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Constantino Mwakamo, Mheshimiwa Maimuna Mtanda...

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Samahani kidogo. Wajiandae Mheshimiwa Maimuna Mtanda, Mheshimiwa Flatei Massay, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga na Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wananchi wa Mlimba wameniagiza leo hii nizungumze kwa habari ya barabara inayounganisha Mikoa ya Pwani na Nyanda za Juu Kusini inayopita Mlimba – Njombe. Wameniagiza nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa utashi wake wa kuelekeza fedha shilingi bilioni 167 ziende zikajenge kilometa 100 kipande cha kutoka Ifakara – Miale – Igima kilometa 62.5 na kipande cha kutoka Miale – Igima – Chita JKT pale makutano kilometa 37.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina furaha ya kusema tu kwamba tayari vipande hivi vina Wakandarasi, na Mkandarasi mmoja huyo wa kwanza kutoka Ifakara – Miale – Igima, ameshaenda eneo la kazi kwa maana ya kwamba, ameshaandaa *camp site* na hivi sasa mitambo iko pale na nina taarifa ya kwamba anajenga nyumba kwa ajili ya wataalamu wanaokwenda kusimamia ujenzi wa barabara hiyo. Hivyo, nina kila sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipande kingine cha kutoka Kihansi - Madeke tangu mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022 kulikuwa na habari ya kwamba tuna fedha kutoka Benki ya Mendeleo ya Afrika *(AfDB)*. Sasa mpaka leo Waziri ingefaa atueleze wananchi wa Mlimba, kile kipande cha kutoka Kihansi – Mlimba kwenda Mpanga, pale Masagati mpaka Madeke kilometa 93 hali ikoje sasa, kwa maana mkandarasi anayekwenda kufanya usanifu na upembuzi yakinifu wa mradi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mlimba pia wameniagiza, na kwa kuwa kaka yangu Mheshimiwa Ulega, yeye ni kaka yangu, nami ni Mjumbe, na Mjumbe hauawi, wananchi wa Mlimba wameniagiza, wamesema leo hii niondoke na shilingi ya mshahara wake. Wameniagiza, nami ni Mjumbe, nasema tu niondoke na Shilingi ya mshahara wake. Kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema nia njema ya Mheshimiwa Rais alielekeza barabara hii ijengwe ndani ya miaka mitatu na mkandarasi amesaini mkataba miaka miwili sasa. Je, kazi hii itakamilika kwa miaka mitatu, na hajaanza kazi? Wangependa kupata majibu ya uhakika, maana majibu kila siku wamekuwa wakipata kwamba hatua ikoje na kwa nini sasa miaka miwili wakandarasi wote wawili hawajaanza kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakipata majibu ya uhakika wameniruhusu niondoe shilingi, lakini bila majibu ya uhakika wamesema niondoke na shilingi ya mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni kaka yangu, lakini mimi ni Mjumbe, na mjumbe hauawi. Anapofanya

majumuisho, wananchi wa Mlimba sasa leo wapo wanafuatilia *TBC live,* wanataka kusikia kauli yake, unakwenda kusema nini kwa habari ya mkandarasi huyu kuanza kazi sasa? Huyo wa kwanza kipande cha kutoka Ifakara kuja Miale - Igima na wa pili kutoka Miale - Igima kwenda Chita wataanza kazi lini? Wakishapata majibu ya uhakika, wameniruhusu niondoe Shilingi ya mshahara wa Mheshimiwa Waziri, na apate mshahara kaka yangu na maisha yaendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine namshukuru Mheshimiwa Waziri, amefanya ziara kwenye Jimbo langu kujionea hali halisi. Sasa nimpe taarifa, lile eneo la Mpanga ambalo sasa barabara imekatika na kuna bwawa hivi, tayari mama mmoja amefariki pale mjamzito. Alikuwa anakuja kupata huduma ya afya kwenye hospitali ya Wilaya ya Mlimba hapa Mngeta, amefika pale barabara haipitiki, na amefariki. Mimi ninamwombea huko aendako Mungu ailaze roho yake mahali pepa Peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi ni kadhia ambazo wananchi wanazipata. Mheshimiwa Waziri *you can feel.* Sasa tangu utoke hamna kilichofanyika. Ninavyozungumza na wewe mpaka sasa ulikwenda kushuhudia, lakini mpaka sasa hali ipo vile. Magari ya kule yamebaki kule na hata eneo lile la Ngwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Ngwasi alipoenda Mheshimiwa Waziri, mpaka sasa kuna magari yaliyotoka Njombe – Mlimba yamebaki. Kwa hiyo, hakuna mwananchi anayefika Ifakara, hakuna mwananchi anayesafiri kwenda Dar es Salaam. Kwa hiyo, hiyo ndiyo hali halisi ya sasa, na Waziri akisema neno moja, nadhani wananchi wa Mlimba watafarijika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili tulikuwa na miradi hapa ya fedha za Benki ya Dunia. Eneo lile la Mpanga lingepaswa kupata fedha zile, lakini nashangaa kwa nini zilikwenda maeneo mengine, lakini Mpanga hawakupata pale bajeti ya daraja la kudumu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende eneo lingine. Nimeyataja maeneo korofi, Ngwasi na Mpanga, lakini niende kwenye eneo la

fedha za maendeleo. Mheshimiwa Waziri labda atueleze wapi tunakwama? Kwa nini karibu mikoa yote hawapelekewi fedha za maendeleo? Kwa mfano Mkoa wa Morogoro, mimi pale nina mradi wa fedha za maendeleo, barabara ya lami kipande cha mita 400 kata ya Mchombe. Hivi sasa mkandarasi alikuja akasembua barabara, ameacha matope barabara haipitiki, na taarifa niliyonayo, mpaka leo pale kwenye ile njia haipitiki sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihitimishe kwa kusema kwamba niombe na nishauri Wizara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda umeisha, ahsante sana.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kuwa na miradi michache ambayo itakamilika kwa wakati kuliko kuwa na miradi mingi ambayo kimsingi haiwezi kukamilika.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba kuwasilisha na naomba niunge hoja mkono kwa sababu ninaamini wewe ni mtu rahimu sana. Utaenda kutupa majibu ya faraja wananchi wa Mlimba leo hii, nami nitasikiliza hapa kwa sababu nitashika Shilingi baadaye. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwakamo, tafadhali.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kama kawaida ya kila mmoja kushukuru. Naishukuru Serikali na Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake wote wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda ni mchache naomba nimweleze Mheshimiwa Waziri kwamba leo nitachangia katika sura ya kumpa salamu nilizopewa nimpe. Pale Mlandizi baada ya jana kuwasilisha hotuba yake, wapo walionipigia simu,

wapo waliompongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais, nami mwakilishi wao nafanya hivyo kwake na kwa Mheshimiwa Rais. Hongereni sana kwa kazi inayofanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia nachukua nafasi ya kushukuru sana kwa sababu nilipoingia hapa nilizungumza habari ya barabara ya Makofia – Mlandizi, Mlandizi – Mzenga mpaka Mwanalumango kwa kila hotuba ya bajeti iliyokuwa mbele yangu kwa kipindi ambacho nimeishi hapa na niliuliza maswali mengi sana juu ya barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maswali na michango hiyo niliyoitoa, na kutokana na hotuba ya jana, baadhi ya watu walinipigia simu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri. Pia, wameniambia nimpe salamu, tena wamenilazimisha nimpe salamu hiyo kwa lugha ya Kizaramo. Kwa kuwa yeye ni Mzaramo, wamenipa methali mbili kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, wameniambia nimwambie kwamba, "*Mkulwa nyamale kalimanduage*." Naye anajua salamu hii amenipa Mzee Matambo, na kwa sababu Bunge hili linasikilizwa na wengi, "*Mkulwa nyamale kalimanduage*", ina kwa maana kwamba, "ukiona mtu mzima amenyamaza, ananyamaza tu kwa kukataa kelele, lakini yapo mambo mengine yanawezekana akabaki na mashaka nayo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee Matambo ameniambia nimwambie methali hii. Pamoja na kumpongeza, anataka kujua fidia ya watu wa Makofia - Mlandizi – Mzenga – Vikumbulu. Pia, pongezi wanayompa, tarehe 4/5/2025 kwenye hotuba yake jana walisikia akisema barabara ya kilometa 23 kutoka pale Mlandizi kwenda Ruvu Stesheni kwenye Stesheni ya *SGR* itasainiwa. Kwenye hotuba, Mheshimiwa Waziri alitumia lugha hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameomba nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba wanamshukuru kwa sababu juzi tarehe 4/5/2025 mkandarasi ameshasaini barabara hii na wamemwona Mlandizi akitembea kutafuta sehemu ya kuweka kambi. Wameniambia nimshukuru sana, ila nimwombe amwambie awahi kuweka kambi wamwone kwa sababu ujenzi

wa barabara ni kukuza Uchumi, lakini ujenzi wa barabara kwa Jimbo langu la Mlandizi na hata Waziri nafikiri anafahamu kwamba ujenzi wa barabara ni siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi tulichonacho wanatarajia wasione kuishia kusaini, wanatarajia waone kazi zikiwa zinaendelea. Mheshimiwa Waziri, niendelee kumpongeza kwa sababu kwenye hotuba hii nimeona amezitaja barabara ambazo zinakatiza Mlandizi kwa maana ya Jimbo la Kibaha Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ametaja Barabara ya Makofia - Mlandizi kwamba ipo kwenye hizo hatua, ametaja Barabara ya Chalinze – Utete, ametaja barabara hiyo ya kilometa 23 ya Mlandizi kwenda Ruvu, lakini imetajwa Barabara ya Kisarawe – Mlandizi ambayo ndiyo hii hii ya Kisarawe – Mwanalumango ambayo inapita Mzenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, imetajwa Barabara ya Kibaha – Mlandizi - Chalinze hadi Dodoma ambayo itajengwa kwa *PPP* kwa maana ya barabara ya mwendokasi. Hizi barabara kwa kweli zikifunguka ni uchumi mkubwa sana wa maeneo yetu. Kwa hiyo, naomba sana atakaposimama hapo baadaye, kwa kweli katika lugha yoyote atakayoitumia, ajaribu kuifafanua namna ya watu hawa watakapopata fidia yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia ya barabara zote alizozitaja ndiyo msingi wa kupata nguvu ya kuona barabara zinakwenda kutekelezwa. Kwa hiyo, wangeomba sana atakaposimama atuelezee vizuri namna ya barabara hii mojawapo iliyotiwa saini ya kwenda *SGR,* lakini pia hiyo ya Makofia – Mlandizi namna ya watu ambavyo wamesimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, methali ya pili walioniambia nimwambie Mheshimiwa Waziri kwa lugha hiyo hiyo wameniambia nimwambie, "*ngwengwe mdisolo jaki.*" Yeye ndio yupo Wizarani leo, hizi barabara zilizotajwa anazijua vizuri. Kwa hiyo, muda wa kukaa Wizarani, asiishie kuzitaja. Wanamwomba sana azisimamie ziende kwenye utekelezaji ili baada ya kutekelezwa, basi zifunguke na wananchi waendelee kutumia barabara hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine najua Wizara hii inasimamia kuzifungua hizi barabara zinazokwenda kwenye Stesheni za *SGR* na Serikali imeweka fedha nyingi sana. Kwenye Jimbo la Kibaha Vijijini ipo barabara inaitwa Kongowe – Soga ina urefu wa kilometa 15. Barabara hii kule mbele ina Stesheni ya *SGR* na ina uwekezaji mkubwa sana wa viwanda.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, barabara hii aichukue nayo aiingize kwenye utekelezaji kwa sababu ni barabara inayotekelezwa na inatarajiwa sana na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, naunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maimuna Mtanda, ajiandae Mheshimiwa Flatei.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Pia namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya pamoja na wasaidizi wake wote wakiwemo Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na timu yake yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukienda ukurasa wa 48 wa hotuba kipengele (b) kinazungumzia miradi ambayo ipo wenye upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Katika kipengele hiki, ipo pia Barabara ya Mtama – Mkwiti – Kitangani – Newala ambayo urefu wake ni kilometa 74. Barabara hii ilishatengewa fedha kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 shilingi milioni 145 kwa ajili ya zoezi la upembuzi yakinifu. Nimeangalia kwenye hotuba hapa, barabara hii sasa ipo kwenye upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu fedha imetengwa mwaka 2023/2024 na leo ni 2024/2025 bado ipo kwenye upembuzi

yakinifu na usanifu wa kina. Naomba wakati wa kuhitimisha bajeti Serikali ituambie ni lini usanifu wa kina utakamilika ili barabara hii iende kwenye hatua ya ujenzi kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nimesoma hotuba ya Bajeti ukurasa wa 36. Naishukuru Serikali imezungumzia barabara ya kutoka Kongowe – Kibiti hadi Lindi. Katika kipengele hiki au katika sehemu hii nimeangalia Serikali inasema inatafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa sehemu mbalimbali. Sasa kwenye sehemu mbalimbali hizo, nimeishika ile ya Kongowe mpaka Marendeko kilometa 160 na Nangurukuru – Mbwemkuru kilometa 95. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba Serikali inatambua umuhimu wa hii barabara, lakini pia niishukuru kwa sababu ilikuwa haipitiki katika baadhi ya maeneo. Serikali ilikesha pale kutafuta namna ili wananchi waweze kuvuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuishauri Serikali kwamba ile barabara inapita kando kando ya bahari na ardhi yake ni oevu. Leo tunaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati. Nilikuwa naomba, kwa sababu hii barabara ni mbovu kuendelea kukarabati kila wakati ni sawa na kumpa *panadol* mgonjwa ambaye yupo mahututi, kila siku unampa tu *panadol* unamwongezea shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana, Serikali badala ya kujikita kutafauta fedha kwa ajili ya ukarabati, sasa itafute fedha kwa ajili ya kujenga upya hii barabara ili kuondoa changamoto iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kama unaenda jimboni ukitumia hii barabara, unapofika kule, lazima gari yako baadhi ya vipuli viwe vimeharibika kwa sababu ya ubovu wa barabara uliyopo. Kwa hiyo, naomba na kuishauri Serikali kwamba sasa ifike wakati itafute fedha kwa ajili ya ujenzi na siyo kuendelea kukarabati kila wakati suala ambalo linaiingizia Taifa fedha nyingi zinatumika lakini kila siku tunaenda kukarabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo pia Barabara ya Mtwara – Mnivata - Tandahimba – Newala – Masasi.

Tunaishukuru Serikali kwamba ilitenga fedha, wakandarasi wapo *site*. Tunashukuru kwa hizo jitihada kwa sababu ni barabara ya muda mrefu na imekaa kwenye ilani kwa muda mrefu pia. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali, tunamshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye barabara hii, sitaki kuingilia utaratibu ambao wakandarasi wamejipangia, ila nilitaka kushauri, kwa sababu matengenezo yanaendelea, wametengeneza matuta kwa kiasi kirefu hasa kutoka Mnivata – Tandahimba kwenda Newala, kuna tuta refu sana. Sasa nilitaka kushauri kwamba tumeshuhudia mvua zilizopita hapa katikati barabara hii ilikuwa haipitiki kwa maana ya zile *diversion* ambazo mkandarasi ameziweka, zilikuwa hazipitiki, magari yanakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unatoka Newala zaidi ya kilometa 174. Utoke Newala – Kitangali uzunguke Mtama kwenda Mtwara wakati kutoka Newala mpaka Mtwara ni kilometa 140. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri, mkandarasi ni jukumu lake kuhakikisha *diversion* zake zinapitika muda wote, lakini magari yalikuwa yanakwama, mkandarasi haangalii wala hashughulikii ili wananchi au wale watumiaji wa barabara hii waweze kupita kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri kwamba ahakikishe wakati wote zile *diversion* zake zinapitika ili kuwaondolea adha na gharama kubwa watumiaji wa barabara hii wanaotoka Newala kwenda Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtanda, ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Gregory Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukubali kuweka barabara yetu hii ya Mbulu – Haydom - Labay kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nina ombi kwa Mheshimiwa Ulega. Ipo Barabara ya Maretadu inaitwa Dongobesh – Maretadu kwenda Haydom. Barabara hii inafaa sasa kupandishwa hadhi kutoka kwenye wilaya zetu kuja kwenye *TANROADS* kwa sababu ina sifa zote. Kwa sasa hivi, nimwambie Mheshimiwa Waziri, haipitiki kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hali ni mbaya na siyo mbaya, ni mbaya zaidi lakini pia Bashay - Endamilay – Haydom nayo ni mbaya, mbaya zaidi. Kwa hiyo, ombi langu, najua Waziri ni mchapakazi, ninakufahamu tangu tukiwa vijana. Nakuomba sasa huu ndiyo wakati wake umefika wa barabara hiyo kuipandisha ije *TANROADS* ikafanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo barabara ambayo kimsingi nimekuwa nikiomba mara nyingi hapa, Barabara ya Karatu – Mbulu - Dongobesh – Haydom – Sibiti - *Lalago River*. Barabara hii inategemewa na Waheshimiwa Wabunge 12 wapo hapa ndani na wangetamani barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini namshukuru Mheshimiwa Rais? Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu amekubali kipande cha Haydom kuja Labay kijengwe kwa kiwango cha lami na walau ametoa 10% kwa mkandarasi ambaye anaendelea na taratibu zinaendelea. Sasa kuna barabara hii ya Mbulu – Garbabi kwa kweli mkandarasi hayupo *site*. Mimi ninavyoona ni hatari kwa sababu ameshajenga kiwango fulani kimefikia, bado tu kumwaga lami. *(Makofi)*

Sasa kaka yangu Mheshimiwa Ulega, wewe ni Waziri, umetoka kwenye Wizara ya Mifugo, umefanya vizuri. Nakumbuka tumekuwa kwenye jumuiya ya vijana wote katika mtindo ule wa Chama cha Mapinduzi. Sasa ndugu yangu wewe ukaingia ukawa m*NEC,* ukaja huku Bungeni, na mimi nikawa Bungeni.

Leo ndugu yangu naomba basi hebu njoo kwenye barabara ile ukawe mwarobaini wa ile barabara, kwa sababu kwanza barabara imesimama, mkandarasi hayupo *site* na balaa zaidi unajua tena barabara ikisimama haijawekewa fedha, haipitiki

kabisa. Kwa hiyo, wananchi hawaitegemei barabara ile kuwa nzuri kwa sababu hakuna fedha inayotengwa kila mwaka kwa *maintenance*.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Ulega barabara ile haipitiki kabisa. Kwa hiyo, wananchi wanaona kuliko ile lami iliyoanza kuwekwa ni bora ungeweka changarawe ya kawaida kuliko hiyo lami inayoendelea kwa sababu yaliyofanyika ndani ya Bunge hili sitaki kusema. Nimeizungumzia barabara hii mara 25 kwenye hotuba kama hii, lakini nikuombe sasa wewe na kijana mwenzio Mheshimiwa Godfrey, najua ni Mawaziri ambao kwa kweli mnachapa kazi, Mheshimiwa Rais amewaamini amewaweka hapo; wamebadilishwa wengi kuja hapo.

Mimi ninajua kwa Mdengereko hakuna kinashoshindwa. Sasa ndugu yangu nikuombe nenda kaweke fedha pale ili mkandarasi awepo *site* wamalizie kujenga ile barabara. Kilometa 25 zinakushindaje ndugu yangu? Mimi ninaamini haziwezi kukushinda, nenda pale fanya hivyo. Ile Haydom kwa sababu mkandarasi ameshalipwa 10%, kwa mujibu wa sheria zetu hana haja ya kuacha kujenga barabara. Endelea, watumie ma-*engineer* wako wamsimamie mkandarasi aendelee kufanya kazi. Kwa sababu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mbulu Vijijini tuna imani na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu barabara ile tangu Mbulu imeundwa au imeanzishwa mwaka 1905 haijawahi kuwa na barabara. Tumemwambia Mama yetu ni msikivu, amekubali kuiweka na imeanza kazi, kilichobaki ni Mheshimiwa Waziri kuisimamia na ndio ana *instrument* ya kusimamia barabara hii. Wasimamie barabara hii ili ijengwe kwa kiwango cha lami na iweze kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini ya kwamba kwa kuwa Mheshimiwa Rais alishakuja, na kwa kuwa aliahidi barabara hii, asije akaonekana mwongo wakati ninyi mpo, kwa sababu imeshaanza, ni kiasi cha kusimamia tu barabara hii. Ombi langu ni kwamba wasimamie barabara hii ili ikamalizike kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu gani nasema hivyo? Ukiangalia kwenye hii bajeti, mimi nafurahi Mheshimiwa Ulega nimeona ameniweka kwenye bajeti yake, ameitengea fedha iendelee kujengwa, lakini kwa sasa kwa sababu hali yake ni mbaya, maana yake angeendelea kuijenga, ingeshamalizika kabisa. Yapo matatu pale ninaomba ayamalize, kwa sababu mkataba wa yule mkandarasi umekwisha, basi uhuishwe ule mkataba ili mambo haya yaendelee na mkandarasi awepo *site* aendelee kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nakuomba kwa sababu Waziri ni kijana mwenzangu, ndani ya mwezi huu atembelee ile barabara akawape matumaini wananchi wa Mbulu kwamba barabara inajengwa au iweje, naye akaone adha wanayoipata wananchi wa Mbulu Vijijini na hasa Mbulu Mjini na Karatu pia wananchi wa Singida na Meatu, awape matumaini, kwa sababu ukishaanza kuepeleka yale *material site*, juzi nimeona wamepeleka kule magreda yameanza kufanya kazi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Sasa wananchi wasije wakaona ndiyo kampeni, kumbe kazi inaanza. Mheshimiwa Waziri njoo uwathibitishie kabisa kwa sababu muda umefika wa barabara hiyo kujengwa.

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Massay. Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea tumepata wageni Bungeni naomba niwatambue.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso ambao ni wananchi kutoka Karatu Mkoa wa Arusha. Kama wapo wasimame,

tunawakaribisha sana, ahsanteni sana karibuni wananchi wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye mgeni wa Mheshimiwa Keneth Ernest Nollo, Mbunge ambaye ni Ndugu Choile Chigarika, mpiga kura wake kutoka Bahi Mkoani Dodoma, kama yupo tafadhali, karibu sana mgeni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, tunaye mchangiaji anayefuata Mheshimiwa Francis Mtinga, ajiandae Mheshimiwa Edward Olelekaita na mchangiaji wetu wa mwisho leo atakuwa Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 116 *paragraph* 321kwenye bajeti yako Mheshimiwa Waziri, umeongelea baadhi ya barabara za Singida, lakini sijui ni kwa bahati mbaya au ni kwa vyovyote, sijaona barabara ya kutoka Iguguno kupita Makao Makuu ya Wilaya pale Mkalama kwenda Sibiti na hatimaye kuunganisha Mkoa wa Singida na Mkoa wa Simiyu. Barabara ambayo kwa kipindi changu chote cha miaka minne Bungeni nimekuwa nikiisemea kwenye maswali na kwenye mchango, lakini mpaka sasa hatuna barabara ya lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu sana, barabara hii ni ya kiinchi. Barabara za Mkoa wa Singida ni barabara za nchi kwa sababu zinagawa nchi katika pande zote nne. Ukitoka mashariki mwa nchi, Dar es Salaam kwenda Mwanza Magharibi mwa nchi, ni lazima upite Mkoa wa Singida, ukitoka Kaskazini mwa nchi kwenda Kusini ni lazima upite Mkoa wa Sigida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii barabara ya Iguguno, kupita Mkalama kwenda Sibiti mpaka Mkoa wa Simiyu inaunganisha Mikoa ya Mara, Simiyu na sehemu ya Mkoa wa Mwanza. Nashauri kwamba hata Wabunge wote wa mikoa hii kwa pamoja kabisa tungeungana kusema kwamba bajeti hii haipiti bila kuweka fedha kwenye hii barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka wenzetu wa Dodoma na Manyara mpaka Arusha, mimi nikiwa bado mdogo, nasikia wale akina Mheshimiwa Kwang'u waliungana wakasema bajeti haipiti; ndiyo hii barabara leo ina lami. Mimi nadhani kuna kila haja, Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Simiyu, Mkoa wa Mara hebu tuungane kwa pamoja kwamba bajeti hii isipite bila barabara hii kuwekewa fedha, kwa sababu ni barabara muhimu inaunganisha Mkoa, ina uchumi, pamba inapita. Watu wa Simiyu leo mkiwa mnaenda Simiyu mnapita Mwanza, mkipita hapo Singida mnaenda karibu kilometa 200 tu, sasa sijui hii barabara itajengwa lini, na upembuzi yakinifu tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kilometa kumi ziko pale nimepewa pale Makao Makuu kwenye hii barabara pamoja na taa zake kwa bajeti inayoisha, lakini hata mkandarasi bado hajafika pale. Hili jambo jamani, Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu, Mwenyekiti mwenzangu wa Umoja wa Vijana Mkoa wa Pwani mimi nikiwa Mwenyekiti wa Vijana Mkoa wa Singida, Mjumbe wangu wa Baraza, tafadhali bwana, mimi Ubunge bado naupenda kaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkalama wameniambia wanahitaji tu barabara, basi nikae vipindi vingine vitatu. Kwa hiyo, nakuomba sana, hii barabara ni mfupa, hebu wewe utafune huu mfupa. Kama wenzako waliopita wameushindwa, hebu wewe utafune, maana upembuzi tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni ya muhimu sana, Iguguno, Mkalama, Simiyu kupita daraja la Sibiti ambalo limejengwa kwa mabilioni ya fedha ili tu barabara za lami ziweze kupitika na kuchukua uchumi wa upande ule kuleta huku Dar es Salaam na sehemu nyingine. Tafadhali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitika sana, baada ya kuiangalia kwenye kitabu sijaona sehemu ambako barabara hii imetajwa kwa umuhimu kabisa, sijaona hata zile kilometa kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, angalieni hii barabara, mnapita wote mkienda kwenye Kamati, wote lazima mpite kwenye barabara hii ya

vumbi. Kwa hiyo, kila mmoja ajue hii ni barabara ya nchi. Ukitoka Dar es Salaam unaenda Simiyu, unatembea kwa lami, ukifika pale unaingia kwenye vumbi, kuna maana gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani unaweza kuvaa suti halafu chini ukavaa suruali ya *jeans*, haijaungana! Unatoka Mwanza unapita kwenye vumbi, halafu baadaye unaanza lami tena. Hebu kwa pamoja kabisa tuone kwamba hii barabara ni ya kitaifa, na siyo barabara ya Mkoa wa Singida kabisa. Hii barabara ni ya kitaifa kwa sababu huwezi kwenda upande wowote wa nchi bila kupita Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, Rais wetu ametutendea mambo mengi makubwa, na hii barabara ameshaipitisha, amenipa kilometa kumi, kilichobaki ni utekelezaji tu ambao unatakiwa uanze kwenye bajeti inayoisha na hii inayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi angalau hizi kilometa kumi ambazo nimepewa, waongezee na hii bajeti hata kilometa nyingine 30 angalau basi kilometa 42 kutoka Makao Makuu ya Mkoa mpaka pale Makao Makuu ya Wilaya angalau na sisi tuione lami. Katika Jimbo la Mkalama, kilometa mbili tu, ile sehemu inayopita Iguguno ndiyo kuna lami tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhalini sana, sijui nifanyeje nipige magoti tena hapa, labda mbele ya hili Bunge ili niweze kusikilizwa. Mimi bado kijana sana, bado nautamani Ubunge, nimekaa miaka mitano, bado wananchi wangu wananihitaji.

Mheshimiwa Waziri, hii barabara nakuomba, niko chini ya miguu yako, natamani kulia kabisa machozi, na haya ni machozi ya wananchi wa Mkalama kwa miaka mitano mfululizo tunaomba hii barabara. Zaidi ya miaka kumi, alianza Mheshimiwa Msindai, ameomba ikashindikana; akaja Marehemu Mheshimiwa Mwambu ameomba, amekuja Mheshimiwa Allan; na mimi sasa, angalau nimepewa mengi, basi hili la barabara limaliziwe ili angalau niwe na uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. Tafadhali sana, namwomba Mheshimiwa Waziri, barabara hii ni ya muhimu sana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, naamini Mheshimiwa Waziri amekusikia. Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau atafuatiwa na Mheshimiwa Benaya Kapinga.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Kwa sababu ya muda, Mheshimiwa Waziri na timu yenu, wote hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nazungumzia barabara mbili; barabara ya Handeni – Kiberashi – Kijungu - Kibaya – Njoro - Chemba mpaka Singida, na barabara hii ina sifa nyingi sana. Kwanza barabara ilikuwa kwenye mradi wa *EPC+F* na tumesaini mikataba tangu miaka miwili iliyopita, lakini nakushukuru kwa sababu bajeti yao hapa ukurasa wa 19 wamesema, hizi barabara zote za *EPC* mpango wa kujenga uko pale pale na wameshabadilisha mikataba. Ushauri wa kisheria tu ni kwamba unaposaini mikataba ni lazima barabara hizi zijengwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu kwa sababu kwanza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia ametoa agizo hapa wakati wa ziara ya Tanga na kwenye bajeti yenu hapa wamesema tayari *TANROADS* na *TPA* wameanza majadiliano kuhusu namna bora ya utekelezaji wa agizo hili la Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo la Rais lazima liwe na *timeframe*. Kwa hiyo, tunategemea baadaye Mheshimiwa Waziri anapokuja kwenye mjadala atuambie sasa hao *TPA* na *TANROADS* wanafanya majadiliano kwa muda gani? Kwa sababu wananchi wanataka kusikia barabara hii inajengwa. Barabara hii ni muhimu sana, kwani Mradi wa Bomba la mafuta unapita kwenye barabara hii, Bandari ya Tanga imejengwa, magari zaidi ya 533,995 yanapita kwenye barabara hii kwa mwaka. Barabara hii itawapunguzia watu wa Tanga kuja Dodoma kwa zaidi ya kilometa 110. Kwa hiyo, ni barabara muhimu sana, lakini barabara hii ni ya wakulima, wafugaji na wananchi wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni barabara inayounganisha mikoa minne, Tanga, Dodoma, Manyara na Singida. Barabara hii itapita pia Manyara ambayo iko kwenye mikoa ambayo ina kiwango kidogo cha lami zaidi ya kilometa 200 hivi. Kwa hiyo, ni barabara muhimu sana. Kwa hiyo, rafiki yangu Mheshimiwa Ulega akija atuambie hayo majadiliano yanachukua muda gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunashukuru kwa sababu kwenye ukurasa wa 119 wamesema watajenga kilometa 50 kutoka Kibaya kwenda Kisima, na kwa kweli hii itatusaidia sana, lakini ushauri wetu tu wa kisheria ni kwamba, kama majadiliano yanaendelea kati ya *TPA* na *TANROADS* kuhusu barabara na agizo la Mheshimiwa Rais kujengwa barabara hii yote mpaka Singida, basi wafanye haraka ili tu-*negotiate* hizi kilometa 50 tuzihamishe kutoka Kibaya zije Kongwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba waanze kujenga barabara hii ya Kongwa kutoka Kibaya kilometa 50. Mheshimiwa Spika Mstaafu, naye atapata kilometa kumi pale. Unajua, mpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tutahamisha tu, kama barabara hii watasaini na wataji-*commit* kwamba hii barabara itajengwa na ushauri mwingine, kwa kuwa hii barabara ni ndefu sana, kwenye *negotiation,* wahakikishe inajengwa kilometa mia mia na wahakikishe wanakuwepo wakandarasi wengi kwa sababu mradi wa kwanza sijui kutoka Tanga hadi ifike Singida itachukua muda mrefu sana. Huu ni ushauri mwingine wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Kongwa – Kiteto - Simanjiro, tumeona wanajenga kilometa 70 hapa, tunashukuru sana, lakini tunataka tusikie kauli hii vizuri kwa sababu tulikuwa tunaambiwa ikitoka Arusha ikifika Losinyai sijui inarudi tena Arusha. Tunataka hizi kilometa 70 zianze kujengwa ili tujue kwamba hii barabara ambayo ni nzuri sana inajengwa. Inapitisha magari 583,270 zinapita kwenye barabara hii kwa mwaka. Ni barabara ambayo inaunganisha mikoa mitatu; ni barabara muhimu sana, na kwa sababu zilikuwa kwenye mkataba wa *EPC+F,* wamesema hapa kwamba wameshahuisha mikataba na kwamba barabara hizi zitajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi barabara zitawanufaisha sana wananchi wa Kiteto, na unajua Kiteto ni *breadbasket*. Hii barabara itasaidia sana kufungua uchumi wa Manyara na wananchi wa Kiteto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri aliniahidi taa 50 za barabarani, hizo tunataka tupate majibu leo. Tunataka ule mji wetu wa Kibaya upendeze. Tunashukuru kwenye ukurasa wa 263 tumeona ametutengea shilingi milioni 300 kwenye ile barabara ya Kibaya - Chemichemi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Edward.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, kuna barabara mbili tunataka tuzipandishe ziende *TANROADS,* barabara ya Dosidosi - Dongo kilometa 56 na barabara ya Kiperesa kilometa 45, hiyo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Edward. Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza naunga mkono hoja; pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wote katika Wizara hii. Kipekee hapa nampongeza *Engineer* wa Mkoa wetu, Eng. Salehe, anafanya kazi nzuri, ana-*respond* kwa haraka sana kwenye matukio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru sana Serikali kwa mradi wa barabara ya Kitai - Rwanda kilometa 35. Mradi huu ulikuwa ukamilike mwezi Disemba, 2023 lakini mpaka hivi leo mradi huu bado uko nyuma sana. Sasa leo nataka nipate majibu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu sana, yanapita magari makubwa yanayosafirisha makaa ya mawe. Makaa ya mawe yote yanayouzwa nchi hii, kwa kiasi kikubwa yanatokea katika njia hii, na imekuwa kero kubwa kwa wananchi wanaokaa sambamba na barabara hii, kuanzia Ruanda, Paradiso, Amani Makoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili lote wakati wa kiangazi linakuwa na vumbi jingi sana. Sasa hivi wakati wa masika hii kwa sababu magari yanayobeba makaa ya mawe ni mazito mazito, ile barabara sasa hivi haipitiki, na ikipitika basi wananchi wale kipande kidogo cha kilometa 20 wanatumia masaa mpaka sita. Kwa kweli haileti afya kwa eneo linalotoa rasilimali kubwa kama hizi halafu hatuoni umuhimu na hatutoi kipaumbele kutengeneza hizi barabara.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mtani wangu naomba utakapokuja kutoa hitimisho hapa, utueleze wananchi wa Mbinga ile barabara ambayo ilipaswa kwisha mwaka 2023 itaisha lini? Pengine usiposema vizuri, leo kwa mara ya kwanza nami nitashika Shilingi kwa sababu sioni sababu kwa nini barabara inayopitisha rasilimali nyingi isijengwe mpaka leo na kukamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande cha pili kuanzia Rwanda hadi Lituhi tunashukuru mkandarasi tayari wameshampata, bado hajapewa fedha za awali kuanza kazi. Sasa na yeye lini anapewa fedha kuanza kazi? Kwa sababu ile barabara inatoka pale Ruanda mpaka Lituhi, na Ndumbi, tumejenga bandari nzuri ya kisasa, lakini ile bandari haitumiki kwa sababu mzigo hauwezi kupita kutoka hapa Ruanda kwenda hadi pale Ndumbi. Kwa hiyo, huyu mkandarasi tuliyempata, ni lini anapewa fedha na anaanza kujenga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, namshukuru sana, barabara ya Kigonsera, Matiri mpaka Mbaha. Barabara hii Mheshimiwa Rais alipita akatoa ahadi ya kutujengea kwa kiwango cha lami, sasa hivi tayari nimeona upembuzi yakinifu umeanza, sasa ni lini unakamilika na lini barabara ile inaenda kujengwa? Kwa sababu Mbaha tuna jambo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa barabara hii umeongezeka sana kwa sababu inatoka Kigonsera inaenda Matiri halafu inafika Mbaha na barabara yenyewe siyo ndefu, ni kilometa 55 tu. Kwa nini tusiijenge, kwa sababu tuna jambo letu pale Mbaha? Naomba sana, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kusimama hapa, atueleze sisi Wanambinga na wananchi wa Mbaha Jimbo la Nyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine ni barabara ya kutoka Mbinga kwenda Litembo kupitia Kindimba, lakini na ile ya Ndengu kuelekea Litembo na yenyewe inafika hadi Nyasa. Barabara hizi ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kujengwa kwa kiwango cha lami. Nashukuru sana upembuzi yakinifu wa barabara hii umefanyika. Sasa lini tunapeleka fedha na kuzijenga hizi barabara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kadhaa nimesema hapa, pale Litembo kuna hospitali teule, wananchi wa Mbinga pale ndipo tunapotibiwa toka enzi na enzi, lakini tunafika kwa shida sana. Kwa hiyo, tunaomba, Mheshimiwa Rais aliona haja ya kupeleka lami pale. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, mtani wangu atekeleze hilo kwa kupeleka hiyo lami, kwani tayari upembuzi yakinifu umefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine ni ya kutoka Nyoni kuelekea Maguu hadi Kipapa na yenyewe inafika hadi Ziwa Nyasa. Barabara hii iko kwenye Ilani ya Chama hiki ambayo sasa tunaenda kuikamilisha. Tayari upembuzi yakinifu umekamilika. Nashukuru inajengwa kipande kipande, sasa ni lini tutaijenga yote kuanzia mwanzo hadi mwisho ili wananchi wa Bonde la Gati wapite na wanufaike na maendeleo ya Chama hiki cha Mapinduzi?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa mara nyingine naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Benaya. Mheshimiwa Florent Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia Wizara ya Ujenzi. Nami niungane na wachangiaji waliotangulia kupongeza sana juhudi za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa nia njema ya kuhakikisha kwamba Wizara hii inatengewa bajeti ya kutosha kuhakikisha kwamba inaboresha miundombinu ndani ya Majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia njema ya Mheshimiwa Rais tunaiona kupitia bajeti ya Wizara ya Ujenzi ambapo mwaka 2024/2025 Wizara hii kwa upande wa maendeleo ilitengewa shilingi trilioni 1.6, lakini leo tunaona ongezeko la 30% ambayo imetengewa shilingi trilioni 2.189, ni pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, napongeza Wizara hii chini ya *Comrade* Abdallah Ulega, ambaye kwa kweli kwa *speed* ambayo ameenda nayo, tunaona ni *speed and standard* katika kusimamia barabara hizi ambazo katika kipindi chake ameingia kipindi cha changamoto, lakini aliweza kukabiliana nazo na kuhakikisha kwamba hali halisi ya miundombinu ndani ya Wizara yake inarudi katika mfumo wa kawaida, akisaidiwa na Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya ambaye pia amekuwa Mtendaji mzuri ndani ya Wizara hiyo bila kusahau Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa *TANROADS*, pamoja na Mameneja wetu wa Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza *Engineer* wangu wa Mkoa Eng. Ntuli pamoja na wasaidizi wake ambaye amefanya kazi nzuri ndani ya Mkoa wetu na Wilaya ya Misenyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hasa kwa upande wa Misenyi, na kwa niaba ya wananchi wa Misenyi kutoa pongezi kwa kazi kubwa ambayo kupitia Wizara hii *TANROADS* imefanya kazi kubwa na kazi za barabara zote ndani ya Wilaya yetu ambazo ziko katika hatua za ujenzi. Nyingine zimekamilika, lakini na nyingine ziko katika hatua mbalimbali, nami kwa niaba ya wananchi hao nashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimerejea katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri, ukiangalia ukurasa wa 292 kuna upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara ambayo nimekuwa nikiililia sana hapa Bungeni, barabara ya Katoma – Kanyigo – Bukwali kilometa 38.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara kwa kweli Serikali imekuwa ikitusaidia, tunajenga mita 400, mita 100, lakini imeweka katika utaratibu wa upembuzi ili sasa ikikamilika naamini Mheshimiwa Waziri hataniacha ili kuweza kuijenga kwa pamoja ili wananchi hao angalau waweze kufaidi lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Serikali imeweza kututengea bajeti ya shilingi milioni 100 katika eneo hilo na imenipa mita 400 za lami ziendelee kujengwa. Naishukuru sana Serikali kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa niaba ya wananchi wa Mutukula, tunayo barabara ya Mutukula – Kakunyu. Hii ni barabara ya usalama kilometa 46 ambayo inaimarisha usalama katika eneo letu, tukijua kwamba tumepakana na nchi ya Uganda, na yenyewe ipo katika upembuzi na usanifu. Mheshimiwa Ulega naomba na hii barabara ni ya muhimu sana kwa Wilaya ya Missenyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kushukuru wananchi wa Missenyi kwa barabara ya Bunazi *Junction - Kagera Sugar* kilometa 25. Hii barabara tangu mwaka 2023 tulikuwa kwenye kuomba, mkandarasi alisaini, lakini mwaka huu Serikali imetupatia fedha shilingi milioni 300 tumelipa fidia, imetupatia fedha shilingi bilioni 5.4 mkandarasi ameshapewa *advance* ana-*mobilize* vifaa vyake kuanza kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru zaidi Serikali kwamba katika bajeti yake imeweka tena shilingi bilioni mbili katika barabara hii. Kwa hiyo, mkandarasi wetu anafanya kazi akiwa na uhakika kwamba akiomba *certificate* inayofuata atalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara ya Ujenzi kwa barabara ya Minziro - Mutukura ambayo imeendelea

kufunguliwa. Imeshafungua takribani kilometa nane na hapa imenitengea tena kilometa nne, shilingi milioni 100. Hii ni barabara ya kimkakati, na ninashukuru sana kufungua mazingira ya kiuchumi kwa wananchi wetu wa Mutukula na Minziro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa kuboresha maeneo ya Makao Makuu ya Wilaya yetu hasa Bunazi, kuna takribani mita 400 kiwango cha lami ambacho imenitengea zaidi ya shilingi milioni 105 na kuboresha barabara ya Nyabiyanga kwenda Kasambya, wananchi hao waweze kuwa katika barabara zenye ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo haya, tuendelee kushukuru barabara yetu ya Kyaka – Katoro - Ibwela mpaka Ketema na yenyewe imeanza na kilometa kumi, lakini basi niombe *speed* iongezeke ili na upande wangu wa Missenyi, upande wa Kyaka - Katoro uweze kufikiwa na tuweze kutengeneza barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naendelea kushukuru kwa ajili ya barabara ya Minziro – Kasambya, ilikuwa na changamoto, Mheshimiwa Naibu Waziri alifika kwa sababu sasa hivi imenyanyuliwa kwa kiwango kizuri kama tuta, wananchi hao kero ya maji yaliyokuwa yanajaa barabarani na wananchi wetu waliokuwa wanaenda kuhiji kule Minziro, wanaenda kwa usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, tuliomba taa za barabarani Kyaka, zimefungwa, lakini ni chache, Bunazi na Mutukura bado. Naomba sasa tumalizie kipande hicho ili wananchi hao waweze kufaidi taa za Mheshimiwa Dkt. Samia. Pia, naomba barabara ya Mshenye ambayo inaenda Mshenye - Bugandika – Kitobo - Buyango hadi Ruzinga na yenyewe iingie kwenye usanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati namalizia, namshukuru Mheshimiwa Waziri, sasa namkaribisha angalau afanye ziara Wilayani Missenyi ili tuweze kukagua hizo barabara na kuweza kuhakikisha kwamba zinajengwa katika kipindi kinachokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kyombo.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na uchangiaji mchana na hoja itahitimishwa kama ilivyopangwa kwa ratiba ambayo tunayo Mezani.

Waheshimiwa Wabunge, pia nimepokea maombi mbalimbali, naomba mtambue kwamba maombi yamefika kutegemea na atakayeongoza kikao mchana, nimeacha Mezani kwa ajili ya maamuzi ya Meza kwa kadri hali itakavyoruhusu. Kwa hiyo, maombi yenu yote yapo hapa Mezani hayajapuuzwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mchana kwa utaratibu uliopo na kama hautabadilika tutaanza na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, atafuatia Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mheshimiwa Innocent Kalogeris, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Mabula, Mheshimiwa Stella Fiayo, Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mheshimiwa Kingu Elibariki na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hili nasitisha Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.02 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, atafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa na Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, ajiandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi. Nami namshukuru Mungu kwa kunipa pumzi jioni hii niweze kuchangia Bajeti ya Wizara hii adhimu, Wizara ambayo ndiyo mishipa ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa dhamira yake njema ya kuifungua nchi na kuunganisha mkoa na mkoa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napongeza pia juhudi za Wizara hii katika kuhakikisha miundombinu hii ambayo ndiyo matarajio yetu, inakuwa imara kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, zipo changamoto, lakini nampongeza Mheshimiwa Waziri, kijana wangu huyu, Mheshimiwa Ulega, Baba Tulia, kwa weledi wake. Amepokea kijiti hiki katika kipindi ambacho tunaamini ataisaidia nchi hii.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake, Ukurasa wa Sita, ameonesha, ameanzia ukurasa wa tano, namna ya kuunganisha makao makuu ya mikoa na mikoa. *Paragraph* ya 16, ukurasa wa sita, Sehemu ya Nne, ameonesha pia Barabara ya Singida – Mbeya, sehemu ya Mlongoji – Itigi – Mkiwa, eneo ambalo ndiyo mimi naliwakilisha katika Bunge lako hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yuko mkandarasi pale anaitwa *CHICO,* ni mkandarasi mahiri sana kwa kazi zake. Tumeona jinsi

anavyojenga barabara maeneo mengine, na kwa hakika kazi yake ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, ziko changamoto. Naomba Serikali kwa ujumla, Wizara hii ya Ujenzi na Wizara ya Fedha, Mkandarasi huyu ame-*raise certificate* nyingi, anadai fedha nyingi, anadai zaidi ya shilingi bilioni tisa na *point*. Sasa amesimamisha kazi huu ni zaidi ya mwezi wa 11 toka kazi imesimama.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa eneo lile matarajio yao yalikuwa ni kwamba barabara hii ikifunguka na wenyewe watanufaika na Uchumi, na watakimbizana katika kutafuta riziki zao kwa namna ambayo ni halali. Barabara hii inaunganisha Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mbeya unapakana na Zambia kwa maana mtu akitoka nchi Jirani, anavuka Tanzania kwenda nchi nyingine, hawezi kupita hapa Dodoma. Akitokea Mbeya akaja kwangu Itigi atapita Singida.

Mheshimiwa Spika, aidha, anakwenda kupitia kule Daraja la Sibiti kwenda Mara ambako atapakana na Nchi ya Kenya au atapita kwenda Babati – Arusha – Namanga au atapita Babati – Arusha – Moshi – Holili. Akipita njia hii atapunguza kipande kirefu cha barabara ukilinganisha na kama anatokea njia hiyo apite, kwa mfano, mpaka ule wa Namanga. Akitokea Namanga kuja Arusha - Babati, aje Dodoma, aje afike Mbeya, ndiyo aende Tunduma, atakuwa amezidisha zaidi ya kilomita 150.

Mheshimiwa Spika, tunataka tuisaidie nchi hii na Bunge lako Tukufu, na Mheshimiwa Rais wetu, dhamira yake hii njema. Tunaomba sana Mawaziri wa Wizara hii na Waziri wa Fedha asaidie kuwalipa hawa wakandarasi ambao wako nchi nzima. Kila Mbunge anayechangia hapa kuna sehemu ime-*stuck*.

Mheshimiwa Spika, tunajua kweli tulikuwa na malengo mazuri. Baadhi ya maeneo tulitakiwa tuyamalizie, lakini tulipomaliza, basi tuangalie namna ya kukwamua hii miradi ambayo imekwama, miradi muhimu sana. Zile kilometa 25 Mheshimiwa Ulega akimlipa huyu mkandarasi, akirudi *site,* muda

mfupi sana atakuwa ameshamaliza ataendelea na zile kilometa nyingine 31 tulizomwongezea juzi, *point* sita ambazo Mheshimiwa Rais alikuja pale na akaona namna ambayo wananchi wa Itigi na Mkoa wa Singida walivyo na dhamira nzuri ya kuunganishwa na wenzao.

Mheshimiwa Spika, barabara hii pia ina changamoto ya upitaji, yaani imeharibika mno baada ya mkandarasi kusimama. Zile *diversions* ambazo alitengeneza, hazirekebishiki na watu wanapita kwa tabu sana, lakini vipande ambavyo havina mkandarasi pia, Meneja wa Mkoa kila ukimwuliza inaonesha naye ana tatizo hili hili la kwamba, hana fedha ya kufanya matengenezo ya dharura.

Mheshimiwa Spika, kipande cha kutoka Lulanga kwenda Itagata kuna sehemu ambayo mvua ikinyesha, kama haya manyunyu yaliyonyesha jana Dodoma hapa, basi tena hatuwezi kupita. Naiomba Serikali isaidie. Kuna maeneo mengi barabara hii ambayo ni mazuri, kwa mfano, ukitoka Kintanula kwenda Mwamagembe ni pazuri, lakini kutoka Rungwa kuja Kintanula pana changamoto. Tunaomba sana Serikali itusaidie kumrudisha mkandarasi barabarani.

Mheshimiwa Spika, vilevile yuko mkandarasi anasimamiwa na Wizara hii ya *TANROADS* pale Itigi, kilometa 10. Naye tunaomba aongezewe fedha kidogo anazodai ili amalizie, na kuna taa zetu za barabarani.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja, lakini tusaidie Mkandarasi yule arudi wa *Tronic* pale Itigi na *CHICO*...

**SPIKA:** Umeshasikika Mheshimiwa.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE: ...**tutafaidika sana watu wa Itigi na tutafurahi tunapoelekea katika uchaguzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii tena ya kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa nafasi aliyonipatia kusimama tena mbele ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa bajeti ambayo nilikuwa naangalia tu zile za maendeleo. Ukifungua ukurasa Namba 16, utagundua kwamba, Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilikuwa karibu shilingi trilioni 1.7 hivi, lakini mwaka 2025/2026 Bajeti ya Maendeleo imeshakwenda kuwa takribani shilingi trilioni 2.1. Ukiangalia ongezeko lake, ni karibu 22.94%. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo sasa inaonekana kuna ongezeko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nawapongeza sana wataalam kwa sababu, wao ndio wachakataji wa shughuli hii; Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wataalam wengine kwa namna ambavyo wamefanya kazi kubwa katika bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda ukurasa wa tano, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, kuna miradi hapo inaoneshwa, ambayo inatuunganisha sisi kama nchi na nchi nyingine, maana yake ni miradi ya Kimataifa. Utaona kabisa kuna miradi, kama Mradi wa Tanzania na Malawi kupitia Barabara ya Mpemba – Isongole, kilomita 50.3. Kwa hiyo, ina maana kazi hii inayofanyika na *TANROADS* tayari imeshatuhusianisha sisi na Mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia tena ukurasa huo huo utaona kuna Tanzania na *DRC* kupitia Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga *Port,* kilomita 107. Hii ni kazi kubwa ambayo inaonesha

wazi kwamba siyo diplomasia tu, namna tunavyoweza kuwasiliana na wenzetu katika kufanya shughuli hizi. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam kwa kazi kubwa ambayo wamekuja nayo hapa.

Mheshimiwa Spika, vilevile iko miradi mingi katika ukurasa huo ya Kitaifa, ambayo inaonekana kwamba, kuna kuunganika mkoa na mkoa. Kuna mahali imeunganishwa wilaya na wilaya, kuna kazi kubwa inafanyika. Changamoto kubwa tu ambayo nimeiona, pamoja na ongezeko hili, inaonekana mpaka Aprili, 2025, Bajeti ya Maendeleo ambayo ilipangwa kutolewa na Serikali imeshatolewa kwa asilimia kama 90.9, lakini utaona kuna miradi mingine bado haiendi kwa kasi sana.

Mheshimiwa Spika, maana yake, kuna dharura nyingi katikati humu na bajeti yetu haiingii kule inakotakiwa kuingia. Kwa hiyo, naomba sana, dharura hizi sijajua tutazifanyaje, lakini inaonekana zinaingia mahali na watu wetu inawezekana wanachelewa au hawalipwi kama ilivyokuwa imekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jimboni Busanda, hii ya Kitaifa ambayo iko huku ndani, asubuhi nilikuwa nauliza Swali Na. 232, niliuliza kabisa barabara yetu kutoka pale Geita kwenda Iloge kupitia Bukole na Nyarugusu, lakini nimeona hapa Ukurasa Namba 28 imeshaoneshwa pale, imeandikwa wazi kwamba ni mpango wa Serikali hii barabara iwe imesainiwa mwisho wa mwezi Mei.

Mheshimiwa Spika, mwezi Mei ndiyo huu, Nawaomba sana Wizara kwa sababu, maandishi yale najua hatutayabadilisha. Mwisho wa mwezi Mei huu tukaone kinachofanyika, kusaini ili barabara hii iweze kutengenezwa kwa sababu, inapita kwenye miradi mingi ya migodi ambayo italeta faida ndani ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile asubuhi hiyo tu nilisema, barabara yetu ya kutoka Ushirombo *T3* kuja Katoro kwenye Barabara ya *T4* kuna changamoto hapa, kipande kile cha kutoka Nyikonga kuja Katoro kinaonekana maelezo yake ya fedha hayakunyooka sana. Hivyo, ukimwuliza mtu kwamba, ni kiasi gani cha fedha hapa? Kitatoka wapi? Atakueleza tu fedha itakapopatikana, lakini

Barabara imeshaingia kwenye bajeti. Niombe sana, hii iwe *defined,* ili kusudi Barabara hii ipate nafasi ya kwenda kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, tumesema wazi kwenye kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ibara Namba 55 (C - G) inaongelea habari ya madaraja. Haya madaraja tayari sisi tunayo Kanda ya Ziwa, Daraja la Kigongo - Busisi. Jana nimesikia linaombewa libadilishiwe jina, lakini Kigongo - Busisi liko zaidi ya 99%.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme wazi kwamba, kuna kazi kubwa imefanyika ambayo inaonekana na ninaamini yako madaraja mengine inawezekana nisiyataje hapa, lakini kuna kazi kubwa imefanyika kwenye Awamu ya Sita kuhakikisha kwamba, wananchi wetu wanapata maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninaamini, kama bajeti hii tuliyoomba sasa tutaisimamia vizuri, tukahakikisha kwamba kila mmoja anakaa mahali pake na kufanya kazi yake vizuri, utekelezaji wa bajeti hii utakuwa mzuri na nchi yetu itaendelea kupitika.

Mheshimiwa Spika, wote tunajua mvua inayoendelea kunyesha nchini kwetu hapa, kwa hiyo, barabara nyingi sana zimeharibika. Niwaombe sana ndugu zangu wa Wizarani, ndugu zangu wa *TANROADS,* akiwemo Meneja wangu Mhandisi Ezra Magogo kuhakikisha kwamba kazi hii, mvua inyeshe, lakini wananchi wetu wanafanya shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, ajiandae.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu ya Wizara ya Ujenzi. Nitumie nafasi hii, nami, kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia, lakini kubwa zaidi kukupongeza kwa kazi kubwa ambayo umeifanya katika

kuendesha Bunge katika kipindi hiki cha uhai wake ambapo tunaelekea mwisho kufikia tarehe 27.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya kuboresha miundombinu katika nchi hii. Vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, mdogo wangu Ulega, pamoja na Mheshimiwa *Eng.* Kasekenya, Naibu wake, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa taasisi ambazo chini ya Wizara, *TANROADS, TBA, TAMESA*, Bodi ya Mfuko wa Barabara na nyingine zote kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kusimamia miundombinu katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi zangu za dhati zimwendee Mheshimiwa Rais kwa utayari wa yeye kuona kwamba, Barabara ya Bigwa – Kisaki inajengwa kwa kiwango cha lami, Barabara ya Ubena – Zomozi – Ngerengere tayari nayo inajengwa kwa kiwango cha lami pamoja na kufanya upembuzi yakinifu kutoka Ngerengere kwenda Mvuha – Kisaki hadi Matemele *Junction* kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere na vilevile kwenye Hifadhi kubwa ya Mwalimu Nyerere. Tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais katika hilo, mimi na mdogo wangu Mheshimiwa Tale.

Mheshimiwa Spika, wamepita Wabunge wengi na kati ya Wabunge waliopita alikuwepo mpaka Naibu Waziri wa Ujenzi, kaka yangu Mheshimiwa Hamza Mwenegoha. Barabara ilikuwa haijajengwa, lakini kwa kitendo cha tarehe 7/2/2024 Mkandarasi wa *Chinese Railways* ameweza kusaini mkataba wa shilingi bilioni 132.4 kujenga kwa kiwango cha lami kutoka Morogoro kwenda mpaka Mvuha, kilomita 78. Tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais na kujipongeza sisi wenyewe Wabunge kwa kazi kubwa ambayo tumeifanya na hatimaye mkataba ukasainiwa.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Ulega, aliniambia katika kipindi kile tunaingia kwenye kipindi cha Kamati kwamba, fedha yote ya kwanza itakayopatikana ataipeleka kule, ili mkandarasi aanze kazi Wanamorogoro Kusini, Wanamorogoro Kusini Mashariki nao waone matunda ya uhuru kwa kupata barabara ya lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa Barabara ya Ubena – Zomoni, tayari imeishaanza. Mkandarasi kapewa *advance payment* na kazi inafanyika. Kwa hiyo, ni kielelezo tosha kwamba, tutafika Kisaki maana yake tunakwenda Ngerengere, lakini Ngerengere upembuzi yakinifu na nimeona kwenye kitabu cha bajeti kuna fedha nyingine zimetumbukizwa ili kazi hiyo ikamilike, tujue tathmini na tujue thamani ya mradi. Naamini katika Bunge lijalo tutafika Kisaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nampongeza Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* kwa Barabara ya Bigwa – Kisaki, kipande cha Morogoro mpaka Mvuha, kukabidhiwa mkandarasi, maana ilikuwa *TANROADS* hawezi kufanya kazi yoyote, lakini nilimwomba kwa hali iliyokuwepo na kaweza kutoa fedha. Mkandarasi amefanya kazi nzuri na sasa hivi kutoka Morogoro mpaka Mvuha japo tunatembea kwenye vumbi, lakini tunaweza kwenda kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, Ombi langu tu kwa *TANROADS* hebu wahakikishe kwamba, tunaendelea kuboresha Barabara kutoka Mvuha mpaka kwenda Kisaki maana yake ni kama pale kuna mahali panaitwa Kisalike, barabara ni mbaya sana, wananchi wetu wanapata adha. Kwa hiyo, naomba tu *TANROADS* watukamilishie kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo ningependa kuchangia ni kwenye suala la Mfuko wa Barabara. Kelele zote ambazo zinapigika humu ndani ya Bunge ni kwamba, *TANROADS* hawana fedha. Hata *TARURA* hawana fedha, lakini Bunge limetenga fedha kwenye mafuta, ambayo ni kwa ajili ya kwenda kufanya kazi za Barabara.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu. Kamati katika ushauri wetu tumetoa kutoka Januari, 2024 hadi Februari fedha ambazo zimekusanywa, zilikuwa ni shilingi bilioni 919 na *point,* lakini hadi kufikia mwezi Februari fedha ambazo zimetoka Hazina kwenda kwenye Mfuko wa Barabara ni shilingi bilioni 289 tu, shilingi bilioni 530 badi ziko Hazina. Nini kielelezo chake?

Mheshimiwa Spika, ni kwamba, tunawapa wakati mgumu Wizara ya Ujenzi kuweza kufanya kazi za barabara wakati fedha hiyo ingepelekwa, ingefanya kazi kubwa na matokeo yangeonekana. Mvua nyingi zimepiga, fedha ambazo ziko *ringfenced* kisheria zinaendeleaje kubaki kwenye Hazina?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, atoe fedha hiyo ampelekee mdogo wangu Mheshimiwa Ulega akafanye kazi. Kule ndugu yangu alivyoingia alikuwa kijana mdogo, lakini leo ukimwangalia, kachoka kwa sababu, wanaumiza vichwa, fedha hakuna, wanakuwa wazee. Hebu pelekeni fedha hiyo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana, muda wako umekwisha.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, umekwisha! Ooh, nadhani inatosha, lakini ujumbe umekwenda. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta. Mheshimiwa Angeline Mabula, ajiandae.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, nami nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, ambaye ameniwezesha jioni ya leo kuwa katika ukumbi huu na kuchangia Bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi. Pia, naomba nimpongeze sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuboresha miundombinu ya nchi yetu bila kumsahau Waziri mwenye dhamana, ndugu yangu Mheshimiwa Ulega, Naibu wake na Ofisi nzima ya Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze moja kwa moja katika jimbo langu. Rais wetu wa Awamu ya Nne, Marehemu Dkt. Mkapa alitoa ahadi ya kujenga Barabara ya lami kutoka

Nangoma hadi Nayumbu. Barabara hii imeanza kujengwa, lakini kwa kiwango cha chini sana, *rate* yake ni ndogo mno.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zinazofanywa na Mkoa wa Mtwara, chini ya *Eng*. Dotto, naiomba Wizara iongeze kiwango cha lami ambacho kinatakiwa kijengwe kila mwaka. Nimeangalia katika bajeti ya mwaka 2025 sijaona ni kiwango gani cha lami kitaendelea kujengwa katika Barabara ya kutoka Nangomba hadi Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iangalie barabara hii ambayo ilikuwa ni ahadi ya mzee wetu, na ingekuwa bora kabisa ikamalizika. Barabara hii inakwenda sambamba na uwekeji wa taa za barabarani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika bajeti yake ameongea kwamba anazo taa za kutosha na kwamba miji yote itawekewa taa. Sasa hii ni barabara ambayo imeanza kujengwa, na sasa hivi ina kilometa kama sita, lakini haina taa hata moja. Ni matarajio yangu kwamba atakapohitimisha hotuba yake atatoa neno.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, pia tuliomba Wizara ichukue barabara ya kutoka Mangaka – Sengenya – Matekwe ihamishwe kutoka *TARURA* kwenda *TANROADS*. Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu swali langu, alikubali ombi hilo na kwamba barabara hiyo ingechukuliwa. Nimeiangalia katika hotuba yake sijaona barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu kwamba atasema neno, kwamba ni lini barabara hii itachukuliwa na *TANROADS;* kwa sababu *TARURA* kiwango cha fedha wanachokipata ni kidogo na matengenezo yake ni ya chini sana. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri afanye hilo jambo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu taa za barabarani. Sisi pale tulipata mradi wa kuwekewa taa za barabarani, lakini mkandarasi ameshindwa kuendelea na zoezi hili kwa sababu hajalipwa. Kuna mkandarasi pale anaitwa Shibesh amefanya kazi hiyo pale Nanyumbu, na Mangaka Mjini, lakini ameshindwa

kumaliza kwa sababu hajalipwa fedha zake na hiyo kazi hajaimalizia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Wizara itueleze ni lini mkandarasi huyu atalipwa fedha ili aweze kumalizia uwekaji wa taa za barabarani katika Mji wetu wa Mangaka ambayo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ya Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba tena nichukue nafasi hii kuipongeza sana Wizara na kumpongeza sana *Engineer* wangu wa Mkoa wa Mtwara ndugu yangu Doto kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuhakikisha kwamba miundombinu yetu inaboreshwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta atafuatiwa na Mheshimiwa Angeline Silvester Mabula na Mheshimiwa Stella Simon Fiyao ajiandae.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyoko Mezani. Pili, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuishi hadi leo. Pia nashukuru kwa ushirikiano mkubwa ninaoupata kutoka kwa wananchi wa Urambo na familia yangu.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Ulega; Naibu wake, *Engineer* Kasekenya; Katibu Kkuu wake, Aisha Amour; na Naibu wake, Dkt. Charles Msonde na Watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi. Kwa kweli Wizara ina kazi kubwa sana, lakini kwa jinsi Mheshimiwa alivyowateua, wao wana uwezo mkubwa na watazikabili shughuli zote ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutusaidia miradi mikubwa sana Urambo. Kwa sababu ya muda nitaitaja michache tu, maji kutoka *Lake* Victoria ambayo yameshakaribia kujaa sasa. Pia, kituo cha kupozea umeme ambapo tulipata Bahati Jumamosi iliyopita; Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ambaye pia ni

Waziri wa Nishati alifika akatoa baraka zake, sasa hivi tunapata umeme moja kwa moja. Tunamshukuru sana Dkt. Samia.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuishukuru Wizara ya ujenzi kwa kutupa miradi miwili mikubwa ambapo nashukuru kwamba Serikali inatujali sisi watu wa Urambo. Kwanza ni barabara inayopita katikati ya Urambo kwenda Ulyanhulu, inapita katikati ya soko la ndizi. Soko la ndizi ni kubwa sana na lina watu wengi sana, tena akina mama ndio wengi zaidi. Wameipandisha ile barabara. Ilikuwa *TARURA*, sasa hivi imekuwa ya *TANROADS.*

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba ile barabara ifanyiwe haraka sana kwenye kazi ya kuweka alama kwa sababu inapita katikati ya soko, halafu iwekewe taa, sasa hivi haina taa. Tunaomba taa ili kunusuru maisha ya watu. Nawaomba Wizara ya Ujenzi waongeze fedha za marekebisho ya alama za barabarani. Yaani kuweka alama ili watu waweze kupona na ajali.

Mheshimiwa Spika, pia, naishukuru Serikali kwa kutupa Barabara ya Tutuo – Usoke au Usoke – Tutuo, maana ni kwamba sasa wanatufungulia mlango. Nimeona katika miradi ya mwaka huu 2025/2026 wameuweka katika kikundi ambacho kitapata usanifu. Kwa hiyo, barabara hii itafanyiwa usanifu. Naiomba sana Wizara ya Ujenzi, hii ni barabara ambayo itatufungulia milango ya magari mengi kutoka Kahama kwenda Sikonge - Tutuo hadi Mbeya. Kwa hiyo, tunaomba iwekewe fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, la tatu napenda kuwaomba Wizara ya Ujenzi kwa heshima na taadhima watusaidie kuweka taa. Barabara ya Kigoma inapita Urambo, inakuja huku mbele, ina maeneo mengi ambayo ajali ni nyingi.

Mheshimiwa Spika, nitaje maeneo ambayo tunahitaji kuwekewa alama, ikiwemo Vumilia, naomba taa na alama; pia, Mbaoni, Kona ya kuingia stendi ya mabasi na barabara inayotoka Polisi kuja kuungana na Barabara ya Kigoma nayo iwekewe taa na alama kwa sababu ajali zinakuwa ni nyingi sana. Halafu na maeneo ya Kona ya Polisi ambayo inajulikana kama ni eneo la Kasu, tunaomba nalo liwekewe alama na taa. Vilevile, Maili Nne, Katuli, Kona ya Usoke na Tutuo nazo ziwekewe alama.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi haya niliyoyataja naomba Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Naibu wake wayachukue ili wayawekee taa kwa sababu tumepata ajali nyingi sana. Hata juzi tu walifariki watu wawili kutokana na kwamba wanavuka wanatoka kwenye barabara ndogo wanaingia kwenye barabara kubwa ya Kigoma, inatuletea matatizo sana.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, barabara inayotoka Kigoma inapokata kona ikitoka Kigoma inakata kona mkono wa kushoto kuingia Urambo Mjini nayo imeleta ajali nyingi sana. Kwa hiyo, naomba maeneo haya yafanyiwe kazi ili kweli tuone nia ya Serikali ya kuokoa maisha ya wananchi wa Urambo.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nilikuwa nafikiria kwamba kukaa na barabara ambazo hazina alama ni hatari sana. Naomba, na tena ninarudia kuwaomba, kwamba waweke fedha za kutosha ili zisaidie kuokoa maisha ya watu kwa kuweka alama.

Mheshimiwa Spika, namshukuru *Engineer* wetu wa *TANROADS* wa mkoa, *Engineer* Mlimaji, anafanya kazi kubwa sana na anashirikiana na sisi. Kwa hiyo, tunamwombea kila la heri na afuatilie hii miradi tukiamini kwamba barabara ndizo zinazofungua maeneo na kuletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, narudia kumwomba tena Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, nina imani naye, kwamba barabara ile inayopita katikati ya soko iwekewe taa na alama haraka iwezekanavyo, halafu kila mwaka wawe wanaongeza kilometa moja kwa sababu ndiyo inayokwenda kuunganisha Ulyanhulu. Tunaomba iongezewe badala ya kilometa moja, basi angalau ziwe mbili kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, ukichukua kilometa moja kila mwaka na ni kilometa 59, si itachukua miaka hamsini na ngapi, na wengine tutakuwa tumeshakwenda Mbinguni! Kwa hiyo, tusaidiwe basi barabara ile iongezewe kilometa, ahsante sana. *(Makofi)*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nawatakia kila la heri na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Angeline Sylvester Mabula atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Simon Fiyao na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka ajiandae.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami nimshukuru Mungu kwa fursa ambayo nimeipata leo ya kuchangia Wizara hii. Nawapongeza Wizara na Serikali yote kwa ujumla kwa namna ambavyo dira ya Wizara imeweza kutekelezwa vizuri, ambapo inazungumzia habari ya kuwa na miundombinu endelevu itakayochochea maendeleo ya kijamii pamoja na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imefanya kazi kubwa hasa katika kuunganisha mikoa. Madaraja na kila miundombinu iliyotakiwa imeweza kujengwa. Tunawapongeza sana, kazi hiyo ni kubwa sana. Tunawapongeza kwa sababu ni mafanikio makubwa katika kukuza na kuchochea uchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninalo jambo moja dogo na la msingi sana kuhusiana na suala zima la barabara zinazotolewa kwa wakandarasi kwa ajili ya ujenzi. Nitolee mfano tu katika Mkoa wa Mwanza, nilikuwa ninajaribu kupitia kwenye wilaya, nilifikiri labda ni kwangu tu peke yake, kwamba barabara ambazo zinatolewa hazikamiliki. Hizi barabara nitakazozitaja zote ni za mweaka 2023/2024. *Airport* Igombe – Kayenze kilometa 46 amepewa mkandarasi kilometa 10 toka 2023/2024 lakini mpaka leo hakuna hata kilometa moja imejengwa na mkandarasi hajafika *site*.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Nyakato – *Steel VETA* mpaka Igombe imeanza 2017, kilometa 18 mpaka leo haijatimia. Kwenye hii taarifa, wanaonyesha kuna upembuzi yakinifu umekamilika kwa kilometa tatu zinazozungumzia suala la Nyakato – *VETA* – Busweru, eneo ambalo tayari limeshajengwa. Kule ambako hakujajengwa, nadhani wamepitiwa katika kuweka

taarifa hizo. Ni mbele kule Shibula kwenda TX ndiko ambako hakujajengwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni Barabara ya Isandula – Magu – Ngudu kilometa 50, ujenzi ni kilometa 10 na kazi bado. Mwanangwa – Misasi – Salawe inaunganisha katika Wilaya ya Kahama kilometa 150, ujenzi ni kilometa tatu, lakini ujenzi huo bado. Ngudu – Jojilo – Mabuki, kilometa 28, ujenzi ni kilometa tatu. Kamanga – Katunguru – Sengerema kilometa 32, ujenzi ni kilometa tatu. Nansio – Rugezi kilometa 11, ujenzi ni kilometa saba.

Mheshimiwa Spika, natoa masikitiko kwa sababu barabara zote hizi zinaunganisha maeneo ambayo uchumi wa Jiji la Mwanza ndiko unakotoka, kwa sababu ni lazima waingie majini kuleta mazao yao. Sasa, kama barabara hizi hazikamiliki lengo la kuchochea uchumi katika jamii linakuwa pia halijafikiwa sana.

Mheshimiwa Spika, naomba sana, kandarasi hizi zimekaa muda mrefu na siyo kwa Mwanza tu, ni *almost* kwa nchi nzima. Mimi nimechukulia *sample* kwa Mwanza kwa sababu kila Mbunge anayesimama analalamika. Kwa hiyo, naomba sana kazi inayofanyika ni kubwa na nzuri. Tumwombe Mungu tusipate tena madhila ya pengine kuwa na mvua nyingi ambazo zinaharibu barabara halafu unakuta bajeti inalegea katika eneo moja. Kwa hiyo, naomba sana katika hili tuangalie ili tuweze kuona ni namna gani tunaweza kwenda.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuwajali wakandarasi wazawa ambao tulikuwa tumeambiwa hapa; kwenye zabuni ambazo wamepewa za thamani ya shilingi bilioni 50 bado ni kidogo kwa sababu hawa wana uwezo mkubwa na wanaweza kufanya kazi kama watapewa. Wanaonekana goi goi pale ambapo fedha inakuwa haitoki, naye pale pale anakuwa anashindwa kukataa kazi. Amepewa kazi anaipokea na hawezi kupata fedha, na matokeo yake unakuta wanapata *portion* ndogo katika keki kubwa ya Taifa. Lengo letu au lengo la Serikali ni kuwaimarisha hawa waweze pia kuwa wakandarasi wakubwa na waweze kufanya kazi zetu kwa uzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia Daraja la Busisi – Sengerema ambalo Mbunge ameomba liitwe hivyo, daraja hili linakwenda kuchochea uchumi mzuri katika maeneo hayo, lakini kutoka pale, ukishavuka, ukitaka kwenda maeneo mengine huwezi kufika kwa sababu barabara hazijatengenezwa. Ukitaka kwenda Buyagu uende mpaka kule Msalala kwa wakwe zangu bado pia ni changamoto. Kwa hiyo, naomba sana, tunapounganisha miundombinu, tuangalie pia kule kwenye *source* ya uchumi ambako kuna wazalishaji mali wengi ambao wanatakiwa pia mizigo yao iweze kufika katika maeneo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara. Mheshimiwa Ulega mjukuu wangu pamoja na *Engineer* Kasekenya, kazi wanayoifanya ni kubwa. Ombi langu, kama fedha ni kidogo zisitolewe kazi nyingi. Tutoe hizo zilizopo zikamilike. Tunaacha viporo vingi matokeo yake wananchi wanalalamika, pia, malipo yanachelewa. Kwa hiyo, twende kulingana na bajeti, tunamaliza hili na tukilianza basi tulimalize. Kilometa 50 unatoa kilometa tatu na 150 unatoa kilometa tatu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Stella Simon Fiyao atafutiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga ajiandae.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika bajeti ya Wizara hii ya Ujenzi, Wizara ambayo ni muhimu sana na inayotegemewa kwa asilimia kubwa sana na wananchi wote wa chini, masikini, na matajiri, wote wanaitegemea Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa na mambo machache kutokana na muda. Jambo la kwanza nitaomba nizungumzie

Barabara ya Igawa – Tunduma. Sote tunajua umuhimu mkubwa wa barabara hii. Zaidi ya 73% ya mizigo inayopitia katika Bandari ya Dar es Salaam inakwenda kupita katika mpaka wa Tunduma, kwa kuwa mizigo mingi inapita inakwenda huko nchi za *SADC,* kwa hiyo, barabara hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, barabara hii imekuwa kuna changamoto sana. Wananchi wanajua kwamba barabara hii inachangia kwa asilimia kubwa kwenye pato la Taifa lakini changamoto ambazo tumekuwa tukikabiliana nazo wananchi tunafika mahali tunafikiri kwamba hivi Serikali wanakiona hasa kile kinachoendelea Tunduma au hawaoni? Kama wanaona, je, ni hatua gani za haraka na za dharura ambazo wanazichukua ili kutunusuru wananchi wa Mji wa Tunduma? Hali siyo nzuri kwa kweli. Tunayasema haya huku tunafikiri kwamba hivi kwenye hii Wizara hakuna fedha za dharura za kuweza kutusaidia pale Tunduma?

Mheshimiwa Spika, mlundikano mkubwa wa magari uliopo Tunduma kwa kweli ni hatari. Siyo magari ya mizigo tu, yako magari ya mafuta ambayo nayo yanakaa kwenye foleni pale zaidi ya masaa, kitu ambacho pia ni hatari na kinaweza kuhatarisha hata mazingira. Serikali hebu walione hili.

Mheshimiwa Spika, sisi tunajua umuhimu wa barabara hii, lakini tuone, wanakuja na mpango wa haraka. Hata kama barabara hii wameiingiza kwenye *PPP,* lakini ukweli ni kwamba changamoto ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, tunajua jitihada kubwa ambazo anazifanya Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha kwamba anafungua uchumi wa nchi yetu, lakini watuone kwa jicho la namna ya pekee kabisa, watuangalie Tunduma, hali siyo nzuri. Kuna umuhimu mkubwa wa kutengeneza barabara nne ili kunusuru maisha ya Wanatunduma na ili kuokoa muda. Jamani tusaidieni, yaani wakati tunasimama kuzungumza mara mbili mbili hapa kwa habari ya Mji wa Tunduma, lakini sisi tunaoishi pale tunaona.

Mheshimiwa Spika, unajua kuna wakati nafikiri Mawaziri hata wakija pale huwa ule msongamano wanau-*balance*. Kwa hiyo,

hawaoni adha ambayo wananchi wa Mji wa Tunduma tunakutana nayo. Natamani siku moja wakija, mahali ambapo wanaweza kutumia dakika tano wakitumia masaa matano pengine wanaweza kufikirifikiri namna ya kutusaidia Wanatunduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatusemi tunayakataa yale malori, tunayakubali kwa sababu ni sehemu ya kuchochea uchumi wetu, lakini je, wanatuchukuliaje na wanatuweka kwenye mazingira gani wananchi wanaoishi kwenye ule mji? Serikali waone namna ya kutusaidia ili kutunusuru na ile adha ya foleni ambayo imekuwa ni *too much.* Hali siyo nzuri. Mahali pa dakika tano unatumia masaa Matano. Wao wakija wana nafuu.

Mheshimiwa Spika, nimesema hapa, mawaziri wakija pale huwa panakuwa *balanced,* wanapata namna nzuri ya kupita, lakini wanaweza kufikiria kuhusu wananchi ambao wanaamka na kulala pale? Ile hali ikoje? Kwamba wameshindwa kustusaidia! Watusaidie basi walau njia nne zianzie Tunduma au hata Chimbuya, pengine wanaweza kutupunguzia ile adha ambayo tunakutana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waangalie basi, kwani ni kilometa ngapi? Mpaka ule unaingiza kiasi gani cha fedha? Mbona ni mamilioni ya fedha yanaingia kupitia ule mpaka. Namna gani wanashindwa kutusaidia? Kutoka *custom* kuelekea Chimbuya tu, yaani kwa kuanzia tu ili watutie moyo tujue kwamba Serikali wanaliona lile ambalo linaendelea pale Tunduma. Watutie moyo hata kwa kilometa 10 ama 20 watakuwa wametusaidia na Tunduma tutajua Serikali wanathamini uwepo wa ule mpaka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, tunaomba watusaidie kuepukana na ile adha ya mlundikano wa magari kwa kututengenezea njia nne ambazo pengine basi zianze tu pale pale. Tumesema yaani walau kwa kututia moyo...

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella, ahsante sana.

**MHE. STELLA S. FIYAO: ...**zianze pale *Custom* ziishie hata Chimbuya halafu ndipo waendelee na huko kwingine. Muda wangu umekwisha?

**SPIKA:** Umekwisha.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Aah, hii ni hatari. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga na Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoitendea haki nchi hii. Vilevile namshukuru na nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Mtendaji Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, pongezi zangu za pili zinakwenda kwa Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Ulega na msaidizi wake, *mate* wangu, Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya na bila kumsahau Mtendaji Mkuu wa *TANROADS,* Mohamed Besta, kuruta mwenzangu, *Operation Programme* ya Chama, Ruvu JKT. Vilevile, nampongeza Mtendaji Mkuu wa Wizara hii dada yangu Aisha.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kuziongelea barabara kuu mbili zinazoingia Liwale. Barabara ya Nangurukuru – Liwale na Nachingwea – Masasi – Liwale. Hapa niweke rekodi sawasawa. Barabara hii ya Nachingwea – Masasi – Liwale upembuzi yakinifu ulikamilika mwaka 2014. Barabara hii kama ingejengwa kipindi kile, maana yake leo ingekuwa ni miongoni mwa barabara zile za kufanyiwa *service*.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kumbukumbu hizo zisipotee, barabara hizi ninazozungumzia, zimezungumziwa kwenye bajeti zote nilizokuwepo katika Bunge hili. Tangu wakati wa Mheshimiwa Eng. Kamwelwe, akaja Mheshimiwa *Engineer* Dkt. Chamuriho,

Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Mheshimiwa Bashungwa na leo Mheshimiwa Ulega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana barabara hizi zijengwe, na nasema muda wote, barabara hizi zilikuwa zinatengewa fedha lakini fedha haziji. Kwa mwaka huu nina imani Mheshimiwa Ulega barabara hii anakwenda kuijenga. Imani yangu inanipa, kwa sababu yeye ni mtoto wa Mhuba na mimi ni mtoto wa binti Mhuba hivyo hivyo. Kwa hiyo, yeye ni wa nyumbani.

Mheshimiwa Spika, naomba sana impendeze barabara hii mwaka huu ijengwe. Nimeiona kuna kilometa 72 Nanguruku – Liwale; kilometa 55 Nachingwea – Liwale. Basi ninaomba sana barabara hizi mbili zijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanapobandua lami au wanapopanua barabara huwa ninachukulia mfano kama vile mama anamwambia mwanaye, usile huu ugali wa jana umechacha, kwa hiyo, anamtafutia ugali mpya ampe; lakini kwenye nyumba hiyo hiyo, boma hilo hilo yuko mtoto wa mama mkubwa, mama mdogo hajala.

Mheshimiwa Spika, naomba busara iwatume kumpatia chakula yule mtoto ambaye tangu jana hajala, badala ya kumpa huyu ambaye jana amekula ila sasa unaogopa leo asile hiki chakula kimechacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yangu ni nini? Ni kwamba barabara sasa, maana kuna watu wengine hapa wanaomba taa za barabarani, wengine hapa wanaomba barabara zipanuliwe, mimi kule kwangu naomba barabara ili ziweze kupitika, wananchi wale waweze kufaidi matunda ya nchi hii na mazao ya wakulima yaweze kufika kwenye masoko. Mheshimiwa Ulega niliomba tu dakika tano niyasema hayo.

Mheshimiwa Spika, juzi Mwenezi Taifa alikuja Liwale, mimi wakati wa kurudi, nikalala njiani, nimelala porini. Juzi nimejipendekeza hapa niende kwenye *May day* nimeingia leo hapa, nimelala njiani lakini jana ilikuwa nihudhurie hapa lakini nimelala porini, nimekuja Dar es Salaam leo asubuhi,

nimeunganisha nipo Dodoma. Nikuombe sana, watu wanateseka.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni ajiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Napenda nimshukuru Mungu kwa kunipa nafasi siku ya leo tena niweze kuongea kwenye hii Hotuba ya Wizara ya Ujenzi. Napenda niishukuru Serikali jinsi inavyopambana kuboresha nchi yetu, lakini muda hautoshi nilenge moja kwa moja kwenye hoja.

Mheshimiwa Spika, Waziri mpya ambaye ameteuliwa hivi karibuni sina cha kumshukuru, bali nina maombi. Barabara ya kutoka Katoro kwenda Ushirombo, naomba kwenye bajeti yake itengewe fedha iweze kufanyiwa ukarabati ikiwezekana iwekewe lami kabisa, maana ni barabara muhimu sana kwa watu wa Bukombe pamoja na Mbogwe.

Mheshimiwa Spika, ipo barabara ya kilometa 72 kutoka Kashero kupitia Mbogwe kwenda Lugunga mpaka Masumbwe. Nikisema hivyo, Naibu Waziri wa Ujenzi anaijua kwa sababu ni mwenyeji maeneo hayo. Hii barabara tunaomba iwekwe kwa kiwango cha lami maana hata kwenye ilani imeingizwa kwamba, ni barabara inayounganisha mkoa na wilaya.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu, kuhusu taa za barabarani. Ninayo maeneo ambayo yanahitaji taa za barabarani, nina Mji wa Lulembela ni mji mkubwa sana, ni mji wa pili ukitoa Mji wa Masumbwe, Lulembela ni ya pili kwa wingi wa watu. Kwa hiyo, pale watu wa Lulembela wamenituma kuomba hapa kwamba taa za barabarani kama vile 100 hivi na kwenye hotuba imeelezwa kwamba, taa wanazo. Kwa hiyo, natamani mwezi wa kumi nifanye kampeni nikiwa kwenye taa za barabarani pale Lulembela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine kutoka Kanegere mpaka Lubeho ni kilometa 20. Hii ni barabara kuu iendayo Congo kutoka Dar es Salaam. Nashukuru kwa yale matangenezo yanayofanyika, lakini yale maeneo yana wafanyabiashara wengi, tunahitaji taa za barabarani sasa kuanzia Kanegere kwenda Lubeho. Haya maeneo Mheshimiwa Kasekenya naomba Waziri anayafahamu, yawekewe taa za barabarani ili wafanyabiashara waweze kufanya biashara zao vizuri na kazi iendelee.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni madaraja. Kutoka Masumbwe kwenda Mwabomba kuna daraja kubwa pale Mheshimiwa Eng. Kasekenya analifahamu. Pamoja na kwamba, limetengewa bajeti, lakini mpaka sasa hivi halijaanza kutengenezwa na kila mvua zikianza kunyesha zile barabara huwa ni korofi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naoimba Serikali haraka iwezekanavyo kabla hatujaingia kwenye nyakati zile ngumu za hatari, iweze kurekebishwa ili kusudi wananchi wa maeneo haya waweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ninaloliomba hapa, kuna Mji wa Segese kupitia Mbizi kuja Mpakali - Masumbwe Mjini. Naomba eneo hili lichukuliwe na *TANROADS* kutoka *TARURA,* hata kwenye vikao vya kimkoa nimeshalipendekeza, kwa sababu ni barabara muhimu ambayo inaingiza mapato mengi. Sasa ikichukuliwa na ninyi watu wakubwa wa *TANROADS* itakuwa inafanyiwa marekebisho ya kutosha, na uchumi wa maeneo ya Mbogwe utafunguka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo lingine hapa ninalotaka niliombe ni stendi ya malori. Mji wa Masumbwe ni mkubwa, pale madereva wanapenda kila wakifika lazima wapumzike, magari yanapaki barabarani. Kwa hiyo, nyakati za usiku watu wanapofanya biashara zao, huwa wanapata shida sana, na ajali zinatokea nyingi. Tulishatenga eneo ili kusudi *parking* ya malori itengenezwe ili madereva hao wanapofika Mji wa Masumbwe waweke magari yao pazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wizara hii nilishaongea na Meneja wa Mkoa anajua. Kwa hiyo, haraka iwezekanavyo hiyo *parking* iweze kuboreshwa ili watu wanapokuwa wakisafiri kwenda nchi za nje, wakifika Mji wa Mbogwe Masumbwe wapumzike pazuri ili kusudi malori yakae pembeni yasikae barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, napenda kukushukuru wewe kadiri unavyotuendesha kwenye Bunge lako hili Tukufu. Hakika mama tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu, wala siyo unafiki unatutendea Wabunge, japokuwa unatupa muda huu ambao umepangwa kwa siku ya leo dakika tano tano, lakini tuna imani kwamba, ujumbe wetu unafika.

Mheshimiwa Spika, cha muhimu tu, tuiombe Serikali, haya mawazo tunayoyatoa hapa, yaani muda tunaoutumia huu mchache kuzungumza hapa, ni vitu muhimu ambavyo vinatakiwa na wananchi. Kama mnavyofahamu sisi ndio wawakilishi wa wananchi, hatuzungumzi maisha ya kwetu, hatuzungumzi mawazo yetu hapa, ndiyo maana nikasema nitampongeza Waziri sana haya niliyoyasema hapa machache kama atayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa siku ya leo haipo sababu ya kushika Shilingi ya Waziri isipokuwa naomba tu haya niliyoyazungumza, ikiwemo taa za barabarani na madaraja akayaboreshe, na sasa atakuwa mtu bingwa sana Mheshimiwa Ulega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** *Wabheja sana, wabheja sana*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya atafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mheshimiwa Elibariki Emmanuel Kingu ajiandae.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, nami nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa hii nafasi kuchangia. Kipekee namshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kule kwetu Manyoni. Namshukuru na nimpongeze ndugu yangu Mheshimiwa Ulega, akiwa Wizara ya Mifugo alifanya mambo makubwa Manyoni, alitujengea mnada mmoja mkubwa sana, mkoa mzima uko pale.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, bila kumsahau *DG* wa *TANROADS,* lakini kule mkoani kwangu na Mheshimiwa Ulega aliniletea Meneja wa Mkoa *Engineer* Singano, anafanya kazi nzuri sana. Kwa kweli namshukuru na ninaomba asimtoe Singida, amepambana sana kule kwenye barabara korofi ambazo kisiasa zilikuwa hazijakaa vizuri, lakini sasa hivi anazitatua. Kwa hiyo, naomba asije akanitolea yule Meneja, tunaenda kwenye uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina maeneo mawili ningependa kuchangia Wizara ya Ujenzi, na kaka yangu, Mheshimiwa Ulega anajua daraja lake la Sanza. Siku hizi Naibu Waziri namwita Mzee wa Sanza kwa sababu kila siku anataja Daraja la Sanza kwenye maswali.

Mheshimiwa Spika, Daraja la Sanza lipo kwenye Ilani ya Uchaguzi, ni Daraja la kimkakati, taarifa nyingi zinaonesha tayari mkandarasi alishapatikana, hatua iliyobaki na taarifa inasema ni kusaini mkataba.

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Ulega hebu hili Daraja la Sanza twende tukalikamilishe, mkandarasi asaini mkataba kwa sababu wananchi wanasubiri sana na Mheshimiwa Rais alienda Manyoni mwaka 2023, kwa kweli aliwaahidi wananchi na aliwapa matumaini kwamba, lazima Daraja la Sanza litajengwa. Kwa hiyo, hili mimi niliomba niweke msisitizo kwa hili Mheshimiwa Waziri Ulega Daraja la Sanza liwe kwenye *priority* zake kwenye huu mwaka ambao tunaenda.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, Manyoni tuna kituo cha pamoja cha ukaguzi wa magari *(One Stop Inspection Station)* cha Muhalala. Hiki kituo kipo vilevile Nyakanazi Kagera Bukoba.

Ujenzi wa hiki kituo ulisimama mwaka 2017/2018 na kilishafikia takribani 60%, cha Nyakanazi kilishafikia 50%.

Mheshimiwa Spika, wale ambao mnapita kuelekea Mwanza, kabla hujafika Manyoni pale Mlimani, kuna nyumba zipo pale zimejengwa. Sasa taarifa niliyonayo ni kwamba, Serikali imeshafanya jitihada nyingi sana kuhakikisha kwamba, inafufua huu mradi, na kwa kiufupi nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu huu mradi ulikuwa umetelekezwa, lakini kwa *commitment* ya Rais, mradi huu unaenda kuanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba huu mkataba upo kwa *Attorney General (AG)* kwa ajili ya upekuzi na taarifa yao inasema hivyo. Sasa ningeomba hili zoezi la upekuzi basi lisichukue muda mrefu kwa sababu tayari huu mradi umekaa muda mrefu haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, huu mradi ni mzuri sana, utachochea sana uchumi wa Manyoni, vilevile, utaenda kukuza na kusaidia sana kwenye ukusanyaji wa mapato ya *TRA*, lakini unaenda kulinda barabara yetu hii ambayo kimsingi malori makubwa yanapita kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, huu Mradi wa Muhalala wa ukaguzi wa pamoja wa magari uwekee kipaumbele na fedha. Taarifa niliyonayo, fedha zipo, kwa sababu ni fedha za *EU,* tatizo tu ni kwamba, ni kufuata *formalities* za kumpata mkandarasi mwingine na tayari mkandarasi mwingine alishapatikana, ni suala la mkandarasi kusaini mkataba mwingine. Sasa hili sidhani kama linahitaji karne au *decade,* ni suala ambalo linaweza likafanyika *within two weeks* na mkandarasi akapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho nina maombi. Nimeona kwenye taarifa yao humu wameweka barabara ya *Manyoni East* – Heka – Sanza - Ikasi - Chali – Igongo - *Bihawana Junction* ya kilometa 192. Hii barabara ni ya kimkakati kwa sababu inalisha Mkoa wa Dodoma ambao kimsingi ni Makao Makuu. Vilevile, inaweza ikatumika kama *diversion road* inapotokea dharura kati ya Manyoni na Dodoma. Tayari imeshawekwa kwenye upembuzi

yakinifu na usanifu wa kina. Mheshimiwa Waziri hii barabara naomba uiweke katika vipaumbele vyako, ni barabara ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya pili ni barabara ya kutoka Singida – Ikungi – Londoni - Kilimatinde takribani kilometa 117 nayo kwenye taarifa imewekwa kwamba, inafanyiwa upembuzi yakinifu. Hii ni barabara ya kimkakati ikitokea dharura kutoka Ikungi kuja Manyoni tunaweza tukatumia hii barabara ya kutoka Ikungi - Londoni – Solya - Kilimatinde kwa ajili ya kufika Dodoma. Kwa hiyo, ningeomba isiishie tu kuwekwa kwenye taarifa, lakini ningeomba ifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, ajiandae.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na uzima, na kabla sijazungumza sana ili nisisahau, niseme kwamba, siungi mkono hii bajeti ili tukae sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani kumbukumbu zinaonesha nimekuwa nikizungumza mara nyingi hapa, nikisisitiza kwamba mimi natoka Sumve, na Jimbo la Sumve halina hata milimita moja ya lami. Tunazungumza hapa watu wazima, Mawaziri wapo na Serikali inatuahidi, lakini haitekelezi. Sasa ni vizuri tugawane mbao kila mmoja aendelee na mambo yake kwa sababu wameamua kutukwamisha kwa makusudi; na kwa ujeuri nami ninatawakwamisha leo kwenye bajeti yao.

Mheshimiwa Spika, sitaiunga mkono bajeti hii, nitashika Shilingi mpaka! Najua hapa hawaendi kujenga wala nini, maana wameshaniahidi mara nyingi sana, lakini bora hata kama siwezi kuwapiga mkaumia, bora nioneshe nimekasirika.

Mheshimiwa Spika, sasa hizi hasira za watu wa Sumve dhidi ya hii dharau inayoendelea kwenye Wizara ya Ujenzi, nimetumwa kuja kuziwasilisha. Ni kwamba, kumbukumbu zinaonesha Wilaya ya Kwimba ipo Mkoa wa Mwanza, lakini ni wilaya pekee ambayo haijaungwa na mkoa kwa lami.

Mheshimiwa Spika, sio mimi niliyeanza kusema. Mwaka 1995, Rais Mkapa akiwa anaomba kura aliahidi atatuunga, haikufanyika. Mwaka 2005 Rais Dkt. Kikwete wakati anaomba kura aliahidi, haikufanyika. Mwaka 2015 Rais Dkt. Magufuli anaomba kura aliahidi, haikufanyika. Mwaka 2022 kwa sababu tuna uhaba wa ziara za viongozi wa Kitaifa, kwa sababu wakifika Mkoa wa Mwanza wanakwamishwa kwenda Kwimba kwa sababu hakuna barabara zinazoeleweka. Makamu wa Rais alipita akaelekeza Wizara iende ikaone, watengeneze barabara ile, hawajaenda.

Mheshimiwa Spika, sasa nafikiri nimeshagundua kwamba, sisi Mkoa wa Mwanza tuliwekwa kimakosa, kwa sababu haiwezekani sisi ndio hatujaunganishwa. Ukiangalia historia ya Mkoa wa Nyanza, Wilaya ya Kwimba ni kongwe katika wilaya za kwanza Maswa, Kwimba, Musoma, Geita, Bukoba, Shinyanga na Mwanza yenyewe zina lami kasoro sisi. Tumezaa Wilaya ya Misungwi, Busega, na Magu zina lami kasoro sisi.

Mheshimiwa Spika, sasa leo nimetumwa tuje tugawane mbao humu, maana haiwezekani tukaendelea kuwa tunafuatafuata tu hapa, tunawaunga mkono, mnatudanganya.

Mheshimiwa Waziri, uongo wa Wizara yako wameshiriki Mawaziri wengi sana humu sio wewe tu. Tumeanza na Mheshimiwa Mzee Eng. Dkt. Chamuriho pale akashiriki uongo, akaja Mheshimiwa Prof. Mbarawa akashiriki uongo, akaja kaka yangu Mheshimiwa Bashungwa akashiriki uongo, na wewe uko kwenye huo huo uongo kwa sababu kuna kilometa 10 feki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri tuliwahi kukutana na watumishi hewa. Sasa kuna kilometa kumi hewa Sumve, barabara hewa ambayo tunaambiwa imesainiwa haijawahi kujengwa hata hiyo

greda kuliona hatujawahi. Tukiwaambia kwamba, lami hatuijui mtuelewe. Wengine mnazibandua, wengine hatuna.

Mheshimiwa Spika, yule mkandarasi yuko pale ni hewa. Naona Waziri hapo anamnong'oneza Mheshimiwa Eng. Kasekenya, yaani watakushirikisha tu huo uongo, hawajawahi kujenga, lakini hapa tunaambiwa wamesaini, wanaandika kwenye makaratasi. Sisi tutapita kwenye makaratasi? Yaani gari zetu zitapita kwenye haya makaratasi yenu ya bajeti? Si yanatakiwa yapite kwenye lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilometa 73 hatujawahi kuona lami. Hatupiti sisi, au tuko Tanzania kimakosa! Haieleweki, yaani kila siku mnatudanganya hapa! Sasa nimeona bora niwaoneshe kwamba tumechukia, hatukubaliani na huu uongo, na sisi watu wa Sumve tunataka tukitokea Magu, tukiwa tunapita Ngudu mpaka Hungumalwa, tupite kwenye lami.

Mheshimiwa Spika, tukitokea Fulo, tupite Nyambiti twende mpaka Maswa kwa lami, lakini ninyi hamtaki, mmethibitisha hili kabisa bila shaka. Hatujaungwa Mkoa mzima wa Mwanza, na viongozi wa kitaifa hawaji kwetu kwa sababu hamna namna watakuja, tumeachiwa tukae na vumbi letu tuendelee na maisha yetu ya shida na ninyi mnatudanganya kila siku na bajeti siiungi mkono, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ajiandae.

Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya, na wamefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Ulega kwa kweli tumeona jinsi unavyochacharika kukimbia huku na huku na kuhakikisha kwamba, barabara zinakamilika. Pia, Naibu wako anafanya kazi nzuri sana, nawapongezeni sana na nina imani hata wananchi wenu watawarudisha tena katika nafasi hizi mnazoenda kugombea kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, pia, niwapongeze watendaji wa taasisi zilizopo chini ya Wizara hii na hasa *TBA,* wanafanya vizuri sana lakini zaidi *TANROADS* wanafanya vizuri sana, wamejitahidi sana kujenga barabara pamoja na madeni makubwa ambayo yapo.

Mheshimiwa Waziri, hebu jitahidi sana kuongea na Wizara ya Fedha, watafute fedha tupunguze haya madeni ili *TANROADS* waendelee kujenga barabara na kuunganisha maeneo mbalimbali. Kazi ni nzuri, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake wa kuamua kwamba, baada ya kuona Watanzania tunavyochacharika na tunavyohangaika kujenga nchi hii, aliona wanawake wako nyuma kiuchumi, akaamua kwamba, katika mojawapo ya barabara ambazo zinajengwa na *TANROADS,* basi itafutwe barabara moja wapewe wakandarasi wanawake ili wajenge.

Mheshimiwa Spika, kila mkandarasi apewe kilometa tano halafu wajijengee uwezo wa kiuchumi, lakini waondokane na umaskini. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara iliyochaguliwa inaitwa njia Panda ya Iyula – Idiwili hadi Nyimbili kilomita 20, kwenye bajeti ya mwaka huu 2024/2025 ipo lakini mchakato wa manunuzi bado haujakamilika. Kumekuwa na changamoto za kukamilisha hiyo barabara.

Mheshimiwa Spika, sasa wale wanawake tuliwaahidi tukasema tutawajengea uwezo, tutawapa hizo barabara kila mtu kilomita tano mjenge. Wananchi kule wakaondoka kwenye

maeneo wakapisha ile barabara ikamilike, lakini mpaka leo bado mchakato haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri Ulega, aangalie namna ya kukamilisha mchakato wa manunuzi, wakandarasi hawa wanawake wapewe hizo barabara waendelee kuzijenga ambazo zina manufaa makubwa sana katika uchumi wa eneo lile katika kusafirisha mazao na vitu vingine. Kwa hiyo, tunakushukuru sana kama hilo litakamilika.

Mheshimiwa Spika, pia namshukuru Mheshimiwa Waziri, *TARURA* wamejenga barabara kilomita 11 kutoka Vwawa kwenda Ndolezi. Palibakia kilomita 1.2 kwenye barabara ya *TANROAD* kufika kwenye kimondo chetu, naona amepeleka mkandarasi anajenga kile kipande, tunakushukuru sana. Kwa hiyo, ina maana sasa kimondo kile, barabara ikikamilika kitakuwa kimeongezewa thamani, tunashukuru sana kwa barabara ile.

Mheshimiwa Spika, tunaomba barabara ya kutoka Mahenge kuja hapo kwenye kimondo kwenda Hasamba – Nyimbili hadi Ileje kwa Naibu wake. Ile barabara ni muhimu sana katika maendeleo ya Mkoa wa Songwe. Ikikamilika itafungua njia, uchumi wa wananchi wa Ileje na wale wanaotoka Malawi na maeneo mengine watakatiza pale kuja mpaka Vwawa kuja Makao Makuu ya Mkoa na biashara zitaendelea vizuri sana. Kwa hiyo, hii barabara tunaona kwamba ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, ipo Barabara ya Ihanda kwenda Ipunga hadi Chindi. Ile barabara itaunganisha Wilaya ya Momba, barabara hii nayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi wa Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Spika, lipo eneo pale Iboya – Kata ya Ihanda. Eneo lile limetengwa kwa ajili ya kutengeneza *check point* ambapo eneo lilichukuliwa karibu miaka 10 sasa toka tunaimba. Wananchi wa eneo la Iboya wamekuwa kila wakati hawaendelezi lile eneo, wanasubiri fidia na kila mwaka tumeahidiwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi wananchi wanasikitika ni lini Serikali itawapa fidia wananchi wa Iboya ili ile *check point* ianze kujengwa tupunguze foleni iliyopo Tunduma? Hiyo ikikamilika, itasaidia sana kupunguza foleni ya pale Tunduma.

Mheshimiwa Waziri hebu lishughulikie hili suala wananchi wale wapewe fidia. Ni shilingi bilioni nne tu, na uhakika ukiongea vizuri na Wizara ya Fedha, wakalipwa, basi hali itakuwa ni nzuri na mambo yatakuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza pia *TANROADS* kwa kujenga *parking* ya malori pale Chimbuya karibu na Mpemba, ambapo *parking* ile itasaidia sana kupunguza changamoto ya usafiri pale Tunduma, ambayo ni kitu muhimu sana.

Mheshimiwa Waziri, naunga mkono hoja endelea kuchapa kazi, Naibu wako na Watendaji wote chapeni kazi, maendeleo ya nchi hii yanawategemea sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso na Mheshimiwa Ighondo Ramadhani, ajiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hii Wizara ya Ujenzi. Nianze kwa kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Hai kwa maafa ambayo yamejitokeza kwenye Jimbo letu la Hai. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu apokee taarifa kwamba kule Hai mvua zinazonyesha ni nyingi, miundombinu ya barabara imeharibika kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyozungumza, barabara ya kutoka kwa Mengi kwenda Kyalia haipitiki kabisa. Kwa hiyo, wananchi wanapata tabu. Barabara ya Makoa kwenda Mferejini kuna daraja pale Kikafu, kule watu wa Lyamungo hawawezi kwenda Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu atazame na hizi mvua zinaendelea kunyesha, zinanyesha kuanzia asubuhi mpaka jioni.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ninavyozungumza, kule Weruweru pale Miembeni barabara imekatika, watoto

hawajaenda shule leo. Karibu kama Kata nne watoto hawakuweza kufika shule. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hati ya dharura kabisa watusaidie michakato ya kutafuta fedha ianze mapema ili mvua zitakavyopungua tu hizi barabara ziweze kujengwa na watu wa Hai waweze kupata barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mara nyingi nimekuwa nikichangia hukuwepo kwenye Kiti, leo upo, nitumie nafasi hii pia kwa niaba ya wananchi na kwa niaba yangu binafsi, kukupongeza kwa kazi kubwa unayoifanya huko duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli unatuwakilisha vizuri sana. Niseme tu, huwa nakupenda na ninakufuatilia sana namna ambavyo unatuwakilisha vizuri. Inaonekana Watanzania na sisi tuna uwezo mkubwa, hongera sana. Nawaomba sana watu wa Mbeya, hiki kichwa hapa tunakihitaji hapa duniani na Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo niseme namshukuru Mheshimiwa Waziri, nimeona kwenye bajeti amenitendea haki. Alifanya ziara kwenye Mkoa wa Kilimanjaro na akaja Wilaya ya Hai, nampongeza ameanza vizuri pamoja na Naibu Waziri wake na watendaji wote, kwa kweli wanafanya kazi yao vizuri, ila kuna viporo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Daraja la Makoa limejengwa vizuri na *TANROAD,* lakini bado hawajamalizia na yule mkandarasi pale ameshalipwa, nimeambiwa hajamaliza ile kazi, lakini tayari wametangaza tenda ya daraja lile la Kikavu kutoka Kalali kwenda Uswaa mpaka sasa hivi mkandarasi hajaingia *site.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna kiporo kingine ambacho yeye mwenyewe alitembelea pale. Barabara ya Moshi – Arusha kwenye lile Daraja la Kikavu wananchi kila siku wanaenda kufundishwa mafunzo ya kulipwa fidia ili wapishe mradi. Naomba waongeze *speed* walipe wananchi wa Masama Kusini ili eneo lile la kwa Sadara waachie ujenzi wa daraja na waanze kazi ya ujenzi wa barabara hii ya Moshi – Arusha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwa Mheshimiwa Waziri wameweka kwenye mpango ujenzi wa barabara mbili, kupanua Barabara ya Moshi – Arusha, kuanzia Maili Sita kwenda Moshi Mjini. Naomba hebu waunganishe tufanye jambo likamilike pale Maili Sita ije mpaka Arusha. Mnaona sasa, hii baada ya Mheshimiwa Rais kutangaza *Royal Tour,* hii barabara imekuwa *busy* sana. Nawaomba mwongeze Mkandarasi, aliyeko *site* apewe hiyo kazi afike pale *KIA* kama itapendeza kwenda hadi Arusha sasa hilo ni jambo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina barabara hapa ya Bomang'ombe – Cheki Maji – *TPC,* hii barabara tumeipitisha kwenye kikao cha barabara mkoa, kwamba ni Barabara ya Mkoa wa Kilimanjaro kwa sababu ndiyo barabara pekee inayochepusha kwenda Moshi Mjini. Najua barabara hii ni ya *TARURA,* tulishaomba barabara hii ipandishwe hadhi ili iwe ya *TANROADS. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri hii barabara aiongezee fedha, pale tumepewa kilomita 3.5 ni ndogo mno kati ya kilomita 25 na sasa hivi likitokea matatizo pale Kikavu Chini hakuna sehemu ambayo tunaweza kupita na hii ni barabara ya Kitaifa maana inatuunganisha mkoa na mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri aliahidi yeye mwenyewe taa za barabarani. Kaka ehee, usiniangushe kwenye hili, ulilisema mwenyewe. Wanasema wako kwenye manunuzi tunataka tuone hizi barabara zetu pale kwa Sadala – Bomang'ombe, lakini na kile kipande Waziri anajua yaliyotokea pale kutoka Njia Panda - Machame kwenda Kyalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yakifanyika, kwa kweli watakuwa wametusaidia sana. Nimeona wametuwekea kwenye bajeti ku-*upgrade* barabara ya Kwasadala kwenda Kware kilomita 15. Naomba Waziri asukume hili, ujenzi uanze kwenda, hiki Kiswahili cha kuwaambia wananchi kwamba tuko kwenye upembuzi yakinifu, nimeshasema sana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA** Haya, ahsante sana.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, nibadilishie msemo ili nikaseme, lami inaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono bajeti hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso atafuatiwa na Mheshimiwa Ighondo Ramadhani na Mheshimiwa Seif Gulamali, ajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Sera ambayo ipo chini ya Wizara hii ambayo Waziri anaisimamia ni kuziunganisha barabara zetu kati mkoa na mkoa kwa kiwango cha lami, na sera hii Waziri anapaswa kuisimamia, lakini wananchi tunapaswa tuione kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni bahati mbaya sana sisi wananchi wa Wilaya ya Karatu hatujaiona hii, na siyo tu kuiona, pamoja na kwamba sera inaelekeza, lakini imekuwa ni ahadi ya viongozi. Tuna barabara kuu mbili muhimu ambayo ni Barabara ya Njia Panda – Mang'ola – Matala mpaka Lalago ambayo inaunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna barabara nyingine ya kutoka Karatu – Kilimapunda kwenda Mbulu. Hii ni barabara ambayo inaunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa Manyara. Ni barabara za muda mrefu. Tumesema hapa Bungeni na Wabunge waliopita wameongea, wametaka utekelezaji wa barabara hizi takribani miaka 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi, mwaka 2005 Mheshimiwa Dkt. Kikwete wakati anakuja kuomba kura alitoa ahadi mpaka leo mmewadanganya, mmewahadaa wananchi wa Karatu, barabara hii haijawahi kufikiriwa kutengenezwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi hii barabara ya kutoka Karatu kwenda Mbulu mwaka 2023 mkamleta mkandarasi, mkaja, mkasaini, mkasema barabara inaanza kwa kiwango cha lami. Mpaka ninapoongea sasa, kwa kweli hakuna chochote kilichofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, sasa atueleze kwa nini kwanza ametupiga *sound* muda mrefu kiasi hiki? Kwa nini ametudanganya? Kwa nini ameshindwa kusimamia sera yao wenyewe waliyojiwekea? Kwa nini wameshindwa kutekeleza ahadi za viongozi ambazo walizitoa kwa wananchi? Kwa nini wamewahadaa wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukapata haya majibu na kama hawawezi, watuambie kabisa kwamba hatuwezi na hatutajenga ili tujue kwamba sisi tupambane na hali yetu kwenye hizi barabara mbili ambazo tumezipigia kelele muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine tuna barabara ya kuelekea kwenye hospitali ya wilaya. Hospitali ya wilaya imejengwa vizuri ina kila kitu, lakini barabara ya kwenda pale takribani kilomita tatu mpaka nne ni mbovu na kipindi hiki cha masika hata *ambulance* ambayo inampeleka mgonjwa pale haiwezi kupita kama mvua zikiwa nyingi. Kuna daraja na mvua.

Mheshimiwa Spika, barabara hii pia tunaomba tupatiwe hizo kilomita kwa kiwango cha lami ili kile ambacho tumekijenga kule hospitali kutoa huduma kwa wananchi, kwa kweli wananchi waweze kupita kwa sababu uhakika wa barabara kupitika upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tuna barabara muhimu sana ambazo kwa sasa zinahudumiwa na *TARURA,* lakini wananchi wanaomba kwa uwezo wa *TARURA* kuhudumia zile barabara, haiwezekani. Tunaomba barabara hizi zitoke *TARURA* ziende kuhudumiwa na *TANROADS* na barabara hii ni barabara inayoanzia Rotia kwenda Mbulumbulu na nyingine inaanzia Manyara – Kibaoni kwenda Kata inaitwa Mbulumbulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii barabara ikifika Mbulumbulu inaenda kuunganisha Wilaya ya Karatu na Wilaya ya Monduli kwa sababu ikifunguliwa wananchi pia wanaweza kutumia hiyo barabara kuelekea Wilaya ya Monduli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni muhimu sana hii barabara pia ikapandishwa hadhi kwenda kuhudumiwa na *TANROADS* ili basi wananchi waweze kupita barabara hiyo kwa kipindi chote. Kipindi hiki cha masika ni kibaya mno. Jana walikuwa na msiba, watu wametoka na maiti Dar es Salaam wameshindwa kupita kwenda kuzika, yaani wameshindwa kabisa. Kuna adha, kuna shida kubwa sana kwenye hii barabara Mheshimiwa Waziri tunaomba ombi hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi, tuna barabara nyingine pia ambayo ni muhimu sana inapita Kata ya Endabash – Endamarariek – Endallah – Chemchem mpaka Manyara Kibaoni ambayo inaenda kuunga barabara hii kubwa ya kutoka Karatu kwenda Arusha. Tunaomba pia barabara hii itoke chini ya usimamizi wa *TARURA* iende kuhudumiwa na *TANROADS* ili iweze kuhudumiwa kwa viwango vinavyotakiwa na wananchi waweze kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, wananchi waliopisha upanuzi wa uwanja wa ndege wa Manyara mliwalipa fidia, lakini mliwaaidi mtawalipa riba ya fidia ambayo yalipaswa. Mpaka leo wananchi wale hawajalipwa, ni miaka karibia 30 mmeahidi, mmesema mmepokea, maombi yako Wizarani, sijui yameenda Wizara ya Fedha mpaka leo wananchi wanatamani kujua ni lini fidia hiyo italipwa kwa wananchi hawa ambao wamepisha upanuzi wa Uwanja wa Manyara – Kibaoni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ighondo Ramadhani atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Gulamali na Mheshimiwa Chaurembo Abdallah, ajiandae.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa nami niweze kutoa mchango wangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti hii muhimu ya ujenzi na nianze kwanza kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu kipenzi Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ameendelea kuwatumikia Watanzania kwa uzalendo mkubwa na kwa upendo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata juzi tarehe 1/5/2025 kujumuika na Wanasingida pamoja na Watanzania kwa ujumla katika kuadhimisha ile Siku ya Wafanyakazi, Wanasingida kwa kweli walifurahi sana kuwanaye siku ile na wewe nilikuona, hongera sana na karibu tena Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri sana na utendaji mzuri, pia ni msikivu Waziri wetu huyu wa Ujenzi pamoja na Naibu wake, kusema ukweli najivunia, kwa sababu mara kadhaa nimemfuata Mheshimiwa Waziri, hata juzi kabla ya bajeti tulinong'ona pale nje nikamwambia barabara yangu ile ya Ilongero isipoonekana patachimbika. Sasa kwa heshima kubwa sana nasimama hapa, nampongeza Waziri na Watendaji wake wote pamoja na Balozi Aisha, Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka miaka miwili 2023 mpaka 2024 iliyopita nilisimama hapa nikaongea mpaka na Kinyaturu kabisa. Sasa leo nakuja na mrejesho wa kusema *Mwajefya,* yaani ahsanteni sana kwa kuiona barabara ile ya Ilongero kutoka pale Singida Mjini – Igauri imeonekana kwamba sasa ujenzi utaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefurahi kuiona ile barabara kwenye kitabu cha bajeti sasa, kitu kikubwa hapa namwomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara ya Fedha, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu wahakikishe ujenzi unaanza mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipoona neno limeandikwa pale Singida – Igauri – Ilongero limeandikwa kwenye kitabu cha bajeti hata wananchi wenzangu pia nikawajulisha kule Ilongero. Maana yake wanaisubiri hii barabara kwa hamu sana kwa sababu ni barabara ya kimkakati, barabara ambayo ndiyo roho ya uchumi wao na maisha yao ya kila siku. Maana yake sasa hivi barabara ni mbaya sasa walivyoiona kwa kweli walifarijika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikubwa tu ambacho wanakisisitiza, wanataka waone mitambo ikiwa barabarani pale inatengeneza ile barabara ili nao wa-*enjoy* angalau waonje matunda ya uhuru ambao wazee wetu walimwaga damu kwa ajili yetu.

Mheshimiwa Spika, hapa hapa pia namshukuru Meneja wetu wa *TANROAD* Mkoa wa Singida *Eng.* Singano kwa jinsi ambavyo anatupa ushirikiano na amekuwa msikivu wakati wote. Kila tukifika tunalia anatusikia japo ni mgeni, lakini ameonyesha kwamba ni mwamba, amekomaa, ni msikivu kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sasa nisisitize mara mbili, tatu. Leo nimesimama kwa ajili ya hii barabara, yaani jambo kubwa ni hii barabara nataka nione kazi ikianza kufanyika. Leo sitaki kutumia maneno ya ukali, nilishayatumia sana huko nyuma kuhusu hii barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leo imesikika, nitoe ombi tu kwamba kazi ianze, na ninatarajia kabla ya bajeti hii kuanza kutekelezwa huko, hapa sasa hivi kuanzia Mheshimiwa Waziri atakapokamilisha, nataka nione kule vumbi likianza kutimka kwenye *site,* kazi ikifanyika wananchi wanaisubiri barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwaambia Wanasingida Kaskazini tuwe na subira, tusisikilize redio mbao. Leo mmeona barabara yetu iko kwenye bajeti, nyie tu sasa hivi mwombeeni Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan afya njema na mumpe mitano tena ili wakati tunapiga kura huku na barabara inapitika. Nina imani kubwa na Rais wetu kwa kuwa ametusikia hata utekelezaji wake utafanyika ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapo hapo ipo ile barabara ya kutoka pale Ilongero inapoishia hii kuelekea Ngamu inakounganisha na kule Mkoa wa Manyara, nayo tuliambiwa itaanza kufanyiwa *feasibility study*. Naomba *feasibility study* ifanyike na yenyewe iwekwe lami. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, sitaki kukuudhi. Naunga mkono hoja, barabara ya Ilongero – Singida kazi ianze kufanyika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Chaurembo na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu ajiandae.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi nami nichangie Wizara hii ya Ujenzi. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambazo ameendelea kuzifanya ndani ya Taifa letu hususan katika hii Sekta ya Ujenzi. Tumeona miradi yote mikubwa ambayo ilikuwa imeachwa, anaendelea kuipatia fedha kuweza kuhakikisha kwamba inakamilika. Hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kaka yetu Mheshimiwa Abdallah Ulega, Baba Tulia, kwa kupewa nafasi ya kuwa Waziri wa hii Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Waziri umepewa Wizara hii kubwa na ni nzito, lakini pia umezaa mtoto umempa jina la Spika wetu, Tulia Ackson. Hebu linda hadhi ya hilo jina, na hii Wizara yenyewe jinsi ilivyo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu, hapo awali hii Wizara alipewa Mheshimiwa Prof. Mbarawa. Mheshimiwa Prof. Mbarawa, wakati akiwa Waziri alituahidi sisi watu wa Manonga hususan Wilaya ya Igunga kutupa kilomita 10 za mwanzo kwenye barabara ya Choma – Ziba kwenda Nkinga mpaka pale Puge mwaka ule 2023/2024 wa bajeti na alisimama hapa mbele ya

Mheshimiwa Spika. Akasema kwamba, nawapa watu wa Manonga kilomita 10 pamoja na Mheshimiwa Dkt. Kigwangala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadaye Mheshimiwa Waziri akawa ameweza kuondoka, akaja Waziri mwingine anaitwa Mheshimiwa Bashungwa na yeye akasimama kwenye hiyo Wizara mwaka unaofuatia 2024/2025, tukamwambia barabara yetu tupe fedha. Yeye kwenye Wizara yake hiyo hiyo ya Ujenzi akasimama kwenye hili Bunge akatuahidi kwamba yeye atatupatia kilomita 10 kwenye hiyo barabara ya Choma – Ziba.

Mheshimiwa Spika, sisi tukajua sasa, maana yake 10 za Mheshimiwa Prof. Mbarawa, 10 za Mheshimiwa Bashungwa maana yake tunaenda kutengeneza kilometa 20 katika barabara yenye urefu wa kilometa 109.

Mheshimiwa Spika, namwona Mheshimiwa Waziri Bashungwa anatikisatikisa kichwa kwamba, haya zilikuwa ni kilometa 10 tu, lakini ndiyo barabara ile ina urefu wa kilometa 109. Sasa kama wewe unatupatia kilometa 10, halafu tena mkatupatia kilometa 10 mpaka tukamalize kilometa 109, itatumia miaka mingapi au bajeti hizi tutazipitisha ngapi humu Bungeni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri mwaka huu kwenye bajeti yake kwenye hii ameisoma vizuri sana, mwanzo mpaka mwisho. Sasa, yeye amefuta kilometa 10 za Mheshimiwa Prof. Mbarawa, na kilometa 10 za Mheshimiwa Bashungwa, amefuta zote na hakuna kitu.

Sasa, Mheshimiwa Waziri nataka katika *wind up* yako hapa utuambie sisi watu wa Igunga, je, wewe utatupatia kilometa 10 au umefuta zote kwamba, umefuta za Mheshimiwa Prof. Mbarawa na Mheshimiwa Bashungwa, na wewe kazi hapo imesimama?

Mheshimiwa Waziri tunataka majibu utakapokuja ku-*wind up* hapa. Usisahau, vinginevyo tutashika shilingi hapa kwamba zile kilometa 109 za ujenzi wa barabara ya lami Choma – Ziba mpaka

Puge kule kwa Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, unatupatia kilometa 10, kilometa 20 au zote kilometa 109? *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri utambue mmeshafanya usanifu, mmetangaza kazi na mmepata mkandarasi, mkatuambia sasa imebaki kazi ya kusaini. Sasa, kama kazi ya kusaini tulitegemea kwenye hii bajeti yako, utuambie fedha za utekelezaji wa barabara hiyo ni hizi hapa. Sasa, maana yake yule Mkandarasi mlikuwa mnazungumza naye kupatana bei, ina maana mmefuta au imekuwaje? Au zoezi hilo la kusaini limeishia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, huyu Mkandarasi ambaye mlikuwa mmempatia kazi na ambapo tuliambiwa sisi wananchi tutasaini mwezi wa kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu akaja mwezi wa tatu pale Igunga na Manonga na pia akaenda kwa Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, akasema kazi iliyobakia ni kusaini, kazi ya ujenzi wa barabara ianze. Sasa, Mkandarasi anasubiri tusaini, leo ni miezi sita hatujasaini. Leo tunataka sijui tushike shilingi Mheshimiwa Waziri? Maana yake kwa utaratibu huu sisi wananchi hawawezi kutuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu anategemewa katika Taifa hili awaambie wananchi wa Manonga na awahakikishie watu wa Igunga, aende na Nzega akawahakikishie watu wa Nzega na Puge kwamba tunachonga barabara hii.

Mheshimiwa Spika, tunaiamini Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inafanya kazi, na fedha inatoa. Tunaomba na sisi tupate fedha. Najua Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba anatakiwa naye atupatie fedha, lakini mwisho ninapomalizia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele imeshagonga.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mheshimiwa Godfrey Kasekenya Msongwe, ajiandae.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi. Pili, namshukuru sana Rais wetu, mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya. Tatu, nawashukuru Mawaziri wote waliohudumu katika Wizara hii katika kipindi hiki cha miaka mitano. Kwa kweli katika kipindi chote hiki cha miaka mitano, Mawaziri wote waliopitia Wizara hii wamenipatia ushirikiano mkubwa sana na ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Mbagala, sina deni na Wizara hii. Barabara zangu zinazoshughulikiwa na Wizara hii ni barabara mbili; barabara inayotoka Kokoto kwenda Kongowe – Mwandege. Mheshimiwa Rais amelipa fidia ambayo ilikuwa shida yetu kubwa ya shilingi 16,800,000,000. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, isitoshe, barabara hii sasa ina Mkandarasi na ameshaweka *camp* ya kuanza kujenga. Tunatarajia muda wowote kuanzia sasa ujenzi utaanza. Pia, nawashukuru, nilikuwa muda mrefu naipigia kelele barabara ya kutoka Mbande - Kisewe mpaka Msongola. Barabara ile imepata Mkandarasi na anaendelea na kazi, lakini hapa ndiyo kwenye tatizo.

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi yule sijui anataka tumfanye nini? Tunazo taarifa ameshapewa malipo yake, lakini kazi haziendelei, kwa nini? Leo hii amekwenda kutusababishia matatizo makubwa sana kwa watu wa Mtaa wa Kisewe. Maji yote ambayo yamekusanyika barabarani kutokana na kurundika vifusi yanatiririka sasa hivi kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, utakumbuka umefanya ziara katika barabara ile na tulikubaliana mpaka mwezi wa Tatu barabara iwe imeisha. Hebu tuombe sana huyu Mkandarasi mzungumze naye, wengine tukianza kuzungumza hapa na tukianza kumwachia Mwenyezi Mungu mambo haya, huyu mkandarasi atakuja kupata matatizo maishani mwake.

Tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri, unatufahamu sisi wengine karama yetu. Mwambie huyu Mkandarasi akasafishe vifusi vyake, aweke lami, amalize kazi. Wananchi wa Kisewe wanaathirika na ile barabara kwa sababu maji yote yanaenda katika mitaa ya watu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri, hebu afikirie hii barabara sasa inayotoka Rangi Tatu kuja mpaka Mbande. Barabara inayo lami, lakini barabara imezidiwa sana. *Population* ya Mbagala imekuwa kubwa mno. Kwa hiyo, tunahitaji barabra hii aiweke katika mchakato wa kuweza kuipanua na hatimaye iweze kuwa barabara ya njia nne au njia sita, ili mwendokasi sasa uweze kufika hadi Pugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, Mtoa hoja ajiandae.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. Nashukuru kwa kupata nafasi kuichangia hii Wizara yenye dhamana ya barabara zetu nchini. Kwanza, nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa miujiza aliyoifanya ndani ya Jimbo la Kibamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapatie pongezi sana Wizara wakiongozwa na ndugu yangu Mheshimiwa Ulega, Naibu Waziri Mheshimiwa Kasekenya na hawa Watendaji Wakuu wa Wizara; Balozi Mhandisi Aysha Salum Amour na Naibu Katibu Mkuu ndugu yangu Charles Msonde. Ninawapongeza sana, watendaji hawa, wameisaidia Wizara kwa kiasi ambacho kila Mbunge hapa anaona aseme hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, niongelee maeneo ya mafanikio zaidi kwenye bajeti hii. Kwanza, niishukuru sana Serikali kwa kutuondolea ile foleni kubwa kwenye Barabara ya Kitaifa ya Kimara – Kibaha kilometa 19.2. Nataka niseme ukweli, sisi watu wa pembezoni mwa Dar es Salaam tulikuwa tunatumia hadi saa saba

kutoka Kibamba kwenda Posta. Ikikukuta siku nyingine mnarudi kutoka ofisini mnafika saa nane za usiku. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kukamilisha hii barabara vizuri na tunamtarajia aje atuzindulie barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ziada ndani ya Jimbo; wananchi wengi wanajua na Waheshimiwa Wabunge kwa sababu wanapita ndani ya Jimbo la Kibamba. Nataka niseme ukweli kabisa ndani ya sakafu ya moyo wangu, leo barabara zimetajwa kwenye bajeti hii, kitabu hiki ndani ya *page* ya 36 aya ya 107, maeneo haya katika vitabu vya nyuma huko hatujazoea kuviona. Leo hii inatajwa Barabara ya Goba – Matosa – Temboni kilometa sita, Goba Njia Nne kuelekea Matosa hadi Saranga ambapo ni Temboni kilometa sita, tayari kilometa moja, bado kilometa tano. Kitabu kinatuambia kazi inaendelea, lakini hapa ninalo ombi.

Mheshimiwa Spika, hii kilometa moja ni miaka mitatu sasa, hizi kilometa tano hatumwoni Mkandarasi kama anatamkwa. Hivi anakuja, haji? Nawaomba sana, mkandarasi aende amalizie hizi kilometa tano ambazo tunahitaji ziishe.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ya pili Kibamba Shule – Mpiji Magohe. Tunashukuru sana, hii ni barabara kubwa, njia panda ya shule inaenda Mpiji Magohe inaelekea hadi Bunju, Barabara ya Kitaifa. Tayari ina zaidi ya kilometa saba na hata leo wakati natoka hii *weekend* nimewaacha wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishukuru sana Serikali na lami ni nzuri ya kiwango cha Kimataifa. Kwa hiyo, niendelee kuwashukuru sana, lakini barabara ya tatu inatajwa kwenye vitabu hivi ni Barabara ya Mbezi - Msakuzi – Makabe *Junction,* tayari kilometa 8.36 ina urefu huo na tayari inaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami kwa hatua mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, ziada ni hii Barabara ya Kimara – Bonyokwa – Kinyerezi ilikuwa ni tatizo la muda mrefu pale Darajani. Mimi niheshimu sana na nishukuru sana Wabunge wenzangu wote; dada yangu Mheshimiwa Bonnah kule mwisho Kinyerezi na kaka yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo hapo katikati na mwanzo ninaanza mimi. Barabara hii

sasa hivi imefikia 13% ina kilometa 6.73 na mkandarasi yupo *site*. Kwa hiyo, hizi ni pongezi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maombi yangu, ipo barabara inatamkwa humu ndani, Barabara ya *Victoria Road.* Viongozi wa Wizara mnaijua na ndiyo kilio changu kama Mbunge, kila mwaka ninaisema. Sasa hivi mliwahi kuitangaza mara mbili kilometa 9.55. Mara ya kwanza hawajatokea wakandarasi, hawajatosha, hawana sifa. Mara ya pili tena na sasa hivi mnazungumza mmeanza kilometa sita.

Mheshimiwa Spika, nataka nijue mkataba ulisainiwa lini na huyu mkandarasi anaingia lini? Hii barabara ni muhimu, ina wananchi zaidi ya 100,000. Barabara moja hii wanaita Mbezi Shule au Kwa Yusuph – Mpiji Magohe kilometa 9.55. Nawaomba sana Wizara kwa unyenyekevu mkubwa wampeleke mkandarasi aanze kazi kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni mafanikio makubwa sana ndani ya Jimbo la Kibamba. Hizi ni Barabara za *TANROADS* au Wakala wa Barabara Mijini. Hatujazungumza hayo mengine ya *TARURA* na *DMDP* huko, tumeshatoka kwenye Wizara nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mafanikio ni makubwa ndani ya Wizara hii na Mheshimiwa Rais ameshafanya makubwa sana katika Jimbo letu la Kibamba. Mwisho, niwatakie kila la heri Wizara, kazi wanayoifanya ni nzuri lakini niwatakie heri kwa sababu tunafanya mapato na matumizi. Basi wayapate haya mapato tunayoyatarajia kwenye hii bajeti ya 2025/2026, ili kazi sasa tuliyoitarajia kama Taifa iweze kwenda kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naiunga mkono hoja Wizara hii na ninamshukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ZULFA MMAKA OMAR:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunifikisha leo nikiwa mzima.

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoendelea nayo kwa kujenga nchi, kwa kweli Tanzania ya Mama Samia ni ya maendeleo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kuipongeza Serikali kwa kutoa fursa katika kampuni binafsi kuweza kuwekeza katika vivuko vya kwenda Kigamboni kwani jambo hili limesaidia sana kupunguza changamoto ya usafiri kwa wananchi wanaoishi huko na wale wanaoenda kwa matembezi. Pili, hili linaenda kuwashawishi wawekezaji kuweza kwenda kuwekeza huko bila ya hofu ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Rais kwa kuweza kujenga madaraja mbalimbali katika nchi yetu, kwani madaraja haya yanaunganisha watu kuweza kuvuka na kuvusha biashara mbalimbali kutoka nchini kwetu na kupeleka nchi Jirani. Pia nitoe pongezi kwa kumalizwa Daraja la Kigongo - Busisi kwani madaraja haya yatazidisha chachu ya maendeleo nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja hii.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa ni pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Abdallah Ulega, Mbunge na Waziri wa Ujenzi kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ushindani wa Kimataifa *(National competitiveness)*. Bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi chake akiwa Waziri wa Ujenzi, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno, kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miezi tisa ya bajeti inayoishia Aprili, 2025, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, imetekeleza miradi mingi ya miundombinu ya barabara, reli, bandari na uimarishaji wa safari za anga ikiwemo ujenzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa hatua nzuri za utekelezaji wa mradi wa kihistoria wa ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* pamoja na uboreshaji wa bandari utaimarisha kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi yetu. *SGR* na bandari ni nguzo imara ya kiushindani katika biashara ya usafirishaji wa ndani na nchi za Maziwa Makuu na hata za Kusini mwa Afrika na Kati. Bandari za Tanzania ni lango la usafirishaji kwa Zambia, Malawi, DR Congo, Uganda, Burundi, Rwanda, Sudan ya Kusini na hata Zimbabwe na Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi kubwa kuhakikisha ujenzi wa *SGR* unaendelea kwa kasi ile ile na pia napongeza jitihada za kuendelea kutafuta vyanzo vya fedha vya masharti nafuu kugharamia ujenzi huo. Pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa, Serikali imefanya maboresho makubwa ya miundombinu na huduma katika bandari zetu hususan Bandari ya Dar es Salaam ili kukabiliana na ushindani mkubwa wa bandari nyingine za ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Dar es Salaam inakumbana na ushindani mkubwa kutoka bandari za Mombasa (Kenya), Beira (Msumbiji), Nacala (Msumbiji), Durban (Afrika Kusini), Lobito (Angola) na *Walvis Bay* (Namibia). Ujenzi wa *SGR* ya bandarini na maboresho mengine ya bandari zetu iendane na kuondoa changamoto nyingine ambazo zinasababisha gharama kubwa za usafirishaji kwa bandari zetu na kusababisha kupoteza biashara ya usafirishaji kwa bandari shindani.

Mheshimiwa Spika, ufanisi wa bandari unategemea pia maboresho ya barabara, reli ya kati *(TRL),* reli ya *TAZARA,* utendaji wenye tija wa wadau wote wa bandari na hata watumishi ili kupunguza gharama za usafirishaji kwa wateja wa bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto za mfumuko wa bei za mafuta na pembejeo, kuna fursa kubwa na hasa mahitaji makubwa ya mazao ya kilimo kwa soko la ndani na nje. Uzalishaji kwa tija unategemea kwa kiasi kikubwa ubora wa miundombinu ya barabara, reli na hata anga. Serikali iweke msukumo zaidi kwenye kuboresha miundombinu ya barabara kurahisisha usafirishaji wa pembejeo na mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na fursa za uzalishaji mkubwa kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, napendekeza mwendelezo wa uboreshaji wa barabara za *Tanzam* kipande cha Igawa - Tunduma; barabara ya *bypass* ya Uyole - Songwe; barabara ya *bypass* ya Iwambi - Mbalizi; barabara ya Mbalizi – Shigamba – Isongole kutokana na uzalishaji wa mazao ya kilimo; barabara ya Mbalizi – Galula – Makongosi kutokana na uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo na madini; na pia barabara ya Isyonje – Kikondo – Makete ambayo ni muhimu sana katika kusafirisha mazao ya kilimo ikiwemo maua, parachichi na viazi kwa soko la nje.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa barabara hizi pamoja na Uwanja wa Ndege wa Songwe ni muhimu sana kwa usafirishaji wa mazao yetu kwa soko la ndani na nje, na kwa kiasi kikubwa utaongeza mapato ya fedha za kigeni. Maboresho ya Uwanja wa Ndege wa Songwe uende sambamba na ujenzi wa maghala mahususi ya maua, mbogamboga, parachichi, nyama, viwanda vya kuongeza thamani za mazao na madini na *EPZ/Industrial Park.*

Mheshimiwa Spika, kutokana na ajali za mara kwa mara za Mlima Iwambi Mbalizi na msongamano wa magari yakiwemo malori ya mizigo na mafuta ya petroli, tunashukuru kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchukua hatua za haraka kuanza ujenzi wa barabara ya njia nne kwa barabara ya *Tanzam* kipande cha Uyole mpaka Uwanja wa Ndege wa Songwe.

Mheshimiwa Spika, katika vipindi mbalimbali, viongozi wa Kitaifa waliagiza upanuzi wa kipande hiki cha *Tanzam* pamoja na ujenzi wa *bypass* ya Uyole – Songwe kilometa 40 na *bypass* ya Mbalizi – Iwambi kilometa 6.5.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara hizi utanusuru wananchi kuendelea kupoteza maisha kwa ajali za mara kwa mara katika eneo hilo. Hatari zaidi ni kwa magari makubwa yanayosafirisha mafuta kupita barabara yenye msongamano mkubwa katikati ya Jiji la Mbeya. Msongamano wa magari makubwa katika barabara ya *Tanzam* ni sehemu ya changamoto zinazopelekea bandari zetu kupoteza biashara kwa bandari shindani.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu sasa, wananchi waliopisha ujenzi wa barabara ya *bypass* ya Uyole mpaka Songwe wamekuwa wakipewa ahadi ya malipo ya fidia, lakini mpaka leo hii hawajalipwa. Naishauri Serikali ichukue hatua za haraka kuwalipa madai ya fidia kabla ya kuanza utekelezaji wa bajeti ya ujenzi ya mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuongezea mchango wangu wa kuzungumza nikianza na *TBA;* nawapongeza kwa kazi kubwa wanazofanya, lakini naomba Mradi wa Temeke Mwisho utengewe fedha na ukamilike.

Mheshimiwa Spika, Temeke ni Wilaya ambayo hakuna nyumba nyingi za watumishi, hivyo tunatamani kuona nyumba zile zimekamilika. Rai yangu pamoja na juhudi za Serikali za kutafuta sekta binafsi kuungana na *TBA,* lakini wasitupandishie gharama za nyumba kwa kuwa mara nyingi sekta binafsi wanaangalia faida zaidi bila kujali hali za wananchi wetu/watumishi wetu.

Mheshimiwa Spika, ndani ya mradi wa ujenzi wa nyumba za *TBA* kuna Shule ya Msingi Mji Mpya ambayo ina mazingira magumu sana, haiwezi kuendelezwa, je, Serikali hawaoni umuhimu wa kusaidia kuendeleza shule hiyo kama sehemu ya mradi huo? Kwa sababu watakaokuja kuishi pale nao watakuwa na familia zao.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, mara kadhaa nimeiomba Serikali kupitia upya madai ya wananchi waliopisha ujenzi wa Barabara ya Bunda kwenda Kisorya, kwani baadhi ya wananchi wanadai kuwa bado hawajalipwa fidia zao. Naiomba Serikali kupitia bajeti ya mwaka huu wa 2025 iwalipe wananchi hao stahili zao.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano ya usafiri kati ya Visiwa vya Nafuba, Sozia, Nyamuguma, Machwela na Buyanza ni changamoto kubwa sana kwa wananchi. Naiomba Serikali ivipatie kivuko visiwa hivi.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, hali ya barabara kutoka Njombe kwenda Ludewa ni mbaya sana, zaidi ya mwaka sasa mkandarasi hajarudi *site*. Sehemu ya Lusitu - Njombe *spring* za magari zitaharibika sana, bodi za magari zinalegea sana, matumizi ya mafuta ya magari yameongezeka na kuongoza gharama za uendeshaji na masaa mengi yanatumika kusafiri kwenye eneo lisilo na umbali mrefu.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na kuendelea kuwawakilisha vizuri wananchi wa Hanang hapa Bungeni. Pia nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Hanang kwa kuendelea kuniunga mkono kwenye kazi zangu za kuwawakilisha Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hii ni bajeti ya tano nikiisemea barabara ya Haydom kwenda Mogitu kilometa 68. Nashukuru sana kuwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika, kinachonishangaza kwenye bajeti hii ya mwaka 2025/2026 Waziri wa Ujenzi ameandika tu kuwa Serikali inaendelea kutafuta fedha wakati wananchi waliahidiwa ujenzi wa barabara. Rejea ukurasa wa 31 sehemu ya 93 ya hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi ukurasa wa 192 wa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi Kasma 4114 eneo la Mogitu - Haydom imetengewa kiasi cha shilingi milioni 500 kwa kilometa 68 wakati maeneo mengine ya barabara hii ya Serengeti *bypass* zimetengewa fedha nyingi mfano Mbulu - Garbabi kilometa 25

shilingi milioni 2,000, Labay - Haydom kilometa 25 shilingi milioni 2,000 na Nkoma - Lalago kilometa 65 shilingi milioni 2,500.

Mheshimiwa Spika, je, eneo lenye urefu wa kilometa 68 kutengewa fedha kidogo kiasi hiki, ni kwamba sehemu hii ambayo inagusa zaidi wananchi wa Hanang umuhimu wake ni mdogo na Wanahanang siyo muhimu kama wananchi wa maeneo mengine?

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni ujenzi wa barabara ya Nangwa - Gisambalang hadi Kondoa kwa kiwango cha lami ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo ina daraja lililokatika, daraja la Munguri toka mwaka 2019 na hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri awaeleze wananchi wa Hanang na Kondoa kuwa je, lini kwanza, Daraja la Munguri ambalo linategemewa kwa shughuli za kiuchumi na kijami na wananchi wa Hanang hasa Kata za Nangwa, Wareta, Dirma, Sirop, Simbay, Lalaji, Balangdalalu na Gisambalang wanazozitegemea upande wa Mkoa wa Dodoma ambao ni makao makuu ya nchi itajengwa?

Pili, ujenzi wa Barabara ya Nangwa – Gisambalang - Kondoa utaanza. Jambo la tatu, Barabara ya Arusha -Singida hasa eneo la Dareda mpaka Gehendu ambayo ipo Wilayani Hanang imekuwa mashimo matupu. Naomba ukarabati wa haraka ukafanyike ili kuondoa kero na adha wanazopata watumiaji wa barabara hii hasa Wanahanang.

Mheshimiwa Spika, kazi ya ukarabati wa barabara hii ufanyike kwa dharura, kwani kwenye bajeti ya mwaka 2024/2025 ilishatengewa fedha za kurekebisha kilometa sita.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja iliyoko Mezani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali, pamoja na kazi kubwa ambayo Serikali imefanya katika kuunganisha miundombinu ya barabara mkoa kwa mkoa na wilaya kwa wilaya katika mikoa mingi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali ikamilishe miradi ambayo haijakamilika kwa muda mrefu. Changamoto kubwa ni kuwa wakandarasi wanapewa kazi na pesa hazitolewi kwa wakati. Naomba nitolee mfano barabara chache za Mkoa wa Mwanza ambazo moja ni ya tangu mwaka 2017 hadi leo kilometa 18.2 ambayo ina miaka tisa haijakamilika.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Barabara ya Nyakato *VETA* - Buswelu - *Igombe TX* kilometa 18.2 tangu mwaka 2017 haijakamilika (Wilaya ya Ilemela). Pili, Barabara ya *Airport* - Igombe - Kayenze - Nyanguge kilometa 46 (ujenzi kilometa 10 na haujaanza tangu mwaka 2023/2024 (Wilaya ya Ilemela); na tatu, Isangula (Magu) - Ngudu (Kwimba) kilometa 50 (ujenzi kilometa 10).

Mheshimiwa Spika, nne, Mwamanga - Misasi - Salawe (Wilaya ya Misungwi) - Kahama (Wilaya ya Kahama Mkoa wa Shinyanga) kilometa 150 (ujenzi kilometa tatu); tano, Ngudu - Jojilo - Mabuki (Wilaya ya Kwimba) kilometa 28 (ujenzi kilometa tatu); sita, Kamanga - Katunguru - Sengerema (Wilaya ya Sengerema) kilometa 32 (ujenzi kilometa tatu); saba, Bukoba - Nyakalilo kilometa 7.8 (ujenzi kilometa tatu); na nane, Nansio - Rugenzi kilometa 11 (ujenzi kilometa saba).

Mheshimiwa Spika, barabara ya pili hadi ya nane zabuni zake ni tangu mwaka 2023/2024, lakini kazi bado hazijafanyika. Aidha, kilometa zinazopangwa kujengwa, kwa nini ni kilometa chache tu zinapangwa kujengwa na bado hazijengwi?

Mheshimiwa Spika, hoja yangu kwa Serikali, kilometa ni chache sana ambako barabara hizi zimeelekezwa ujenzi ukamilike kabla haijatoa zabuni nyingine ili kumaliza hivi viporo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa kusisitiza ukamilishaji wa barabara hizi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Abdallah Ulega na Naibu wake Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya, watendaji wote walio chini ya Wizara hii kwa kazi kubwa wanazofanya kwenye kutengeneza mitandao ya barabara na madaraja maeneo mbalimbali nchini. Kipekee naipongeza *TANROADS* Mkoa wa Kilimanjaro wakiongozwa na Mhandisi Palimaka Mota kwa ushirikiano wao mkubwa na Mbunge.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utahusu changamoto za barabara zinazojengwa na *TANROADS* katika jimbo langu la Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Moshi Vijijini liko katika maeneo ambayo wananchi wengi wanajishughulisha na shughuli za kilimo cha kahawa, ndizi, pamoja na mboga mboga na matunda ya aina mbalimbali. Vilevile wanajishughulisha na ufugaji pamoja na biashara na miji mbalimbali, ukiwemo Mji wa Moshi.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha shughuli za wananchi wa jimbo langu, uwepo wa barabara zinazopitika muda wote ni jambo muhimu sana. Ni kwa mantiki hiyo, naiomba Serikali itekeleze ahadi yake ya ujenzi wa barabara zinazojengwa na *TANROADS* ili ziweze kupitika kipindi chote cha mwaka na kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji wa mazao na kuchochea ukuaji wa uchumi wa wana Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, barabara ya *Kibosho Shine* - Kwa Raphael - *International School* iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi toka mwaka 2005 na inajengwa na *TANROADS,* ila haijakamilika. Mkataba uliopo sasa hivi unaonesha kwamba ujenzi wa barabara hii unatakiwa kukamilika mwezi Novemba, 2025.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itenge fedha za kutosha na kukamilisha ujenzi wa barabara hii kwani umechukua zaidi ya miaka 14.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa kuanza ujenzi wa barabara ya Kiboriloni - Tsuduni - Kidia kwa kiwango cha lami. Barabara hii inajengwa na *TANROADS* na bado haijakamilika.

Bado kuna malalamiko kutoka kwa wananchi wanaoitumia hii barabara kwamba kasi ya ujenzi ni ndogo na mkandarasi hajaonekana *site* kwa muda mrefu, ujenzi umelegalega.

Mheshimiwa Spika, kuna sehemu mbaya sana kwenye barabara hii na wananchi wanailaumu sana Serikali. Naiomba Serikali itenge kiasi cha fedha za kutosha na kukamilisha ujenzi wa barabara ya Kiboriloni - Kikarara - Tsuduni - Kidia kwa kiwango cha lami, kwani wananchi wanalalamika sana.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni ya kimkakati, kwani itatumika kuwasafirisha watalii wanaopanda Mlima Kilimanjaro kupitia lango la Kidia ambalo linatumiwa na watu mashuhuri *(VIP)*. Barabara hii imetengewa shilingi milioni 900 katika bajeti ya mwaka 2025/2026 kufanya marekebisho ili iweze kupitika. Naiomba Serikali itenge kiasi cha fedha za kutosha na kukamilisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Rau - Uru - Shimbwe yenye urefu wa zaidi ya kilometa 13 ilikuwa kwenye ahadi za viongozi wa Kitaifa kujengwa kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara hii umeanza kwa kasi ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto ya ujenzi wa barabara hii kutokana na kupangiwa bajeti finyu kila mwaka. Ubovu wa barabara hii unasababishia usumbufu na gharama kubwa za usafiri kwa wananchi wanaoishi huko milimani.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itenge fedha za kutosha na kukamilisha ujenzi wa barabara ya Rau - Uru - Shimbwe kama wananchi walivyoahidiwa na viongozi wakuu wa Serikali kwa nyakati tofauti, kwani ahadi ni deni.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Uru - Kishumundu - Materuni inajengwa kwa kiwango cha lami. *TANROADS* inajenga barabara hii kwa niaba ya *TARURA*. Kero kubwa ni kwamba kasi ya ujenzi ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itenge fedha za kutosha na kukamilisha ujenzi wa barabara ya Uru - Kishumundu - Materuni

kwani ina mchango mkubwa kupeleka watalii *Materuni Water Falls.*

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Moshi Vijijini, barabara ya Kwa Rafaeli - Mto Sere inaunganisha Wilaya ya Moshi na ya Hai. Barabara hii inahudumiwa na *TANROADS* ambapo wameshaweka mitaro katika baadhi ya maeneo na haijajengwa hata kidogo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni muhimu kwani ni sehemu ya kusafirisha watalii wanaokwenda kupanda Mlima Kilimanjaro kupitia njia na mlango wa Umbwe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maagizo ya Waziri kwa *TANROADS* kuhusu kuzingatia ubora na viwango vya barabara wanazozijenga, ombi langu kwake ni kwamba asiishie kutoa maagizo tu, bali aje *site* mwenyewe katika Jimbo la Moshi Vijijini ajionee kazi zinavyotekelezwa na kutoa maelekezo.

Mheshimiwa Spika, baada ya ushauri niliotoa hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutuletea miradi mingi katika jimbo letu la Lushoto. Wananchi wa Lushoto wanaendelea kumwombea dua na Mwenyezi Mungu ampe siha na afya njema ili aendelee kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Lushoto lina kilometa 52 ambazo zinahudumiwa na *TANROADS* na kilometa zote 52 ni za changarawe na barabara hizi zina changamoto hasa wakati wa mvua zimekuwa hazipitiki na barabara hii kila mwaka ninaisemea. Kwa hiyo, naiomba Serikali katika kipindi hiki cha bajeti iweze kupatiwa bajeti ili zianzwe kutengenezwa kwa kiwango cha lami. Kilometa 34 zimeanzia Mkuzi hadi Mlola na kilometa 18 zimeanzia Nyasa kupitia Gare hadi Magamba.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iniangalie kwa jicho la kipekee na la huruma iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, Naibu wa Ujenzi, Mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anazoendelea kuzifanya katika nchi hii. Pia, namshukuru kwa kuendelea kuniamini katika nafasi hii ya Unaibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi. Pia, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nikushukuru wewe mwenyewe, Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti kwa jinsi ambavyo mmekuwa mnaliendesha hili Bunge kwa umaridadi na kwa kweli kwa hali ambayo ni ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, pia, niishukuru sana Kamati ya Miundombinu chini ya Mheshimiwa Selemani Kakoso, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kwa jinsi ambavyo wamekuwa wanatoa maelekezo na kutoa ushauri kwa Wizara.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge siyo tu kwa kuchangia hoja, lakini kwa jinsi ambavyo mmekuwa mnatoa ushauri kila inapobidi lakini sana sana kwa hoja mbalimbali ambazo mmezitoa leo wakati tukiwa tunajadili hii bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Ileje kwa ushirikiano mkubwa ambao wananipatia bila kuisahau familia yangu pia kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia na kunipatia huu utulivu ambao ninao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitakuwa na mambo machache na ninaamini Mheshimiwa Waziri ataongea zaidi, lakini mimi nitajikita zaidi kuelezea yale mambo ambayo tumeyafanya katika kipindi hiki na yale machache ambayo tunategemea kuyafanya. Kwa

sababu ya michango mingi, sitataja majina lakini pia itakuwa ni vigumu sana kugusa kila Mbunge alichochangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwamba tunaamini moja ya kipimo cha maendeleo yoyote ya nchi pia ni miundombinu ikiwemo barabara. Pia, tunaamini ukiwa na barabara bora maana yake unapunguza gharama, muda, unachochea uchumi, unarahisisha kusafirisha, pia unafanya watu waweze kuwasiliana, na unaimarisha pia huduma mbalimbali za kijamii. Pia, unakuwa na uwezo wa kuunganisha eneo na eneo ikiwa ni pamoja na kusafirisha bidhaa kutoka eneo moja kwenda lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara ya Ujenzi, Ilani ya Chama cha Mapinduzi pia ni sera kwamba tuna wajibu mkubwa wa kuunganisha mikoa na mikoa, miji na miji, na pia kuunganisha nchi na nchi. Sasa, ni kuunganisha Makao Makuu ya Wilaya na Makao Makuu ya Mikoa yetu.

Mheshimiwa Spika, pia, tunahangaika sana na barabara zile za kimkakati ambazo tuna hakika tukizijenga zitainua uchumi bila kusahau barabara za mipakani na barabara za ulinzi. Kwa sababu hiyo, ndiyo maana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, moja ya eneo ambalo amelitilia mkazo sana ni kuhakikisha kwamba anaifungua nchi na kuiunganisha nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaona katika kipindi hiki tumeweza kuunganisha Tanzania na Malawi kupitia Mpemba kwenda Isongole. Sasa hivi tunajenga barabara ya kutoka Mpanda kwenda Kalemie ikiwa ni kuunganisha na *DRC*. Pia, tunajenga barabara ya kutoka Sumbawanga – Matai kwenda Kasesya kuunganisha na Zambia. Pia, sasa hivi tunafanya ukarabati mkubwa sana wa barabara *ET3* ambayo ni ya kutoka Lusahunga kwenda Rusumo ambayo ilkuwa imekufa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima niwahakikishie wananchi wa Tanzania na Waheshimiwa Wabunge kwamba, kama Wizara kazi hiyo tunaendelea kuifanya na tunaifanya kwa umakini mkubwa sana. Waheshimiwa Wabunge, wameongelea

matatizo mbalimbali kuhusu barabara zao, lakini nataka niwaambie kwamba katika kipindi hiki cha awamu hii tuna barabara nyingi sana ambazo tumezijenga na kwa sababu ukishapata, basi hiyo inakuwa siyo ajenda, ajenda ni kitu ambacho unakihitaji.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi watu hatuongelei tu kupitika kwa barabara, maana yake ni ya lami. Zipo barabara ambazo tumezikamilisha katika kipindi hiki ama tunaendelea kuzijenga. Tuna barabara ya Mnivata – Tandahimba kwenda Masasi ipo inajengwa kilometa 160.

Mheshimiwa Spika, tumekamilisha barabara ya Mbinga kwenda *Mbamba Bay* katika kipindi hiki ambayo pia inaunganisha Mkoa wa Ruvuma na Ziwa Nyasa kwenda Malawi. Tumejenga Lusitu – Mawengi, barabara ya zege. Tumejenga Tabora – Koga – Mpanda moja ya barabara ya mfano kabisa kilometa zaidi ya 350. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumejenga Kaliua – Nguruka ikiwa ni pamoja na kuunganisha na Mkoa wa Kigoma, lakini sasa hivi tunakamilisha kipande cha Malagarasi – Uvinza ili tuunganishe 100% kwenda Kigoma. Tumekamilisha Vikonge – Luhafwe kule Mpanda. Sasa hivi kutoka Kigoma hadi Mwanza unatembea kwa lami kilometa 260 ambazo tunazikamilisha na kwa sasa unatembea kwenye lami katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, tumekamilisha barabara ya kuunganisha na Daraja la Kitengule ikiwa ni pamoja na Daraja la Kitengule. Tumejenga Barabara ya Chaya – Nyahua, kwa hiyo, kutoka Manyoni kwenda Tabora zile kilometa ambazo zilikuwepo pale sasa hivi vumbi tumeshaliondoa katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, Makutano Sanzate tumejenga. Pia tumejenga Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Bulamba katika kipindi hiki. Waso – Sare tumekamilisha, Dumila – Kilosa tumekamilisha, Kidatu – Ifakara tumekamilisha, *list* ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kazi zimefanyika nyingi hatuwezi tukataja zote. Pia kwa sababu tunajua ili ufanye biashara na shughuli za kijamii hasa kwenye miji lazima upunguze msongamano. Katika miji hasa, nianze na Mji huu wa Dodoma, tunapoongea sasa hivi *outer ring road* yenye kilometa 112.3 ipo 84%, zaidi ya kilometa 70 au 75 zimeshawekwa lami. Itakuwa ni barabara ya aina yake ambayo tunategemea ifikapo mwezi Agosti, itakuwa imekamilika.

Mheshimiwa Spika, hii ni barabara ambayo itakuwa na taa kote kilometa 112 pia itapandwa miti barabara yote na upana wake ni zaidi ya mita 150, ambapo kutakuwa na maeneo mengi sana ya kufanya shughuli mbalimbali za kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kutoka katikati ya Mji ambapo sasa hivi tupo kwenye manunuzi, kutoka katikati ya Mji kutakuwa na njia nne ambazo zinaunga barabara ya kwenda Iringa, barabara ya kwenda Arusha, barabara ya kwenda Dar es Salaam na barabara ya kwenda Singida. Hiyo ni mipango ambayo tunaifanya ili Dodoma hii kusijekutokea changamoto.

Mheshimiwa Spika, unapokwenda Jiji la Mbeya tunaendelea na ujenzi wa njia nne kutoka Nsalaga – Ifisi – *Airport*, Mkandarasi yuko *site*. Barabara ile imeelemewa, nguvu kubwa ya Wizara sasa hivi ni kuhakikisha kwamba tunaifungua.

Mheshimiwa Spika, unaposikia changamoto ya Tunduma mabasi, Mbeya inawezekana ikawa ni mara mbili kwa sababu unaweza ukatumia zaidi ya saa mbili. Kwa kweli nguvu zote tumeweka kuhakikisha kwamba zile barabara zinakamilika ili kupunguza changamoto ya usafiri pale Mbeya.

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam tunaendelea na *BRT, BRT one* na *two* zimekamilika, *three* iko mwishoni, *four* inajengwa, na *five* ambayo inaanza Ubungo – Buguruni hadi Kurasini; pia Matumbi – Tabata Dampo – Kigogo, Matumbi – Kinyerezi, upande wa Kinyerezi; lakini nyuma hapa Segerea, ziko kwenye hatua za manunuzi. Zote hizo ni kazi kubwa ambazo Mheshimiwa Rais anataka kufungua, kuunganisha na kurahisisha shughuli za kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda Jiji la Mwanza, tunavyoongea tuko kwenye hatua za manunuzi kuhakikisha kwamba tunajenga barabara ya njia nne kutoka Mwanza katikati – Mkuyuni – Nyegezi – Mkolani – Buhongwa – Nyashishi – Usagara, itakuwa ni njia nne ambazo hizo zitakuja kuunganisha sasa na Daraja la Kigongo – Busisi, maarufu kama Daraja la Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Daraja la Kigongo – Busisi ama JPM ninadhani limeelezewa na watu wengi na Waziri atalielezea lakini ni daraja la aina yake kama walivyoliongelea, nasi tukiwa kama sehemu ya mafanikio hayo tuna kila sababu ya kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye wakati anapokea hiyo kazi lilikuwa siyo zaidi ya 25%. Tunavyoongea sasa hivi, anasubiriwa yeye akalifugue hilo daraja. Ni kazi ambayo katika Afrika Mashariki na Kati haipo, kwa hiyo ni kati ya vitu ambavyo Watanzania tunasema tunayo miradi ya kielelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nigusie suala la viwanja vya ndege. Tunajenga kiwanja cha ndege kikubwa sana cha Msalato, ambacho wanasema ni *State of the Art*. Kitakuwa kama viwanja vyovyote. *Plan* yake ni kwamba, kadri mji utakavyokuwa unapanuka, wameweka utaratibu kwamba *design* itakuwa kila Mji unavyopanuka na mahitaji yanaongezeka, ule uwanja utakuwa unaongezeka kadri mahitaji yanavyoongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunavyoongea sasa hivi tuko zaidi ya 85% kwenye *runway*, 55% kwenye hizi *facility* nyingine za viwanja. Ule uwanja utaunganishwa na barabara ambayo itatoka *Airport* Msalato – Ofisi za Mtumba – Chamwino Ikulu. Kwa maana kwamba hakutakuwa tena na sababu ya foleni pale ambapo viongozi wanaokwenda Chamwino Ikulu ama Mtumba kuingiliana na barabara nyingine hizi. Kwa hiyo, unaweza ukaona hiyo mipango ambayo ni mipango ya kisasa kabisa tunayokwenda kuifanya.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kwenye viwanja vya ndege, Uwanja wa Ndege wa Mbeya umekamilika, uwanja ambao sasa hivi ni maarufu sana. Uwanja wa Songea umekamilika, Uwanja wa Mtwara na hivi vimekamilika katika

kipindi hiki. Uwanja wa Mtwara umekamilika, tunajenga uwanja wa Sumbawanga, tunajenga Uwanja wa Tabora, tunajenga Uwanja wa Shinyanga, tunajenga Uwanja wa Musoma, na sasa hivi tunahamia *Lake* Manyara na Tanga. Mheshimiwa Waziri ataelezea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Wizara tumejipanga na tunategemea kwamba yale yote ambayo tumeahidi kwenye bajeti tutayatekeleza. Yale ambayo tutashindwa kuyajibu kwa mdomo, basi mtegemee kwamba tutawaletea kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Waziri wa ujenzi, aje ahitimishe hoja yake. Mheshimiwa Waziri karibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema na Mwingi wa Ukarimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru pia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani yake kwangu na kwa timu yangu yote ambayo amenikabidhi nishirikiane nayo katika Wizara ya Ujenzi katika kulijenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pia, naiomba nikushukuru wewe, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Kamati yetu ya Bunge kwa namna ambavyo mmekuwa mkitushauri na kutusimamia kwenye utekelezaji wa kazi mbalimbali za ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pia, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa mdomo na wale ambao wamechangia kwa maandishi. Jumla ya Wabunge 81 wamechangia hoja yetu. Ahsanteni sana kwa namna ambavyo mmetupa changamoto kubwa sana, na

mmetushukuru mkatupongeza, vilevile mmetupa ushauri mbalimbali wa namna ya kuyaendea mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishatangulia kusema, hoja ni nyingi sana za Waheshimiwa Wabunge na ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe kwa namna ya utangulizi aliyoanza nayo. Amesema vema kwamba, wale ambao tutakuwa tumewajibu hapa na wale ambao hawatakuwa wameyasikia majina yao wajue tu hoja zao tutazijibu zote hata kwa maandishi. Kwa hiyo, tutahakikisha kila hoja ya kila Mbunge iliyozungumzwa katika Bunge hili tunaipa uzito wake unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mazungumzo yaliyopita leo na jana hapa Bungeni, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia pia juu ya kuomba kupandishwa hadhi kwa barabara. Hapa wapo Wabunge wengi waliosema, lakini naomba niwataje wachache na niwaelekeze wataalam wangu na kwa sababu utaratibu wa upandishaji hadhi barabara unajumuisha kufanya tathmini na ipo Kamati ya Kiserikali ambayo yenyewe hushughulika na kuangalia vile vigezo.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, nawaagiza wataalam wangu hapa ya kwamba wazichukue hizi barabara zote zilizosemwa na Waheshimiwa Wabunge hapa ndani. Mfano barabara zimesemwa kuanzia jana na Mheshimiwa Njalu Silanga, Mbunge wa Itilima, Mheshimiwa Edwin Swalle, Mheshimwia Emmanuel Cherehani Mbunge wa Ushetu, Mheshimiwa Boniventura Kiswaga wa Magu, Mheshimiwa Flatei Massay, Mheshimiwa Phillipo Mulugo na Mheshimiwa Dkt. Ritta E. Kabati.

Mheshimiwa Spika, wote hawa katika jumla ya Waheshimiwa Wabunge waliosema juu ya barabara katika maeneo mbalimbali nchini, Ninataka niwahakikishie, tunakwenda kulifanyia kazi jambo hili na tutayapata majibu ikiwezekana kabla Bunge hili halijafika mwisho wake. Nina imani kwamba tutakuwa tumepata majawabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wabunge pia wamezungumzia juu ya jambo linalohusu *advance payments*

(malipo ya awali) kwa wakandarasi. Hapa wako wa namna mbili, wako wakandarasi wamelipwa fedha, lakini hazijafika kiwango cha 15% na wako wakandarasi hawajalipwa kabisa. Naomba nitoe mfano wa baadhi ya maeneo na ninaomba, katika kesi hii wako Wabunge wawili ambao wameniambia kuwa watashika Shilingi. Nawaomba kwa heshima kubwa na taadhima wasishike Shilingi.

Mheshimiwa Spika, rafiki yangu *Comrade* Mheshimiwa Kunambi, Mbunge wa Mlimba, yeye anazungumzia barabara ya kutoka Ifakara – Chita – Mlimba – Madeke, kwa sababu barabara hii, mmoja katika wakandarasi amelipwa kiwango, lakini hakijafika kile ambacho anapaswa kulipwa cha *advance payment*, na mwingine hajalipwa kabisa. Kwa hiyo, hakuna kinachoendelea katika eneo lile, shughuli zote zimesimama.

Mheshimiwa Spika, vilevile amezungumzia juu ya mambo yanayoendelea, ukweli ni kwamba eneo la Morogoro hasa Wilaya ya Malinyi ambako jana Mheshimiwa Antipas alichangia, Ifakara na Ulanga ni maeneo ambao yamepigika sana hasa na hizi mvua.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia tu Mheshimiwa Kunambi, eneo la Mpanga ambalo umetolea mfano wa msiba uliotokea pale ni kwamba hizi tunavyozungumza tayari wataalam wetu wamerejesha mawasilino. Tayari tumejenga eneo lile la dharura, tumeweka ma-*culvert* 15 ya chuma ambayo yatatosheleza kupitisha maji, tayari tumeshatengeneza tuta na kwa hiyo, sasa hivi watu wanaweza kupita.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kuendelea pale ni kwamba tunajenga *box culverts* ambazo zina jumla ya midomo sita. Kwa hiyo, tatu mara mbili tutakuwa tumejenga pale na itatosheleza kwa *study* tuliyoifanya na tunaifanya hiyo mara tu baada ya kutokushika shilingi na kuturuhusu bajeti hii ipite na tunakwenda kuifanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana na hili suala la Ifakara – Chita – Mlimba – Madeke, miongoni mwa fedha zitakazopatikana za *advance payment*, tumeshaandika barua

tumeipeleka upande wa wenzetu wa Wizara ya Fedha nao wanatupa ushirikiano mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu hapa Mlimba kwa maana ya Ifakara – Chita, vilevile na barabara ya kutoka Bigwa – Kisaki kule ambako Mheshimiwa Tale na Mheshimiwa Innocent Kalogeris wamepazungumza kwa uzito sana ndani ya Mkoa wa Morogoro na zenyewe tunakwenda kuzipa kipaumbele haraka sana baara ya kuwa tumeipata fedha ya *advance payment*. Tutakwenda kuwaondolea shida hii.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie kwamba tuliposema juu ya kwamba bajeti hii ni bajeti ya kazi na utu, ni kwa sababu tunatazama zaidi namna ya kutatua kero na changamoto hasa zinazowakabili wananchi.

Mheshimiwa Spika, pia naomba vilevile niwape hongera sana na pongezi Waheshimiwa Wabunge hawa kwa sababu ya namna ambavyo wamekuwa wakiziwasilisha hizi hoja na namna ambavyo wamekuwa wakizisimamia, kwa kusema ukweli wakati wote hawapungui katika jambo hili, wakipiga simu, wakiandika *message*, ama wakisema humu Bungeni. Hongereni sana kwa kuwawakilisha vema wananchi katika Majimbo yetu kote nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile wapo ambao wamezungumzia juu ya taa za barabarani, Wabunge wengi sana wameonesha kwamba jambo hili ni jambo muhimu na wamelipa kipaumbele sana. Nimeshakueleza katika bajeti kwamba, jumla ya taa 5,200 tunakwenda kuzinunua, ni wastani wa taa 200 kwa kila Mkoa.

Mheshimiwa Spika, wako hapa Wabunge ambao wamesema, mfano mtani wangu mmoja Mbunge wa Mbogwe, Mheshimiwa Maganga, anasema hana cha kunishukuru kwa sababu hajapata jambo. Nataka nimhakikishie kwamba atapata taa hizi 200 na zitakwenda kumulika pale Mbogwe ili kusudi yale mambo mbalimbali ya kuweza kufanya biashara katika maeneo yale yapatikane.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Massare wa pale Itigi ameomba hizi taa, tutazingatia. Mheshimiwa Olelekaita, yuko

Mama Sitta, Mheshimiwa Kyombo, Mheshimiwa Cherehani, vilevile yuko na Mheshimiwa Saashisha wa pale Hai, wote hawa wameomba taa. Nataka niwahakikishie kwamba tunayo maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, taa zinaleta nuru na taa zinapunguza ajali vilevile, na taa zinapendezesha sana miji yetu. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, tutalifanya hili jambo mapema ili kusudi kama alivyosema Mheshimiwa Maganga, kabla ya mwezi wa 10 wakati tunaingia kwenye *iyena iyena* mambo yawe yameshapendeza ili kusudi tuendelee kuaminiwa na kupata kura za kutosha kutoka kwa wananchi wetu, vilevile kupeleka maendeleo kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge kadhaa wamezungumza juu ya barabara ya Chalinze – Segera. Ni kweli barabara hii ilijengwa miaka ya 1990. Wabunge kadhaa wa Mkoa wa Tanga wamezungumza, Mheshimiwa Shangazi, Mbunge wa Mlalo na Katibu wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi humu Bungeni, huyu amezungumza kwa mapana sana juu ya barabara hii, na ni kweli barabara hii ni finyu.

Mheshimiwa Spika, yuko Mheshimiwa Mnzava, vilevile Mheshimiwa Omari Kigua, Mheshimiwa Ummy, Mheshimiwa *Eng*. Mwanaisha Ulenge, yeye aliendelea na akaongeza na ile *bypass* ya Kiomoni kwa maana ya pale Mkinga – Mlingano. Hii ninataka nimhakikishie tumeshafanya Usanifu wa Kina na baada ya kuwa tumekamilisha Usanifu wa Kina tunaipeleka sasa iweze kuwa ni katika barabara mbadala. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi maana jana alizugumza kwa hisia kubwa ya kwamba ni kwa nini barabara hii haipewi kipaumbele? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa wote niliowataja juu ya barabara hii ya Chalinze – Segera, sasa hivi tunakamilisha *detail design*, tumekamilisha hatua ya kwanza, tunataka tupate usanifu wa kina wa hii barabara. Ni kweli ni finyu, imejengwa miaka mingi, sasa hivi haikidhi tena haja, kwa hiyo tukimaliza usanifu wa kina, hatua inayofuata tunaitafutia fedha ya uhakika ili kusudi barabara hii iweze kutanuliwa. Hii ni barabara kubwa ni barabara

ya kiuchumi nami nimekubaliana nanyi na sisi tunakwenda kuipa kipaumbele pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lililochukua nafasi kubwa sana humu ndani, pamoja na pongezi nyingi ambazo Waheshimiwa Wabunge takribani wote mmetupongeza, na sisi tunashukuru sana kwa kutupa matumaini na kututia moyo kwa kazi kubwa inayofanyika, tunashukuru zaidi namna ambavyo Waheshimiwa Wabunge wote mmetambua kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme mbele ya Bunge hili, ukweli Mheshimiwa Rais ameifanya kazi kubwa na ninyi mna haki pale mliposema sasa kazi iliyobaki ni mimi na timu yangu ya Mheshimiwa *Eng*. Godfrey Kasekenya Msongwe na wasaidizi wetu. Hatuna tunachomdai Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa kweli kazi ameifanya kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hapa limesemwa jambo linalohusu malipo ya wakandarasi. Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia wamesema juu ya jambo hili. Nataka niwape takwimu kiasi na nitasema kwa kiwango fulani juu hata ya hoja ya dada yangu Mheshimiwa Halima Mdee alipozungumzia juu ya *performance* namna alivyoisoma kwa ufasaha sana kutoka katika vitabu vya *CAG*. Nami ninamheshimu, sina tatizo na ninamshukuru kwa ufuatiliaji wake, lakini ninataka niwakumbushe tu kwamba, kuanzia mwaka mwaka 2021/2022 Mheshimiwa Rais ameingia, mpaka hivi leo, jumla ya fedha shilingi trilioni 2.5 zimelipwa kwa wakandarasi hapa kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kazi inaendelea na sisi sote ni mashahidi. Kazi kubwa ya ujenzi katika nchi yetu inafanyika. Unajua niseme, kwa mfano kila mmoja hapa amepongeza juu ya Daraja la Kigongo – Busisi. Daraja la Kigongo – Busisi limejengwa kwa viwango vikubwa na ni daraja la mfano. Sasa, ninawahakikishia, Wakandarasi pale wataendelea kulipwa na wale walichokibakiza ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, hata hawa wakandarasi wetu wa ndani, ukitazama *figures* ambazo walikuwa wakidai wakati huo na *figures* ambazo zinadaiwa hii leo, kila wakati na kila mwezi Wizara ya Fedha imekuwa ikiendelea kutupa fedha, na tunalipa kiwango kwa kiwango.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba bado kuna madeni yanayodaiwa. Wakandarasi wandani wanatudai na wakandarasi wa nje wanatudai lakini jitihada za kulipa zinafanyika. Yapo makubaliano tuliyoyafanya, sisi Wizara ya Ujenzi na wenzetu Wizara ya Fedha, kadri fedha zinavyokusanywa na wao wanatuletea zile fedha sisi tunawalipa wakandarasi wetu na madeni mapya yanazaliwa kwa sababu hatujasimama, kazi ya kujenga nchi yetu inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukumbushane hapa pia, hata tulipojenga *SGR* ni fedha hizi hizi ambazo zinakusanywa, kikapu ni hicho hicho na zinakwenda kujenga katika *SGR*. *SGR* ambayo Watanzania wote leo tunajivunia, Watanzania wote leo tunaona kuwa ni ufahari mkubwa sana, na hiyo ni kazi ambayo imefanywa na Serikali, ni kazi ambayo imefanywa na Bunge hili na ni kazi ambayo imefanywa na Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesema juu ya hata Bwawa la Mwalimu Nyerere. Tumeambiwa hapa juzi na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, ambaye pia ni Waziri wetu wa Nishati, kazi imefanyika kule. Miongoni mwa watu wanaofanya ile kazi inayofanyika kule *contractors*, wasimamizi wanatoka huku huku Wizara ya Ujenzi. Ni katika *performance* hiyo hiyo, kwa hiyo, wametawanyika nchi nzima wanasimamia mambo haya kwa sababu, fedha hizo ni za kwetu wenyewe, zinalipwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumefanya kazi hiyo kama Watanzania wote, na kwa hiyo, tukisema juu ya *performance,* sikatai imesemwa katika vitabu, lakini ni *performance*. Ukiitazama kwa mapana maana yake ni kwamba kazi imefanywa na sisi wote katika nchi. Ndiyo maana tunapongezana kwa miradi hii mikubwa na mizuri iliyofanywa na Serikali ya Chama cha

Mapinduzi ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa heshima kubwa sana nimemwelewa sana dada yangu, Mheshimiwa Halima Mdee. Najua kiu yake ya kutaka kuona kazi kubwa na nzuri ikiendelea kufanywa. Ni mpenda maendeleo, na sina shaka hatashika Shilingi kwa sababu na yeye huwa anapanda *SGR* kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma na kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam na tutamwalika akaone *performance* kubwa ya Daraja la Kigongo – Busisi. Nitatamani sana atembee kwa miguu kilometa 3.2; hakuna Afrika ya Mashariki, ni jambo la mfano.

Mheshimiwa Spika, hapa niwaunge mkono Mheshimiwa Tabasam, Mheshimiwa Musukuma na Wabunge wengine wengi wa Kanda ya Ziwa waliposema kwamba, wanamsubiri kwa hamu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, aende akalifungue lile daraja ambalo linakwenda kuwa ni mfano katika Afrika ya Mashariki na Kati, ambalo ni tunu sasa.

Mheshimiwa Spika, yaani lile ni jambo ambalo sijui tuliweke katika alama zetu za Taifa hivi, maana ni kazi kubwa sana. Ni jambo kubwa sana limefanywa. Kwa hiyo, naona tuyatazame mambo haya kwa upana sana na tusiyatazame haya madogo madogo ambayo yatatufanya tunyong'onyee na tusitembee kifua mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa inaendelea kufanywa na kupitia hili ndiyo hapa sasa nataka nimwombe vilevile mtani wangu Mheshimiwa Kasalali Mageni, bwana, usiwe na wasiwasi mimi nimekusikia. Hawa waliokwambia huko mwanzo, umetumia lugha ya kusema wamekudanganya, nawe sasa mtani, Mheshimiwa Ulega umeingia katika uwongo huo huo; usiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, jambo lipo katika vitabu na ninataka nikuhakikishie nina safari ya Mwanza, tutakwenda mimi na yeye kule kwake Sumve, nitakwenda kulisimamia jambo hili na ninajua hivi sasa watani mnapenda sana maendeleo, mmechoka kufanya ile biashara. Huwa nawatania wakati mwingine na

uniruhusu, katika nchi yetu utani upo, maana wameomba taa nyingi sana, wanakusudia kuwakimbiza fisi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana Mheshimiwa Kasalali amekuwa mkali sana juu ya jambo hili. Ndiyo maana Mheshimiwa Cherehani na Mheshimiwa Kiswaga wamezungumzia sana juu ya taa za barabarani. Najua shida yenu ni kuwafukuza wale jamaa. Mimi nataka asikasirike, sisi tunamhakikishia hataharibikiwa kwa sababu ya barabara hii.

Mheshimiwa Spika, tukimaliza tu hii bajeti, tunafanya *procurement* ya haraka, *advance payment* watapata na tutakwenda kusukuma kwa pamoja watu wa kule Sumve, ili kama tatizo ni hilo tujitahidi kwenda kukutetea. Labda kama wana matatizo yao mengine, hilo sasa ni yeye na wao, lakini mimi nataka nimhakikishie, kwa jambo hili limpe *comfort* mtani wangu, mambo yake yatakuwa mazuri sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile niseme hapa. Nilimsikia ndugu yangu, Mheshimiwa Mnzava, amesema vizuri sana, amesema juu ya Barabara ya kutoka *Old Korogwe* kwenda kwa Mndolwa na tena akagusia mpaka viongozi wa dini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali ya Awamu ya Sita inaheshimu na kuwapenda sana viongozi wa dini. Naomba nianzie hapo. Inaheshimu na kupenda sana viongozi wa dini katika Taifa letu, na ndiyo maana ile barabara aliyoisema ya kutoka *Old Korogwe* mpaka Kwa Mndolwa, amesema Wabunge wameiomba, lakini ikasisitizwa zaidi na kiongozi wa kiroho, Mufti wa Tanzania, *Sheikh* Abubakar Bin Zubeir Bin Ally.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunakwenda kutengeneza hiyo barabara kilometa zile 10 kwa kuonesha msisitizo namna Serikali hii inavyoheshimu dini na inavyoheshimu viongozi wa dini. Pale Kilimanjaro tuna Barabara ya Askofu Shoo, maarufu kabisa, tumeitengea fedha na yenyewe tunakwenda kuweka lami pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule Tabora tuna Kituo cha Hija cha *RC,* Kanisa Katoliki, na kwenyewe tumetengea fedha, tunakwenda kuweka lami pia. Hii ni mifano michache ya namna ambavyo Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, inaheshimu na kuthamini sana viongozi wa dini.

Mheshimiwa Spika, ningependa sana tukubaliane, tutapitisha maombi katika Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, barabara zile zinazoombwa na kusisitizwa sana na viongozi wa dini, ikiwa ni pamoja na ile ya Kituo cha Hija kinaitwa Inafa, pale Tabora, tuzipe majina ya hawa viongozi wetu wa dini ndio, itapendeza sana na itaonesha heshima kubwa namna sisi Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambavyo inathamini sana dini na viongozi wa dini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa lipo jambo pia, limezungumzwa juu ya wakandarasi wa ndani. Namshukuru sana kaka yangu, Mheshimiwa Getere, amelisema vizuri sana jambo hili kwamba, tuwathamini wakandarasi wa ndani na tuwawezeshe. Akasema, kwa nini hatutengenezi sheria na kanuni?

Mheshimiwa Spika, Bunge tayari lilishatengeneza Sheria na tayari tumeshapitisha Kanuni, ipo Kanuni ya 39, Kanuni Ndogo ya Tatu na ya 10, ambapo hii Kanuni ya Manunuzi ni ya Mwaka 2024. Inasisitiza juu ya kuwapa kipaumbele wakandarasi wake wa ndani, lakini inasisitiza vilevile juu ya kuhakikisha miradi. Wale wanaotoka nje kuja hapa ndani tunafanya nao *JV*.

Mheshimiwa Spika, kazi tunayoisubiri hivi sasa ni kuhakikisha kwamba, *documents* za mifumo ya manunuzi, ambayo hii sasa ipo chini ya Wizara ya Fedha na sisi tayari tunafanyanao mazungumzo, ili kusudi wazibadilishe, maana zile kanuni zetu mpya hazijaingia bado katika mfumo ule wa manunuzi.

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie, katika mwaka wa fedha 2024/2025 kwa kuwa, sisi upande wa kanuni tumeshakamilisha, ina maana na wenzetu wa Wizara ya Fedha *PPRA* watakamilisha na sasa tutakwenda kuwapeleka wakandarasi wetu waweze kufanya *JV* na kampuni yoyote

itakayokuja kupata kazi hapa nyumbani Tanzania. Hiyo itawajengea uwezo wa kitaaluma, uwezo wa kifedha na vilevile uwezo wa kivifaa.

Mheshimiwa Spika, hili tumelitengenezea mpaka *formula* kwamba, tutakapofanya hiyo *JV,* mzawa kampuni yake iwe na asilimia ngapi na mgeni kampuni yake iwe na asilimia ngapi, lakini wakati huo huo kwa kuanzia, Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, nimesema na sasa narudia kusema kwamba, katika ile miradi ya dharura iliyofanywa mwaka 2025 uliokwisha, baada ya mvua za *El-Nino* na Kimbunga Hidaya, jumla ya miradi 81 yenye thamani ya shilingi bilioni 566.9 ilisainiwa.

Mheshimiwa Spika, katika miradi hiyo 81 makandarasi wa ndani wamechukua miradi 70 yenye jumla ya fedha shilingi bilioni 414 na hizi fedha wameshalipwa, *advance payment,* zaidi ya shilingi bilioni 80. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, fedha hizi zipo kadiri ya wanavyofanya kazi, wanaleta *certificate,* tunawalipa.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana jana hapa katika mimbari hii nilizungumza juu ya kwamba, tunawapongeza sana makandarasi wetu wa ndani, na nikatolea mfano wakandarasi kadhaa, akiwemo yule ambaye amezungumzwa vizuri hapa, anaitwa *Makapo Contractors*. Yule nilipofanya ziara ya kwenda kukagua fedha hizi, nilikuta kabla hajapewa hata *advance payment*, ameshafika asilimia 25 ya utekelezaji wa ule mradi.

Mheshimiwa Spika, huu ni uthibitisho ya kwamba, wapo wakandarasi wazawa wazalendo, wapo *serious,* wanafanya kazi yao kizalendo na sisi tutaendelea kuwazingatia na tutahakikisha kwamba, tunawaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, leo katika kikao, kwa sababu, ipo hoja hapa ilizungumzwa na Mheshimiwa Getere pia, ya kwamba, kwa nini tusitengeneze mfuko? Mfuko upo, tena upo kwa mujibu wa sheria. Mfuko ule unategemea tozo za Bodi yetu ya Wakandarasi, ambayo mpaka sasa hivi ina shilingi bilioni 4.2, ndiyo ile uliyoiona katika kitabu na Bodi ya Wakandarasi imeingia katika

makubaliano na Benki ya *CRDB* kwamba, wao wanaweka shilingi bilioni nne na *CRDB* inaweka shilingi bilioni nne.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata taarifa hiyo, nimewaambia wataalamu wangu, tunaanzisha hili jambo mchakamchaka wa kuhakikisha kwamba, tunatafuta fedha za kuongeza kwa sababu, *CRDB Bank* ipo tayari, sisi tukiwa na shilingi bilioni 100 na wao wanaweka shilingi bilioni 100. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, hiyo itasaidia wakandarasi wetu wa ndani kupata fedha za uhakika za *advance*, hiyo itasaidia wakandarasi wetu wa ndani. Kuna kitu kinaitwa *big security,* watakuwanayo ya uhakika na kwa hiyo, hata tunapowapeleka katika *JV* na wao watakuwa *comfortable* kwa sababu, wana uwezo. Hili jambo tunakwenda kulifanya tukishirikiana na wenzetu wa Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza humu juu ya ukarabati wa Barabara Kuu ya Dar es Salaam – Kibiti – Lindi. Waheshimiwa Wabunge nataka niwahakikishieni kwamba, jambo hili ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, na hata Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa ametumwa na Mheshimiwa Rais kwenda kukagua barabara ilipokatika, naye akasisitiza maelekezo yale ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, tunakwenda kuifanya kazi hii kwa ufasaha. Pia niwaondoe hofu ndugu zetu wa Mikoa ya Kusini, kazi kubwa kule inaendelea. Hivi leo nataka niwaambie, tuna jumla ya shilingi bilioni 400. Zaidi ya shilingi bilioni 400 zinakwenda kujenga Barabara ya kutoka Mtwara mpaka Mnazi Mmoja, pale Mingoyo na inayotoka Mnazi Mmoja, Mingoyo, inakwenda mpaka Masasi.

Mheshimiwa Spika, hiki ni kitu cha uhakika, kutoka Mtwara mpaka Mnazi Mmoja tumeshasaini na Mkandarasi tumeshampa pesa zake za awali. Baada ya wiki mbili tatu zijazo tunamlipa na mkandarasi wa kutoka Mingoyo, kwa maana ya Mnazi Mmoja, mpaka kule Masasi. Barabara hii ina fedha za uhakika, tunakwenda kuijenga.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niwape uhakika ya kwamba, kazi nzuri na kubwa Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, inaitekeleza katika maeneo yale. Vilevile namshukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Eng. Kasekenya, pale alipoeleza juu ya Barabara ya Newala – Mnevata na yenyewe ipo na inajengwa. Kwa hiyo, hakuna mahali ambapo hapajaguswa, hakuna mahali ambapo pataachwa bila ya kufanyiwa kazi. Nchi nzima inajengwa na tutaendelea kuijenga nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ipo Barabara ya kutoka Dodoma mpaka Iringa. Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati amezungumzia juu ya suala la kutengenezwa kwa *bypass,* ametoa ushauri, kwa nini Kitonga haipati suluhu?

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na takribani watu wote sisi ambao tunatumia barabara hii, pale Kitonga, sasa tunakwenda kutafuta *bypass* na tunaiweka katika bajeti ya mwaka 2025/2026, zitaongezeka kilometa 32, lakini hata zikiongezeka kilometa 32 ni bora zaidi kuliko kwamba, barabara inakatika na baadaye hatuna pa kupita. Kwa hiyo, hili tunakwenda kulitekeleza haraka iwezekanavyo katika mwaka huu wa fedha wa 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile imezungumzwa hapa Barabara ya kutoka Babati – Singida. Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Manyara wameizungumza. Mheshimiwa Asia Halamga kataja majina hapa, Dareda, Katesh mpaka Gehandu. Nataka niwahakikishie, na yenyewe yote tumekubaliana tunakwenda kuifanyia ukarabati.

Mheshimiwa Spika, jana Mheshimiwa Issaay na Mheshimiwa Flatei waliniomba, kwamba nifanye ziara kule Mbulu, kwa ajili ya kwenda kumsukuma yule mkandarasi. Tunakwenda haraka iwezekanavyo. Tutakwenda kusimamia ile Barabara, kwenda kumsukuma yule mkandarasi ambaye, anasimamia eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Barabara ya kutoka Dodoma kuelekea Dar es Salaam, kwa maana ya Morogoro, na yenyewe

imeelezwa hapa. Tutaendelea kuifanyia *maintenance* kadiri tunavyopata fedha.

Mheshimiwa Spika, naomba pia, nijelekeze katika baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao wameonesha nia hapa ya kusema watakwenda kushika shilingi. Yupo Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, namwomba asishike Shilingi kwa sababu, barabara ile aliyoizungumza, ya Litukila – Songea, ile barabara ina pesa za uhakika. Tupo katika hatua ya mwisho ya kupata mkandarasi na baada ya kumpata mkandarasi, basi hata ile *bypass* ya pale Songea na yenyewe ni sehemu ya Mradi ule mkubwa wa Lutikila – Songea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba pia, nimtoe hofu Mheshimiwa Gulamali, ambaye amezungumza hapa akisema kwamba, watangulizi wangu waliahidi barabara kilometa kadhaa. Cha ajabu, mimi naonekana nimekuja kuifuta kabisa barabara yenyewe. Namwomba Mheshmiwa Mbunge sasa atembelee ukurasa wa 278 na 210 atakuta hizi barabara zipo mle. Kwa kuwa, ameisema hapa na sisi tutasisitiza juu ya kuweza kupata, kuanza kuwekwa vipande vya lami ile barabara.

Mheshimiwa Spika, vilevile Waheshimiwa Wabunge kadhaa, yupo mama yangu leo asubuhi amezungumza kusema, Serikali inafanya usanii. Hatufanyi usanii. Kusema ukweli, ipo barabara kule Same, na nilikwenda Same. Niliombwa na Mheshimiwa Mama Malecela Anne Kilango kwamba, twende kule barabara, imekatika, na kweli tulikwenda, tukaikagua ile Barabara ya Ndungu – Mkomazi, pale Same, na tukarudishia ile njia.

Mheshimiwa Spika, sasa barabara ikianza, imeanza, ikiandikwa katika vitabu vya Serikali ni vizuri kuendelea kuisimamia ijengwe, lakini tukizungumza lugha ya kusema tuitoe kabisa kwa sababu, kinachofanyika ni kama usanii, hii siyo kweli.

Mheshimiwa Spika, nadhani jambo la msingi ni Serikali kuendelea kuisimamia. Namshukuru Mheshimiwa Mama Anne Kilango kwa sababu, ameendelea kusimamia juu ya jambo hili. Yeye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati, amenieleza, amenikumbusha tukiwa katika Kamati kwamba hebu isimamie hii

barabara, nami nitaendelea kuisimamia na tutapata hizo tano, 10, 15, 20 mpaka kuendelea na hatimaye barabara ile ya wananchi itawaondolea watu kero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge, Serikali inapoanza maana yake imeanza, na itaendelea kuifanyia kazi hiyo ahadi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa viwanja vya ndege. Tayari Mheshimiwa Naibu Waziri ameelezea baadhi ya viwanja vya ndege ambavyo vilikuwa vimekwama kabisa, lakini niseme tu kwamba, Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya kazi nzuri. Vipo viwanja vya ndege watu walikuwa wameshaanza kukata tamaa, lakini ukweli ni kwamba, vimefufuka. Hata wale wa Tanga, ambao wenyewe wanasema waja leo kuondoka majaaliwa, sasa wamesisitiza wanataka kiwanja cha ndege.

Mheshimiwa Spika, Kiwanja cha Ndege cha Tanga tumeshafanya manunuzi na tumeshapata mkandarasi na kwa hivyo, mkandarasi, tunakwenda kumpa *advance payment* kwa sababu, hela zake ni za uhakika na tunakwenda kuanza kujenga kile kiwanja. Kwa hiyo, Uwanja wa Ndege wa Tanga unakwenda kujengwa vizuri na ndiyo maana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia, alipofanya ziara pale Tanga alisisitiza na kusema anaifungua Tanga kibiashara.

Mheshimiwa Spika, sasa Tanga itapitika kwa njia zote, itapitika upande wa kutoka Bagamoyo mpaka Pangani, Tanga, lakini vilevile itapitika kupitia barabara kubwa ambayo leo mmeizungumza hapa Waheshimiwa Wabunge karibu wote wa mkoa huu wa Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kiwanja cha ndege kitakuwa kimepatikana. Kwa hiyo kuna wengine walitaka kuchukua Shilingi yangu, akina Mheshimiwa *Eng.* Mwanaisha Ulenge, na alisisitiza sana, anaogopa akichukua hii Shilingi mdogo wake kule nyumbani atakuwa hana cha kupika. Basi usichukue, nakuomba kwa heshima kubwa na taadhima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuendelea kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja zote tumezichukue. Ni wengi sana wamechangia, ambao ni 81, na hili ni jambo kubwa sana. Tumelichukua jambo hili na wengi hapa tumekubaliana kwamba tutakwenda kufanya ziara katika maeneo yao mbalimbali waliyoyasema. Nimeyachukua yote yale ambayo wameyasisitiza na tutakwenda kuyafanyia kazi na ziara tutazifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kujenga barabara katika nchi yetu bila ya kuchoka, bila ya kusimama. Naomba kwa heshima kubwa na taadhima Waheshimiwa Wabunge watuunge mkono, watupitishie bajeti hii. Imepanda kwa viwango vizuri, shilingi trilioni 2.2 kutoka shilingi trilioni 1.6, ni ongezeko la zaidi ya 28%.

Mheshimiwa Spika, tutafanya kazi usiku na mchana, hatutachoka na utakwenda kila kona ya nchi yetu. Hapa hapa katika hii miezi miwili iliyosalia tutahakikisha tunafika kadri iwezekanavyo mimi na mwenzagu na wataalamu wetu kuhakikisha kwamba tunakwenda kusaidia kutatua changamoto mbalimbali walizonazo Waheshimiwa Wabunge kwenye majimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe hoja, na ninaomba kwa heshima kubwa na taadhima Waheshimiwa Wabunge watuunge mkono katika hoja hii. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wangeni ambao wamekuja baada ya tangazo la awali la wageni na mengi yaliyofuata.

Wapo wageni wa tatu wa Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila, hawa ni wanachama wa Taasisi ya Taifa Letu, Kesho Yetu kutoka Wilaya ya Tunduma Mkoani Songwe. Karibuni sana. *Makofi)*

Tunaye mgeni aliyetembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, huyu ni Ndugu Prisca Ngusa kutoka Mugumu, Serengeti. Karibuni sana. *(Makofi)*

Basi Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……………………………Sh. 2,451,294,575

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina mshahara wa Waziri, na ninayao majina hapa ya Wabunge wawili wanaoomba nafasi. Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa mujibu wa sera ya nchi, ya Barabara, inasema kwamba mikoa na mikoa inatakiwa kuunganishwa kwa barabara

za lami pamoja na mikoa na wilaya, lakini kwenye baadhi ya maeneo imekuwa tofauti wakati maeneo mengine yameungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikatoa tu mfano wa barabara ya muhimu sana katika kuunga mikoa zaidi ya mitatu barabara ambayo tumekuwa tuisemea kila mara na haipati majibu yanayoridhisha. Barabara itayotoka Fulo kupitia Koromije – Nyambiti – Malya – Shishiyu - Lugulu - Itilima Kisesa – Meatu – Sibiti – Mkalama mpaka Iguguno, ambayo imekuwa ni kilio na ni muhimu sana kwenye kuunganisha mikoa hii na ni muhimu kwa utalii wa Serengeti ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nahitaji maelezo ya kutosha kuhusu barabara hii na barabara nyingine ikiwepo ya Magu – Ngudu mpaka Hungumalwa. Vinginevyo, nitaomba uniruhusu niondoke na Shilingi ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru kwa maelezo ya Mheshimiwa Kasalali Mageni. Barabara hii ya Fulo – Nyambiti – Malya ilikuwa haijakamilika usanifu wake, na kwa hiyo, tunatarajia mwezi Julai mwaka huu tutakuwa tumekamilisha Julai mpaka Agosti. Ni barabara ya kilometa takribani 73, na ni kweli ni barabara muhimu, nakubaliana naye kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tumalize usanifu kisha tutaiwekea bajeti na yenyewe tuweze kuijenga. Namwomba kwa upande wa barabara hiyo, akubaliane nasi tukamilishe usanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile ya upande wa Ngudu – Hungumalwa ambayo ameilalamikia sana kwamba imekuwa ikizungumzwa lakini haipati ujenzi wa lami, hii ya Ngudu – Hungumalwa na yenyewe ipo katika vitabu. Ni kweli iko katika bajeti, nami nimemwelewa sana na ninataka tu nimwombe atuamini na sisi tutakwenda kuifanya hii kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari hii, na *Inshallah* Mwenyezi Mungu atamjalia arudi salama, haya maneno ya kwamba

amekuwa akiambiwa lakini hayatekelezwi, namwomba, sisi tunajua, sisi ni wachungaji na tutaulizwa kwa vile ambavyo tumevichunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ni mahali patukufu. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutakwenda pamoja mimi na yeye mtani. Namwomba kwa heshima kubwa sana asichukue Shilingi yangu, mimi niendenayo, naye atuachie tukaifanye kazi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge ameelewa. Kwa hiyo, ameketi, ahsante sana. Mheshimiwa…*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa unajua haya makofi yamenichanganya kidogo, kwa sababu wakati anaongea nilisikia makofi, sasa hivi amesema hoja ameendanayo, nimesikia makofi. Ninaamini makofi ya sasa yanamhusu Mheshimiwa Waziri kwamba amemridhisha Mheshimiwa Mbunge.

Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Halima James Mdee. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hoja yangu inatokana na hoja ya madeni ya wakandarasi na Wahandisi Washauri; sijaridhika na majibu ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa. Tukirejea kwa ajili ya uzito wake, Kamati yako ya Bunge imesema kwamba imebaini kwamba *TANROADS* imekosa uwezo wa kulipa madeni ya wakandarasi na Wahandisi Washauri wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2025 *TANROADS* ilikuwa na jumla ya deni lililozalishwa la shilingi trilioni 1.299. Katika deni hilo shilingi bilioni 137 ni deni la wakandarasi na wahandisi wa ndani na shilingi bilioni 974 ni deni la wakandarasi na Wahandisi Washauri wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kusema kwamba katika hayo madeni shilingi bilioni 652 ni deni la miradi iliyokamilika. Kwa hiyo, kwa deni hilo kutokuendelea kulipwa riba

inazidi kuongezeka na inaathiri uchumi wa wakandarasi wa ndani na vilevile kuathiri miradi ya maendeleo ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelisema hili kwa nini? Waziri ameeleza hapa kwamba tokea mwaka 2021/2022 madeni yalishalipwa shilingi trilioni 2.5, ni sawa kabisa; lakini dawa ya deni unalipa, kwa sababu kila mwaka tunapopitisha bajeti na kuelekeza miradi ya maendeleo kila bajeti ama kila mradi unakuwa umetengewa kiasi chake. Sasa mradi unaweza usifanikiwe kama Serikali itakuwa imekusanya makusanyo pungufu ya kile ambacho kilitarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo amerejea kwa mwaka mzima wa 2023/2024, ripoti iliyotoka Machi mwaka huu, tulitakiwa tukusanye shilingi trilioni 44.3 tukakusanya shilingi trilioni 46.5. Ukija taarifa ambayo tumepewa mwezi huu Januari na Wizara ya Fedha, ilikuwa mpaka Januari tukusanye shilingi trilioni 29.1 nadhani, tumekusanya shilingi trilioni 29.3; yaani tunakwenda vizuri kimakusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wakandarasi hawa hawalipwi, katika ripoti ya Machi mwaka huu riba ilikuwa shilingi bilioni 55 kwa mwaka 2023/2024. Sasa hivi tunavyozungumza mpaka mwezi wa Nne, hii juzi riba imeongezeka kutoka shilingi bilioni 55 kwa sababu ya wakandarasi kutokulipwa mpaka shilingi bilioni 136.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili jambo ni kubwa, na Kamati imeeleza kabisa kwamba changamoto kubwa inayosababishwa na mlolongo wote huu ni zile fedha ambazo zimelindwa kisheria zinatakiwa zipelekwe Mfuko wa Barabara, hazipelekwi. Imeelezwa hapa, na Wajumbe wa Kamati wamezungumza na Kamati imezungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2024 hazikupelekwa shilingi bilioni zaidi ya 600. Hazina imekusanya, imepeleka shilingi bilioni 800, bilioni 600 imebaki nayo. Sasa hivi tunavyozungumza mwezi huu wa Tano, imekusanya shilingi bilioni 800 na kitu imepeleka shilingi bilioni 200. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo mimi najua

likifanikiwa hata Mheshimiwa Waziri mwenyewe inamsaidia katika utendaji wake wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali itoe *commitment* ya kweli kwenye jambo hili ili tuweze kuisaidia hii nchi iweze kwenda. Wakandarasi walipwe, na vilevile miradi iweze kutekelezwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri akishindwa kunipa *commitment* ambayo ni yenye umakini sasa kuelekea bajeti kuu, nitatoa shilingi. Ninashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naona kama wote mnataka kusimama. Aah, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Lukuvi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa, Mheshimiwa Halima alitoa hii hoja wakati anachangia na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi amejitahidi kumweleza vizuri sana na ametueleza wote kwamba, kama nchi fedha hizi hazina alama kwamba hizi ni za maji, za mifugo zinakusanywa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi tafsiri yake ni ujenzi wa miradi yote. Maana huyu anasimamia wakandarasi wanaojenga Bwawa la Nyerere, wanaojenga daraja, wanaojenga reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Halima, kama Mheshimiwa Rais asingeamua kulipa fedha zote kwa mkupuo wa ujenzi wa Bwawa la Nyerere, riba ingekuwa kubwa kuliko hii ya barabara. Kama asingeamua kulipa kukamilisha mradi wa mkubwa wa daraja kwa wakati mmoja, riba ingekuwa kubwa sana kwa sababu miradi ile ni mikubwa. Kama asingeamua kujenga reli na kulipa kwa *cash* kwa mkupuo riba ingekuwa kubwa sana kuliko hizi shilingi bilioni 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kumhakikishia Mheshimiwa hili kwa niaba ya Serikali, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati ametuhakikishia kwamba Bwawa la Nyerere limekamilika. Bila shaka linatupa pumzi ya fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa hapa na Waziri wa Ujenzi kwamba daraja lile limekamilika na fedha zimelipwa. Linatupa nafasi ya pumzi ya fedha zile ambazo tulikuwa tunalipa nyingi kwa wakati mmoja sasa zitakwenda kutengeneza zile barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninataka kumhakikishia Mheshimiwa Halima, mpaka wakati huo, na tuna miezi miwili sasa mpaka kufika bajeti, atakapokuja kuzungumza tena kwenye bajeti ya mwezi wa Sita takwimu zitakuwa zimebadilika. Namhakikishia hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri amesema kuanzia mwezi huu, bahati mbaya sana, Mwenyezi Mungu naye ametupa hali ya hewa njema yenye mvua nyingi. Leo Malinyi, Ulanga kwa Mheshimiwa hapa mwaka 2024 tumetumia zaidi ya shilingi bilioni 800 kwa dharura, na zote zilikuwa ziingie kwenye bajeti. Nataka kumhakikishia kuwa Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, Serikali ya Awamu ya Sita itasimamia ili kuhakikisha kwamba barabara hizi na wakandarasi wanalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepanga wenyewe Bungeni, tumeishauri Serikali na Serikali hii ni sikivu, nasi tusingependa kufanya barabara zisikamilike kwa sababu tumepanga wenyewe. Kama tulikuwa na nia zisikamilike, tusingeweza kuweka *contractors*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kumhakikisha Mheshimiwa Halima Mdee mdogo wangu, rafiki yangu kwamba Serikali itafanya kazi hii kama ilivyopanga. Ipo kwenye Ilani na tutajitahidi sana. Kama alivyoahidi, bila shaka mwezi Juni ataona kwa sababu yupo hapa hapa, takwimu zitakuwa zimebadilika kidogo, ni kwa sababu tu sasa tunakwenda kwenya afueni, miradi mikubwa na mzigo mkubwa wa Serikali sasa umepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka tu kumwomba tu Mheshimiwa Halima atupe subira, katika miezi hii miwili tumejipanga vizuri kama Serikali ili kuhakikisha kwamba tunapunguza deni kubwa la wakandarasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, naona umesimama tena.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya Bwawa la Mwalimu Nyerere mimi nilikuwa kwenye Kamati ya Bajeti…

**MWENYEKITI:** Ngoja, kwenye ngazi hii ukishasimama Mheshimiwa Halima huelezi tena hoja kwa sababu ulishaeleza awali. Kwa hiyo, sasa hivi unasimama kwamba majibu hayajakuridhisha, unashika shilingi. Ama umesimama kusema nimeridhika na majibu, unaketi. Kwa hiyo, kama unataka kuungwa mkono, unatoa hoja Wabunge wakuunge mkono.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu hayajaniridhisha. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono ili hili jambo tulijadili kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Wamefika 10 hao? Hawajafika 10. Haya, ahsante. Basi hawajafika 10 Mheshimiwa. Kwa hiyo, hoja haijaungwa mkono. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ufafanuzi umetolewa wakati wa Kamati ya Matumizi, wakati Mheshimiwa Waziri akitoa ufafanuzi hapo ameeleza kwamba ujenzi ni ujenzi, na akatoa mfano wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, kwa sababu fedha hizi alizokuwa anazizungumzia Mheshimiwa Halima kwenye hoja yake ni fedha ambazo zimetajwa matumizi yake. Sasa yale ya Bwawa la Nyerere hayawezi kuwa sehemu ya ule ujenzi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hapa hii Sheria ya Barabara na Tozo ya Mafuta, Sura Namba 220, inahusu ujenzi ambao unamhusu Waziri wa Ujenzi ambaye anashughulika na barabara. Sasa ya kule ujenzi mwingine unaweza kuwa sasa nao unaitwa kweli ni ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, lakini ni dhahiri haupo chini ya muktadha uliokusudiwa na ile sheria ambayo ilikuwa inatajwa hapa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nimeona niliweke sawa pamoja na kwamba tupo kwenye Kamati ya Matumizi ili tuwe tumeweka sawa jambo ambalo lipo kisheria. Kwa hiyo, ufafanuzi Mheshimiwa Waziri ameutoa na Wabunge mmefanya maamuzi. Tunaendelea sasa.

Waheshimiwa Wabunge, zimesalia pungufu ya dakika 10, kwa hiyo tunaingia kwenye kupitisha mafungu.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 98 – Wizara ya Ujenzi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……..……………………..Sh. 2,451,294,575
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*………......Sh. 817,115,660
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*……..……Sh. 648,329,550
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*.....Sh. 292,597,500
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*…….Sh. 453,309,400
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*……………………..Sh. 367,765,780
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit*…………………....Sh. 288,186,500
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*………..……..……..…….Sh. 233,530,750
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*..…..Sh. 330,013,140
Kifungu 2002 – *Technical Services Division*…........Sh. 26,696,151,045
Kifungu 2005 – *Roads Division*………..……..…....Sh. 57,363,261,665
Kifungu 5002 – *Safety and Environment Unit*….……Sh. 465,969,435
Kifungu 6001 – *Airport Construction Unit*………………..Sh. 60,745,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 98 - Sekta ya Ujenzi**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*……..….Sh. 246,371,400
Kifungu 2002 – *Technical Services Division*….…....Sh. 53,105,214,000
Kifungu 2005 – *Roads Division*…….…….……..…...Sh. 1,791,136,171,096
Kifungu 5002 – *Safety and Environment Unit*...…....Sh. 1,370,147,000
Kifungu 6001 – *Airport Construction Unit*……….Sh. 343,869,654,504

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona mmesimama kabla. *(Kicheko)*

Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Mtoa Hoja, taarifa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake, hivyo naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni. Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka 2025/2026 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwahoji na ninyi wengi wenu kusema mnaafiki, basi nitumie fursa hii kutangaza rasmi kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepitisha rasmi Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hivyo, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, lakini pia Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote chini ya Wizara hii, na tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa yale ambayo mmewaahidi Wabunge kupitia bajeti yenu na vilevile yale mliyowaahidi Wabunge wakati wa ufafanuzi wa hoja ambazo wamezileta mbele yenu kutoka kwa wananchi wanaowawakilisha.

Pia, natumia fursa hii kuwapongeza sana Kamati yetu kwa namna ambavyo huwa inasimamia Wizara hii. Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote tunawashukuru sana kwa kazi nzuri na Wabunge wote kwa kweli Wizara hii imepata wachangiaji wengi sana kuashiria kwamba, kwanza kazi inafanyika.

Wengi wenu mmeanza kwa kupongeza kwanza jitihada za Serikali na mambo yanayoendelea huko. Ni dhahiri kwamba, Wizara hii inahitaji fedha nyingi zaidi kuliko uwezo wa nchi, lakini yote hayo mmeyaeleza kwa sura ambayo inaonesha kwamba bado upo uhitaji mkubwa sana wa kuhakikisha Wizara hii inapata fedha za kutosha.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kipindi hiki cha bajeti na sisi tuendelee kutafakari namna gani mapato ya Serikali yataongezeka, tuendelee kubuni na sisi vyanzo ili tuishauri Serikali Wizara hii ipate fedha nyingi zaidi na barabara kwenye maeneo yetu ziendelee kujengwa ikiwa ni pamoja na zile ambazo zimeharibika. Kwa mujibu wa Mheshimiwa Kuchauka, anaona kule kulikoharibika kidogo kungesubiri ili na wengine waonje lami kidogo, lakini uhalisia ni kwamba vyote viwili lazima viende pamoja kwa sababu hii ambayo imetengenezwa, isipokarabatiwa maana yake tutaanza tena ile ya usipoziba ufa utajenga ukuta.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, yote mliyoyasema, Mheshimiwa Waziri amesema ameyachukua na ataleta majibu, na kwa yale ambayo hayahitaji majibu, basi bila shaka kwa sasa kwa sababu tunayo Wizara ambayo inashughulikia mipango, basi bila shaka zitaingia kwenye mipango, hizo barabara za kutoka kwenye maeneo yetu; na kwa sababu tunajua Bunge hili pia tutajadili Dira, basi hayo nayo tutayasema kwa sura hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kuna Mwongozo ambao uliombwa na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira kuhusu kauli ya Naibu Waziri, Mheshimiwa Patrobass Paschal Katambi akijibu swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Jasson Rweikiza katika swali la msingi namba 196.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 2 Mei, 2025 katika Kikao cha 16 cha Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge, Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira aliomba Mwongozo wa Spika kuhusu kauli iliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Patrobass Katambi. Naibu Waziri alikuwa akijibu swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Rweikiza katika swali la msingi namba 196.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dkt. Rweikiza katika swali lake la pili la nyongeza kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu aliuliza ifuatavyo:-

"Katika ajira chache zilizopo, Serikali labda unakuta *TRA* au jeshini au wapi wanaajiriwa vijana nafasi 200, nafasi zinalalamikiwa kwamba zinaenda sehemu moja ya nchi au sehemu chache za nchi, unakuta mkoa katika nafasi 200 unaambulia nafasi moja au mbili. Hili likoje? Serikali inalishughulikia vipi?"

Waheshimiwa Wabunge, swali hilo lilijibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri kama ifuatavyo:-

"Mheshimiwa Spika, kwanza msingi wa ajira umekuwa *well-founded* au umejitika vizuri zaidi katika msingi wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 13 ambayo inaitaka Serikali au mamlaka zozote za Serikali zilizopo na zilizoanzishwa kwa mujibu wa katiba kutoa nafasi zozote za utumishi wa nchi bila upendeleo wowote; na kwa msingi huo, hata Sheria ya Utumishi wa Umma na michakato yote ya kiajira ikiwa ni pamoja na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini na Sheria ya Utumishi wa Umma zinakataza… zote za ubaguzi." Sasa hapa ninadhani kulipaswa kuwa na neno aina.

"Mheshimiwa Spika, inapotokea pengine mkoa mmoja umepata nafasi mbili au tatu, siyo tatizo la kwamba wamepangiwa hivyo, isipokuwa inaweza ikawa ni ule ushindani watu mmejitokeza, mkoa fulani walikuwa wameamka kielimu wakajikuta wamekamata nafasi nyingi zaidi, lakini hakuna msingi wowote wa upendeleo katika utoaji wa ajira za sekta ya umma." Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na majibu hayo Mheshimiwa Lugangira aliomba Mwongozo wa Spika kwa kutumia Kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, aliuliza kama ifuatavyo:-

"Ningependa kufahamu, je kauli ile ni sawa, kwamba mikoa ambayo haipati watu wengi kwenye ajira Serikalini kwamba ni kwa sababu mikoa hiyo ina mwamko wa chini kielimu?"

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maombi hayo ya mwongozo nilitoa maelezo kwamba nitarejea majibu ya Naibu

Waziri kwenye *Hansard* ili niweze kujiridhisha kama kauli hiyo inaruhusiwa ama hairuhusiwi.

Nimeipitia *Hansard* na nimeona maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Rweikiza na vilevile nimepitia majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu kwa swali la pili la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Rweikiza.

Waheshimiwa Wabunge, *Hansard* inaonesha kuwa swali la pili la nyongeza lilitokana na maelezo ya Serikali kuwa ajira zote zinazotangazwa na Serikali na mamlaka mbalimbali za Serikali zinatolewa kwa watu wanaoomba kazi bila ubaguzi wowote. Maelezo hayo ya Serikali yalieleza zaidi kuwa msingi huo umewekwa katika Katiba pamoja na Sheria za Kazi na Ajira.

Vilevile, Mheshimiwa Naibu Waziri alieleza kuwa ajira zimekuwa zikitolewa kwa kushindanisha watu wanaoomba ajira. Kingine alichogusia Mheshimiwa Naibu Waziri ni kuwa kutokana na ushindani huo, wapo watu wa baadhi ya maeneo wamekuwa wakijitokeza kuomba ajira na maeneo mengine wamekuwa na mwamko hafifu wa kuomba ajira Serikalini na kusababisha watu wa baadhi ya maeneo hayo kutoajiriwa Serikalini.

Aidha, alieleza kuwa ajira hizo hupatikana kwa ushindani sawa kwa watu wote wanaoomba ajira zinazokuwa zimetangazwa. Baada ya kutafakari maombi ya mwongozo huu, na baada ya kupitia *Hansard,* na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 51 na 53 ya Kanuni za Kudumu za Bunge kuhusu maswali ya nyongeza, nimeridhika kwamba majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri yalikidhi kiu ya Mheshimiwa Rweikiza ya kupata majibu ya swali lake kutokana na kujibiwa kikamilifu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Ibara ya 13(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na sheria zinazosimamia kazi na ajira nchini zinakataza ubaguzi wa aina yoyote katika masuala yanayohusu ajira.

Vilevile, kwa mujibu wa sheria hizo Serikali haina utaratibu wa kuajiri kwa kutumia kigezo cha ubaguzi, bali kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa. Ajira Serikalini huzingatia ushindani wa wanaoomba kuajiriwa na pia taratibu hizo zinahakikisha kuwa ushindani huo unakuwa wa wazi kwa watu wote wanaoomba kuajiriwa.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kutoa wito kwa wananchi wote kwa ujumla kuendelea kujitokeza kuomba kuajiriwa na Serikali kila nafasi za ajira zinapotangazwa. Nafasi za kazi Serikalini zipo wazi kwa kila Mtanzania mwenye sifa. Vilevile, utaratibu unaotumika kupata waajiriwa wapya ni wa kuwashindanisha watu wote wanaoomba ajira kwa usawa bila kujali maeneo wanayotoka, kabila, rangi, dini, jinsia au hali yao ya maisha.

Hivyo basi, mwongozo wangu ni kwamba maneno aliyoyatumia Mheshimiwa Naibu Waziri hayakulenga kuonesha kuwa kuna ubaguzi kwenye nafasi za ajira, bali alikuwa anasisitiza na kuwahamasisha wananchi wa maeneo mbalimbali nchini kuomba ajira kila zinapotangazwa na Serikali na kuwahakikishia kwamba mchakato wa ajira Serikalini ni wa wazi na hauna ubaguzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwongozo wangu kwa kile kilichokuwa kimeombwa na Mheshimiwa Neema Lugangira. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, nnawashukuru sana kwa ushiriki wenu katika siku hii ya leo katika Shughuli zetu za Bunge. Kwa kusema hivyo, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.52 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 7 Mei, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*